# MWONGOZO WA RIPAT

## Jitihada Shirikishi za Kuleta Mageuzi ya Kilimo Vijijini

*J.M. Vesterager, Mfuko wa Hisani wa Rockwool, Denmark*
*D. Ringo, C. W. Maguzu na J.N. Ng'ang'a, RECODA, Tanzania*



## Wasifu wa kitabu hiki

‘Huu ni mwongozo mzuri sana wa hatua-kwa-hatua na rahisi kufuata unaohusu namna mashirika yanayofanya kazi na wakulima wadogo wadogo yanavyotakiwa yafanye kazi zao. Kitabu hiki ni rasilimali ya lazima kwa watoa huduma ya ugani wote na wafanyakazi wote wa maendeleo vijijini kuwa nayo, iwe wanatoka serikalini au taasisi zisizo za kiserikali. Kwa muda mrefu hapajawahi kuwa na mwongozo wowote nchini Tanzania wa kuongoza kazi ya ugani. Mwongozo huu kwa hakika utaziba pengo hilo.’

*Profesa Amon Z. Mattee, Idara ya Elimu ya Kilimo na Ugani,*
*Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro, Tanzania.*

‘Katika wilaya za Arumeru na Karatu nilishuhudia wakulima wakitumia mfumo wa RIPAT kuongeza tija na kipato chao kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji wa ndizi; kuboresha kiwango chao cha uvumbuzi, ushiriki na umiliki wa miradi yao; na hivyo kubadili maisha yao. Mfumo pia umetatua suala la utegemezi kwa wafadhili wa wakulima na uhimizaji wa matumizi ya kanuni iliyo bora kabisa ya kujitegemea katika maendeleo yao.’

*Mh. Isidore Leka Shirima, Mkuu wa Mkoa mstaafu*
*wa Arusha, Tanzania*

# Mwongozo wa RIPAT

## Jitihada Shirikishi za
## Kuleta Mageuzi ya Kilimo Vijijini

J.M. Vesterager, Mfuko wa Hisani wa Rockwool, Denmark
D. Ringo, C. W. Maguzu na J.N. Ng'ang'a, RECODA, Tanzania

**Mfuko wa Hisani wa Rockwool, Denmark**

*Hakimiliki © Rockwool Foundation, 2013*

Kitabu hiki kinaweza kunakiliwa bure na kusambazwa kwa namna isiyo ya kibiashara, kwa ridhaa ya mmiliki.

**Kunukuu:**
Vesterager, J.M., Ringo, D., Maguzu, C. W., Ng'ang'a, J.N. (2013) - Mwongozo wa RIPAT: Jitihada Shirikishi za kuleta Mageuzi ya Kilimo Vijijini, Copenhagen: Mfuko wa Hisani wa Rockwool.

**Shukrani**

Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa shirika lisilo la kiserikali la Denmark PULS (Projekt U-landshjælp til Selvhjælp), shirika ambalo hatimaye miradi yake imepelekea kupatikana dhana ya RIPAT (angalia maneno ya utangulizi kuhusu maelezo ya historia ya RIPAT).

Tunapenda pia kuwashukuru wakulima, wawakilishi wa serikali za mitaa na watu wengine waliochangia kuanzishwa mbinu ya RIPAT tangu 2005. Kwa kipekee tunamshukuru Mkuu wa Mkoa wa Arusha mstaafu, Mh. Isidore Leka Shirima, na pia Wakuu wa Wilaya za Arumeru, Karatu na Korogwe kwa ushirikiano mzuri na msaada wao kwa miradi ya RIPAT iliyotekelezwa katika maeneo yao ya utawala.

Tunapenda kumshukuru ndugu Peder Nørfelt Lund kwa mchango na ushauri wake wakati wa mchakato wa kupanga na kuandika Mwongozo huu wa RIPAT.

Mwisho tunapenda kutambua vema msaada wa hali na mali tulioupata kutoka Ubalozi wa Denmark nchini Tanzania kwa nyakati mbali mbali tangu tulipoanza 2005 wakati Carsten Nilaus Pedersen akiwa Balozi. Tena mnamo 2011, Balozi Bjame Henneberg Sørensen alitusaidia kupanga kikao Dodoma ambacho Waziri wa Kilimo alidokezwa juu ya mradi wa RIPAT, na hatimaye, katika miezi ya mwishoni, Balozi Johnny Flentø aliwezesha maandalizi ya uzinduzi wa Mwongozo huu wa RIPAT uliofanyika mnamo Machi 2013, jijini Dar es Salaam sambamba na uzinduzi wa kitabu cha *Chaguo la Mkulima-Tathmini ya mtazamo wa uenezaji wa teknolojia ya kilimo Tanzania*.

*Mfuko wa Hisani wa Rockwool na RECODA*

Michoro: Goodwill Manson Chomo, OMEGA Arts, Arusha, Tanzania.

Imetafsiriwa kwa Kiswahili na RECODA, na kuhaririwa na Mbarwa Lemilia Kivuyo.
Mwongozo huu ni toleo la kwanza la kazi kubwa sana inayoendelea. Maoni na mrejesho vinakaribishwa kutoka kwa watumiaji na yatumwe kwa:
Mfuko wa Hisani wa Rockwool
Kronprinsessegade 54, 2. tv.
1306 Copenhagen K,
Denmark Baruapepe:
ripat@rockwool.org Tovuti:
www.ripat.org

## *Kuhusu Mfuko wa Hisani wa Rockwool*

Taasisi hii ya kutoka Denmark ilianzishwa mwaka 1981. Kazi zake hulenga maeneo mawili makuu:

1. *Utafiti* wa masuala ya uchumi wa jamii na matatizo yanayokabili mataifa ya Magharibi na mataifa yanayoendelea. Lengo la utafiti huu ni kuongeza ufahamu zaidi, na ubora wa majadiliano ya umma na kuweka misingi mizuri kwa ajili ya maamuzi yanayofanywa na wanasiasa.
2. *Miradi* inatekelezwa kwa ajili ya kuchangia uelewa/ufahamu na kutengeneza mifano kwa ajili ya maendeleo endelevu. Kwa hiyo miradi ya maendeleo inalenga sana uvumbuzi, uandikaji na usambazaji wa mbinu bora.

Mfuko wa Hisani wa Rockwool
Kronprinsessegade 54, 2. tv.
1306 Copenhagen K, Denmark
Simu: +45 4656 0300
Barua pepe: rockwool.fonden@rockwool.org
Tovuti: www.rockwoolfoundation.org

ROCKWOOL FONDEN
ROCKWOOL FOUNDATION

## Kuhusu RECODA

RECODA (Research, Community and Organizational Development Associates) ni AZAKI iliyopo Tanzania. Ilianzishwa mwaka 2000 ikilenga kuziba pengo la teknolojia katika maendeleo kupitia utafiti, ushauri-elekezi, kujenga uwezo na kuwezesha miradi ya kijamii. Mwanzoni kazi kubwa ya RECODA ilikuwa kutoa ushauri-elekezi kwa mashirika ya maendeleo. Kuanzia 2006, kazi kubwa ya RECODA imekuwa ni kuunda mfumo wa RIPAT. RECODA ina idara tatu:

1) *Idara ya maendeleo ya uchumi wa jamii* ambayo inaratibu miradi ya RIPAT na miradi mingine inayotekelezwa na RECODA
2) *Idara ya "akademia" ya RECODA* ambayo hutoa mafunzo yanayoandaliwa kulenga uhitaji wa wawezeshaji wa maendeleo ya vijijini ili waweze kuanzisha miradi kama RIPAT na kutekeleza maendeleo kwa ujumla
3) *Idara ya Ufuatiliaji na Udhibiti wa Ubora* ambayo hufanya zoezi la kuangalia ubora na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya RIPAT.

RECODA
Viwanja vya Nane Nane Themi– Njiro,
S.L.P. 10633, Arusha
Tanzania
Simu +255 27 2549350/ +255 0768 224052
Barua pepe: info@recodatz.org au recoda11@gmail.com
Tovuti: www.recodatz.org

RESEARCH, COMMUNITY AND ORGANIZATIONAL DEVELOPMENT ASSOCIATES
RECODA
BRIDGING TECHNICAL GAP

## Kuhusu Waandishi

**Jens M. Vesterager** ni Meneja wa Programu (Uhakika wa Chakula na Kuondoa Umaskini) katika Mfuko wa Hisani wa Rockwool. Ana shahada ya uzamili (1994) na uzamivu (2001) katika kilimo (lishe ya chakula na rutuba ya udongo) kutoka chuo kikuu cha Copenhagen (kitivo cha Sayansi ya Uhai). Utafiti wake (shahada yake ya uzamivu na kuendelea) na mafunzo yamelenga mifumo ya uzalishaji wa zao la mahindi katika maeneo kame ya Afrika na matokeo ya kuchanganya na mikunde, kuzungusha mazao, uhifadhi maji, lishe ya mimea kwa uzalishaji kwa ujumla. Kati ya mwaka 2003- 2008 alifanya kazi kama mshauri mwandamizi/meneja programu katika shirika la Denmark liitwalo Adventist Development and Relief Agency, akiratibu na kusimamia miradi kadhaa ya msaada na ya maendeleo katika nchi saba za Afrika akifanya safari nyingi kutembelea miradi. Kazi hiyo pia ilihusisha kujenga uwezo wa mashirika yasiyo ya kiserikali (AZAKI) ambayo yalishiriki kutekeleza miradi hiyo. Tangu mwaka 2008 amefanya kazi Mfuko wa Hisani wa Rockwool na amewajibika katika miradi ya RIPAT Tanzania na miradi mingine ya maendeleo katika nchi nyingine sita.

**Dominick Ringo** ni Mkurugenzi Mtendaji wa RECODA ambaye amefanya kazi kwa miaka tisa. Ana stashahada ya uzalishaji mazao (1988), shahada ya Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) na shahada ya uzamili ya Uratibu wa Mifumo ya Mazingira na kubobea katika masuala ya uharibifu na urutubishaji wa udongo kutoka International Institute for Aerospace Survey and Earth Sciences (ITC) Uholanzi (1999). Awali alifanya kazi na Wizara ya Kilimo Tanzania kama mtafiti katika Idara ya Udongo, Uyole (Kanda ya Nyanda za Juu Kusini) na baadaye katika Chuo cha Utafiti cha Selian (Kanda ya Kaskazini). Akiwa Wizara ya Kilimo, alihusika na usimamizi wa rutuba ya udongo, uchunguzi wa udongo, kilimo mseto, mifumo ya kilimo na kilimo hifadhi. Pia alihudumu kama mkufunzi wa kilimo katika uzalishaji mazao, chuo cha Wizara ya Kilimo cha Uyole. Akiwa RECODA amefanya kazi kama mshauri wa kubuni, kutekeleza na kutathmini miradi na pia kujenga uwezo wa mashirika, uchambuzi wa sera na utetezi. Amechangia kubuni miradi ya RIPAT na kusimamia utekelezaji wake. Ameandika uchunguzi kifani wa Wilaya ya Karatu uliochapishwa katika kitabu kiitwacho *Kilimo cha Uhifadhi kama inavyoendeshwa Tanzania (2007)* na alichangia uandishi wa kitabu cha *Kilimo cha Uhifadhi: Mwongozo wa wakulima na watoa huduma za ugani Afrika*.

**Catherine W. Maguzu** ni Mshauri Mwandamizi na Mkurugenzi wa Programu RECODA ambako amefanya kazi kwa miaka tisa katika kubuni, kutekeleza na kutathmini mfululizo wa miradi ya RIPAT na miradi inayofanana na hiyo. Ana shahada ya Maendeleo ya Jamii (1999) na shahada ya uzamili katika Maendeleo ya Kiuchumi ya Jamii (2011). Hapo awali alifanya kazi kwa miaka minne kama mratibu wa afya na lishe katika wilaya tano za Kenya chini ya mpango wa uhakika wa chakula. Ana uzoefu wa miaka 12 kama mshauri wa maendeleo katika kufundisha, utafiti wa masuala ya uchumi wa jamii, uratibu miradi na maendeleo ya jamii. Ameandika uchunguzi kifani wa Wilaya ya Arumeru uliochapishwa kwenye kitabu kiitwacho *Kilimo cha Uhifadhi kama inavyoendeshwa Tanzania (2007)* na

alichangia uandishi wa kitabu cha *Kilimo cha Uhifadhi: Mwongozo wa wakulima na watoa huduma za ugani Afrika*.

**Josephine N. Ng'ang'a** ni mhitimu katika fani ya kilimo, ana shahada ya kwanza ya kilimo cha mbogamboga na ya uzamili katika sayansi ya udongo na usimamizi wa ardhi. Amefanya kazi na kampuni kadhaa binafsi zikiwemo za kilimo cha maua, Tropiflora (K) Ltd, kampuni ya mbegu za mbogamboga Regina Seeds (K) Ltd na SVS Holland. Baadaye alijiunga na shirika lisilo la kiserikali la RUDECT (Dar es Salaam) kama Afisa Miradi akiwa na jukumu la kusimamia miradi ya maliasili na mazingira. Alijiunga na RECODA kama Meneja wa Miradi ya uchumi ya kijamii na akashiriki kubuni na kutekeleza mlolongo wa miradi ya RIPAT. Ana uzoefu wa miaka 21 katika kuendeleza biashara ya kilimo, usimamizi wa miradi, ufundishaji na ushauri-elekezi katika maendeleo.

# YALIYOMO


Shukrani iv

Kuhusu Mfuko wa Hisani wa Rockwool na RECODA v

Kuhusu Waandishi vi

Dibaji xii

Namna ya kutumia mwongozo huu xvii

**Sehemu ya 1: Mwongozo kwa shirika linalotekeleza mradi 1**

SURA YA 1: Utangulizi kuhusu RIPAT na vipengele vyake vikuu 3

SURA YA 2: Mpangilio wa mradi wa RIPAT na majukumu ya watendaji wakuu 11

SURA YA 3: Shughuli za awali kabla ya mradi 15

Hatua ya 1 Uchaguzi wa maeneo yanayofaa kwa mradi 15

Hatua ya 2 Mikutano ya utambulisho kwa viongozi wa serikali za mitaa 15

Hatua ya 3 Utafiti wa awali na wasilisho ya kwanza ya kapu la uchaguzi 19

Hatua ya 4 Mchanganuo wa mradi na maandalizi ya mradi 24

SURA YA 4: Kuanzisha mradi 25

Hatua ya 1 Kukutana na maafisa wa wilaya katika ngazi ya makao makuu ya wilaya 25

Hatua ya 2 Kukutana na Kamati ya Maendeleo ya Kata kwenye makao makuu ya kata 27

Hatua ya 3 Uhamasishaji na ukusanyaji wa jamii kwenye mkutano kwa kila kijiji 27

Hatua ya 4 Kuunda vikundi vya RIPAT 32

**Sehemu ya 2: Mwongozo wa Mwezeshaji wa Kikundi 35**

SURA YA 5: UTEKELEZAJI 37

Hatua ya 0 Kazi yako kama mwezeshaji wa kikundi 37

Hatua ya 1 Mchakato wa Kuzoeana: Siku ya kwanza pamoja na kikundi 41

Hatua ya 2 Uchambuzi wa matatizo na uwezekano wa kupata matarajio ya kweli 42

Hatua ya 3 Uchaguzi wa viongozi wa kikundi 47

Hatua ya 4 Kuandaa Katiba ya kikundi 48

Hatua ya 5 Kukuza mshikamano na uwezo wa kikundi 56

Hatua ya 6 Kuimarisha utetezi stadi wa vikundi 58

Hatua ya 7 Kuchagua shamba la kikundi 60

Hatua ya 8 Kufanya tafiti linganishi 65

Hatua ya 9 Kuunda kamati ndogondogo na kuchagua teknolojia na kusambaza kwa wakulima vichocheo 71

Hatua ya 10 Utunzaji wa kumbukumbu na usimamizi wa fedha- kazi inayoenda Sambamba kwa kipindi chote cha mradi mzima 76

Hatua ya 11 Kikundi kujifunza kutoka kikundi kingine na mafunzo ya uongozi 82

Hatua ya 12 Siku ya wakulima na mahafali 86

Hatua ya 13 Baada ya mahafali: kueneza teknolojia zaidi na kuunda shirika la Muungano wa vikundi 89

**Sehemu ya 3: Ufuatiliaji na udhibiti wa ubora 91**

SURA YA 6: Ufuatiliaji na Udhibiti wa Ubora 93

**Viambatanisho 111**

KIAMBATANISHO CHA 1: Taratibu za uchaguzi 113

KIAMBATANISHO CHA 2: Mwongozo wajinsi ya kuandaa katiba ya kikundi 115

KIAMBATANISHO CHA 3: Mwongozo wa kitaalamu na rasilimali 121

KIAMBATANISHO CHA 4: VIELELEZO 124

4A: MKATABA WA KUKODISHA SHAMBA LA K!KUNDI 124

4B: FOMU VA MKATABA UNAOHUSU MNVORORO WA MGAWANVO WA WANVAMA 126

4C: FOMU VA MKATABA WA PEMBEJEO/ZANA 128

40: KIELELEZO CHA MKATABA WA MAKUBAL!ANO 130

4E: FOMU YA ZIADA VA UFUATILIAJI WA DATA/TAKWIMU KWENYE VIKUNDI 133

KIAMBATAN!SHO CHA 5: VIFUP!SHO KIAMBATAN!SHO 135

CHA 6: FAHARASA VA MANENO 136

KIAMBATAN!SHO CHA 7: K!lIMO CHA MIGOMBA KWENVE MIRAD! VA RIPAT 140

KIAMBATAN!SHO CHA 8: REJEA NA KUSOMA ZAIDI 142

**Michoro - Vielelezo**


| | | |
|---|---|---|
| 0.1 | Ramani ya miradi ya RIPAT 1 -4 | xiv |
| 0.2 | Muda wa RIPAT 1 – 4, utekelezaji na ukusanyaji taarifa | xv |
| 2.1 | Uhalisia wa muundo wa taasisi | 11 |
| 3.1 | Mti wa matatizo | 23 |
| 5.1 | Mfano wa shamba la majaribio lililopimwa - kulinganisha njia mbali mbali za maandalizi ya shamba kwa mfumo unaoeleweka | 68 |
| 5.2 | Kulinganisha teknolojia bora na kilimo cha kawaida ya wakulima. | 68 |


**Majedwali**


| | | |
|---|---|---|
| 3.1 | Hatua za kufuatwa katika kuanzisha mradi. | 16 |
| 4.1 | Hatua zinazohusika wakati wa kuanzisha mradi | 26 |
| 5.1 | Sifa na majukumu ya viongozi wa kikundi | 49 |
| 5.2 | Kuielewa katiba ya kikundi | 50 |
| 5.3 | Kuandaa katiba ya kikundi | 51 |
| 5.4 | Ulinganisho kati ya mahindi na migomba kwenye eneo la eka moja kwa kuangalia gharama na mapato (TZS) | 78 |
| 5.5 | Gharama za uzalishaji mahindi kwa eka moja | 79 |
| 6.1 | Mfano wa wakati wa kukusanya taarifa za uigaji wa teknolojia | 96 |
| 6.2 | Fomu ya ufuatiliaji wa taarifa za Migomba [M] | 97 |
| 6.3 | Fomu ya ufuatiliaji wa taarifa za mbuzi [M1] | 97 |


**Masanduku**


| | | |
|---|---|---|
| 2.1 | Maeneo maalum yawahusishayo maafisa ugani katika miradi ya RIPAT | 14 |
| 3.1 | Vifaa vya Uchambuzi Shirikishi (PRA) | 20 |
| 3.2 | Kapu la uchaguzi | 22 |
| 4.1 | Orodha ya mada zitakazofundishwa wakati wa mikutano ya Halmashauri ya Wilaya na Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK). | 27 |
| 4.2 | Pembejeo | 30 |
| 4.3 | Orodha kwa ajili ya mkutano wa kijiji | 31 |
| 5.1 | Ushauri wa jinsi ya kufundisha watu wazima | 39 |
| 5.2 | Simulizi zilizochaguliwa | 63 |
| 5.3 | Vitu halisi vya kulinganisha katika agronomia ya kilimo | 69 |
| 5.4 | Mazao | 72 |
| 5.5 | Mifugo | 73 |
| 5.6 | Mfano wa kamati ndogo ndogo na majukumu yake | 74 |
| 5.7 | Mwongozo wa taarifa ya kikundi kwa ajili ya mkutano wa robo | 84 |
| 5.8 | Mifano ya kuwapa zawadi wakulima bora na vigezo vyake | 88 |
| 6.1 | Nguvu na umuhimu wa kupima matokeo | 93 |

## Dibaji: Historia ya RIPAT - mpaka sasa

Hadi 2004, Mfuko wa Hisani wa Rockwool (RF) ulitumia rasilimali zake kufadhili utafiti wa mada za jamii. Mara nyingi utafiti huu ulihusisha watafiti wa kutoka kitengo cha utafiti cha RF na watafiti kutoka vyuo vikuu na taasisi za utafiti ndani na nje ya Denmark.

Matokeo ya tafiti hizi za kijamii zimechapishwa kwenye vitabu na majarida. Matokeo haya hutumiwa na wanahabari na wanasiasa ili kuelewa masuala husika; kama wakiona ni mambo mazuri, wanasiasa wanaweza kutumia kwenye sera na kanuni za utawala.

Mwaka 2004, Bodi ya RF ilianza mjadala juu ya uwezekano wa taasisi ifanye miradi kabisa ili kujua kama matatizo mahsusi yanayokabili jamii katika nchi za Denmark, Ulaya au katika bara lingine lolote yanaweza kuondolewa au kupunguzwa kwa kutumia mfumo fulani mpya ambao umeelezewa kwa kina. Hii sio njia nyepesi kwa taasisi kufanya kazi. Kwanza ni muhimu kuwa na nadharia tete kuhusu njia nzuri ya kukabiliana na tatizo husika. Baada ya hapo, ilihitajika kupata mjasiriamali jamii ambaye anaweza kufanya kazi ya usimamizi na awe na ujuzi wa kusimamia utekelezaji wa miradi. Hatimaye ni muhimu kusimamia mradi na kutathmini kama kuna faida iliyotarajiwa.

Mfuko wa Hisani wa Rockwool sasa unafadhili miradi katika maeneo manne tofauti. Aina ya kwanza ya miradi ni kuhusu jitihada za kupunguza umaskini kwa watu vijijini katika nchi zinazoendelea.

Awali, taasisi ilifadhili utafiti uliofanywa na Profesa Martin Paldam (1997) wa Chuo Kikuu cha Aarhus ambao ulichambua matokeo ya misaada ya maendeleo inayotolewa. Inasikitisha kuwa utafiti huu ulibaini ya kwamba kwa miongo iliyopita, misaada mingi ilishindwa kuleta matokeo yaliyotarajiwa. Miradi mikubwa ya kilimo Afrika haikuridhisha katika suala la kuleta matokeo yaliyotarajiwa. Sababu nyingi ziliainishwa na Profesa Paldam na wachumi wengine. Mojawapo ya maelezo yaliyotolewa ni kwamba misaada ya kigeni imevuruga vichocheo vya uchumi wa ndani ya nchi.

Kutokana na matokeo haya ya utafiti, sisi katika Mfuko wa Hisani wa Rockwool tulikuwa na sababu nzuri ya kuamini ya kwamba eneo hili lingekuwa na changamoto nyingi kwetu. Hata hivyo, tulichukulia suala la sekta ya kilimo katika nchi zinazoendelea kukosa tija kuwa la muhimu sana kuliboresha na tulitaka kufanya juhudi kulishughulikia.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa Paldam na wachumi wengine, tuliamua kuanza na dhamiri ya kutokudhoofisha uchumi wa eneo tunakofanya kazi. Nadharia tete yetu ilikuwa ni 'utegemezi kwa mfadhili' huvuruga jitihada za maendeleo kwa sababu: Ikihisiwa kuna mtu fulani amepokea fedha au zawadi ya aina yoyote kutoka kwa wafadhili au serikali, watu wengine nao wataelekeza nguvu zao katikakupokea zawadi na kuacha au kupunguza uzalishaji kwa ajili ya mahitaji yao. Kwa hiyo tulitafuta washirika ambao tungeweza kuwashirikisha kile tulichokiamini.

Wakati wa chakula cha jioni pale A.P. Møller – Mærsk A/S huko Esplanaden, Copenhagen, mwezi Januari 2005, nilikutana na Bi. Eva Plessing, mjane wa miaka 99 aliyeachwa na hayati Rais wa Tanganyika Planting Company (TPC Ltd, iliyokuwa ikimilikiwa na A.P. Møller). Akagusia maoni ya Profesa Paldam ya matokeo mabaya ya misaada, lakini akasema alikuwa na mawasiliano na shirika ndogo lisilo la kiserikali la Kidenmark linaloitwa PULS (Projekt Ulandshjælp til Selvhjælp). Aliamini shirika hili lilikuwa na uwezo wa kuleta mabadiliko kwa sababu msaada wao ulikuwa unatolewa kwa kufuata kanuni ya kusaidia ili kujimudu na kuwasaidia wengine.

Hii ndiyo ilikuwa sababu iliyonisukuma mimi na mke wangu kutembelea PULS. Tulikutana na mwenyekiti wa PULS, Elly Vesterager na baadhi ya wenzake kwenye Bodi ya PULS huko Videbæk, Jutland, Denmark. Katika miezi ya joto ya 2005, mimi na mke wangu tulienda Arusha, Tanzania, ambako tulikutana na timu ya uongozi wa shirika dada la PULS, liitwalo Help to Self Help (HSH) na RECODA ambalo ni shirika mwenzao. Dominick Ringo alikuwa bado ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa RECODA. Ana shahada ya kwanza ya kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine, Tanzania, na shahada ya uzamili kutoka Chuo cha ITC cha Uholanzi. Mradi wa kilimo ulikuwa umebuniwa na PULS/HSH na RECODA, na ulikuwa umeanza mwaka 2003. Tukiwa hapo Arusha, tulitembelea miradi miwili iliyokuwa imefadhiliwa na PULS. Ilikuwa Manyire ukanda wa chini mashariki mwa mlima Meru, na kijiji cha Likamba kilichoko upande wa magharibi mwa mlima huo.

Matokeo yalijieleza yenyewe. Wakati mashamba mengine maeneo yale yaliyopandwa mahindi yalikuwa na mazao hafifu, mashamba yaliyokuwa kwenye mradi tuliyotembelea kwa muda mfupi yalikuwa yakizalisha mazao kama ndizi, ambayo tofauti na mahindi, ndizi hulisha kaya mwaka mzima na pia ni zao la biashara lenye thamani kubwa.

Hii ilikaribiana sana na kile ambacho Bodi ya Mfuko wa Hisani wa Rockwool ilikuwa ikitafuta. PULS na RECODA waliwekeza katika kutoa mafunzo bila kugawa misaada. Wakulima walilipia miche ya migomba waliyopewa na mradi kwa kuwapa wakulima wengine watatu idadi ya miche waliyopewa, hivyo kuanzisha usambasaji. PULS na RECODA walitaka kuingia gharama ndogo tu kwa kila kaya iliyowezeshwa. Jitihada zilifanyika kuwatia moyo wakulima ili waweze kuona miradi ni yao, hivyo kuufanya mradi uendelee hata baada ya miaka mitatu ya mfadhili na uwezeshaji kutoka RECODA kukoma.

Miezi iliyofuata majadiliano na RECODA yalianza kuhusu uanzishwaji wa mradi mkubwa zaidi uliopewa jina la RIPAT 1. Huu ulihusisha teknolojia nyingi zaidi kuliko ile miradi ya PULS, lakini mfumo uliotumika unafanana kwa kiasi kikubwa na ule wa miradi mitatu iliyofadhiliwa na PULS. RIPAT 1 ilikuwa na vikundi 16, kila kikundi kikiwa na wakulima 30 – 35; ulitekelezwa katika vijiji nane. Mradi ulitekelezwa kati ya mwaka 2006 – 2009.

Jina “RIPAT” lilipendekezwa na RECODA kwa mara ya kwanza na likaonekana kwenye andiko la kwanza la mradi mwaka 2005 likisimamia maneno *Rockwool Initiative for Poverty Alleviation in Tanzania*. Baadaye tuligundua uwezo mkubwa wa mradi huu na kwa hivyo tukaamua kubadilisha kuwa *Rural Initiatives for Participatory Agricultural Transformation*.

Katika miaka miwili ya kwanza ya RIPAT 1, PULS ilikuwa ikifanya mawasiliano ya siku hadi siku na RECODA. Mikutano kupitia simu ilikuwa inafanyika kila robo mwaka kati ya PULS, RECODA na RF na maamuzi muhimu juu ya shughuli, mikakati na marekebisho ya mradi vilifanyika kupitia majadiliano marefu na ya kina kati ya wadau hawa watatu. Ndipo mtoto wa kiume wa Elly Vesterager, Jens M. Vesterager (Shahada ya Uzamili, Kilimo) aliteuliwa kuwa Meneja wa Programu ya Uhakika wa Chakula na Mfuko wa Hisani wa Rockwool mwaka 2008, na ikaamuliwa kwamba PULS sasa wasiingilie mawasiliano kati ya RECODA na RF.

Kuteuliwa kwa Elin Schmidt kuwa Rais wa Mfuko wa Hisani wa Rockwool baada ya msimu wa baridi mwaka 2007 kulikuwa na tukio muhimu la kihistoria kwa RIPAT. Bi. Elin amewekeza nguvu zake nyingi RIPAT na miradi mingine ya Mfuko wa Hisani wa Rockwool, akiwa mwenyekiti wa mikutano ya simu ya robo mwaka na kutembelea maeneo ya miradi pamoja na watu wanaotekeleza miradi siku hadi siku.




Afrika, kuonesha Tanzania | Tanzania kuonesha Mikoa | Maeneo ya miradi ya RIPAT(wilaya)

Mchoro 0.1: Ramani ya miradi ya RIPAT 1-4

Miradi ya RIPAT 2 na 3 iliidhinishwa na Bodi ya Mfuko wa Hisani wa Rockwool mwaka 2008. Mradi wa RIPAT 2 ulitekelezwa upande wa nyuma wenye kivuli cha ukame wa mlima Meru, wilaya ya Arumeru. Hili ni eneo kame kiasi, limekaliwa na Wamasai na tuliogopa kwamba ukame wa eneo hili ungefanya uzalishaji kuwa mgumu kufikiwa. Kwa sababu hii, mradi wa RIPAT 3 ulikuwa Wilaya ya Karatu, eneo ambalo lina hali ya hewa nzuri zaidi kwa ajili ya kilimo na yote iliidhinishwa kwa wakati mmoja. Kwa sababu ukame ulikuwa mkali mwaka wa kwanza, miradi ilitekelezwa kwa miaka minne.

Mwaka 2009, tuligundua kwamba RIPAT ilikuwa ikileta matokeo mazuri ambayo yalihitaji kutafitiwa na kuchapishwa. Kwa hivyo, wachumi kutoka Kitengo cha Utafiti cha RF, watafiti kutoka Idara ya Anthropolojia na Uchumi ya Chuo Kikuu cha Copenhagen, na mabingwa wa Huduma za Taifa za Ushauri, Uganda, Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa na Chuo cha Denmark cha Mafunzo ya Kimataifa, waliombwa watathmini mradi wa RIPAT 1. Tathmini ililenga kuwa na takwimu za idadi na stahilifu za matokeo ya mradi wa RIPAT 1 lakini pia takwimu stahilifu zilikusanywa kutoka miradi hiyo mingine mitatu. Inaweza kuulizwa ni kwa nini tathmini haikufanyika kwa RIPAT 2, 3 na 4, na jibu ni kwamba ni zoezi ghali.

Miradi iliyofanyika baada ya RIPAT 1 iliboreshwa kutokana na uzoefu uliopatikana na matakwa ya wakulima. Baadhi ya vitu viliondolewa vilivyoonekana havina tija, na vingine havikutakiwa na vitu vizuri zaidi viliongezewa.

RIPAT 4 ulianza mwaka 2011 katika Wilaya ya Korogwe, eneo ambalo lina mvua za uhakika. Katika mradi huu, mafunzo kuhusu mikopo kwa vikundi vya kuweka na kukopa yalifanyika kwa kufuata kitini cha UKKV/VSLA kama kipengele mojawapo katika utekelezaji wa mradi. Mafunzo kama hayo hayajawahi kutolewa katika miradi mitatu ya awali.




Mchoro 0.2: Muda wa RIPAT 1 – 4, utekelezaji na ukusanyaji taarifa

Kadhalika, usambazaji wa teknolojia kwa wakulima walioko nje ya vikundi 20 vya RIPAT kwa kutumia maafisa ugani na wakulima wenye vipaji (wakulima vichocheo) baada ya makundi yote kupitia mafunzo juu ya taratibu za RIPAT kutoka “akademia” ya RECODA, ulikuwa sehemu ya mradi tangu katikati ya mwaka wa pili, tofauti na ueneaji wa miradi ya RIPAT 1, 2 na 3 ambayo ilianza katika vipindi vya mwisho vya miradi hiyo.

Miaka sita sasa imepita tangu kuanza kwa RIPAT. Taasisi zote mbili zilizohusika zinaamini kwamba muda umefika wa kushirikisha uzoefu wetu na kuufahamisha ulimwengu yale tuliyoyafanya na matokeo ya awali ya wataalamu.

Sawia na kuchapishwa kwa mwongozo huu, tumechapisha kitabu kiitwacho *Chaguo la wakulima - Tathmini ya mfumo wa kuchukuliwa kwa teknolojia za kilimo Tanzania* ambacho kinawasilisha tathmini ya RIPAT iliyotajwa hapo juu.

Lengo la mwongozo huu una sura mbili. Lengo la kwanza ni kutia moyo mamlaka na AZAKI kuufuata hatua-kwa-hatua ikijumuisha taratibu zilizotajwa kuhusu kudhibiti ubora. Lengo lingine ni kuhamasisha mamlaka na AZAKI zinafuata misingi ya kanuni zilizopo kwenye mwongozo huu katika miradi ya kilimo wanayotekeleza vijijini.

Ni matumaini ya Bodi ya RF na utawala wake kwamba tumekuja na mwongozo huu wa namna ya kuendesha miradi ya RIPAT na faida zake. Mamlaka za nchi zinazoendelea pamoja na wafadhili na mashirika ya misaada watapenda kufanya miradi yao kufuata mfumo wa RIPAT kutokana na ushahidi uliowakilishwa hapa. Watu wengi wakitumia mfumo huu, inawezekana siku za usoni ukaboreshwa na kuboresha uwiano wa faida-na-gharama. Chapisho hili la kwanza la Mwongozo wa RIPAT linawezekana likafuatwa na machapisho mengine yatakayoongeza matokeo zaidi kutokana na utekelezaji wa mfumo huu.

Imeamuliwa kwamba marejeo ya mwongozo yachukue mazingira ya Kitanzania lakini lengo letu ni kuelezea mbinu ambazo zinaweza kutumika katika nchi zote zinazoendelea kuziba pengo la teknolojia kwa wakulima wadogo. Tunaamini itakuwa rahisi kwa watumiaji wa mwongozo kuamua namna ya kutekeleza mwongozo pale ambapo mifano bayana imetolewa badala ya kanuni ya jumla hata pale ambapo mifano hiyo inahusu nchi tofauti.

Mwisho tungependa kusema kwamba wazo la RIPAT lilizaliwa kwa kusukumwa na taratibu na miongozo mingine ya mabadiliko vijijini. Tunapenda kutaja hasa kazi ya Bw. Hugh Allen kwa vikundi vya kuweka na kukopa na mwongozo alioutoa juu ya wazo hili. Kufundisha UKKV/VSLA kulikuwa ni mojawapo ya vitu vilivyofanywa kwenye miradi yote

minne ya RIPAT. Mfuko wa Hisani wa Rockwool pia walifadhili mradi wa UKKV/VSLA wa miaka mitatu wilayani Karonga, Malawi, ambako kaya 3,000 zimefundishwa juu ya UKKV/VSLA. Kitengo cha Utafiti cha RF na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Oxford na Chuo Kikuu cha Southern Denmark sasa wanatafiti matokeo ya mradi huu.

Tukiwa na uzoefu wa UKKV/VSLA na mfumo wa RIPAT, tungependa kueleza kwamba mfumo wa RIPAT una mambo mengi makubwa kuliko ule wa UKKV/VSLA. Kwa hiyo tunahimiza mashirika yanayotaka kutekeleza miradi ya RIPAT wasiache kusoma juu ya Ufuatiliaji na Udhibiti Ubora. Kwa kuijumuisha sura hii, wataweza kufahamu kama utekelezaji wao unaenda sawasawa, au kama msaada wa nje una manufaa.

Ni matumaini ya Mfuko wa Hisani wa Rockwool kwamba kwa kuchapishwa mwongozo huu na taarifa ya tathmini ya *Chaguo la wakulima: Kutathmini mbinu za kuwezesha uchukuaji wa teknolojia miongoni mwa wakulima Tanzania* tutakuwa tumechangia katika maendeleo ya kilimo kwa wakulima wadogowadogo wa nchi zinazoendelea.

*Tom Kähler*
*Mwenyekiti, Mfuko wa Hisani wa Rockwool, Desemba 2012*

# Namna ya kutumia mwongozo huu

## Kundi lengwa

Mwongozo huu umetayarishwa kwa ajili ya matumizi ya mashirika ya maendeleo ambayo yanataka kutekeleza miradi kama ya RIPAT (Rural Initiatives for Participatory Agricultural Transformation - Jitihada Shirikishi za Kuleta Mageuzi ya Kilimo Vijijini) - au miradi inayofanana na RIPAT na hasa kwa ajili ya matumizi ya wawezeshaji. Wawezeshaji ndio watu ambao wanafanya kazi moja kwa moja na wakulima wanaoshiriki. Kazi yao ni kufundisha na kutoa mafunzo juu ya teknolojia mpya na kuwezesha mafunzo shirikishi kwenye vikundi vilivyoanzishwa na mradi. Maafisa ugani wa serikali za mitaa wanaofanya kazi na wakulima nao pia wafundishwe jinsi watakavyoweza kutekeleza mfumo wa RIPAT.

## Ushirikiano na serikali za mitaa

Mradi wa RIPAT unashirikisha serikali za mitaa wakiwemo viongozi wa vijiji na maafisa ugani kwa lengo la kukubalika miongoni mwa wananchi wa eneo husika, na kuhamasisha maendeleo ya mradi na kueneza ujumbe wa mradi kwa jamii hata baada ya mradi kufikia tamati. Mwongozo huu una kifungu muhimu ambacho kimeweka mkazo maelekezo kwa SLM katika maeneo haya. Mpaka sasa RIPAT imetekelezwa kaskazini mwa Tanzania na kwa hivyo mwongozo umetumia mifano ambayo ni mahsusi kwa ajili ya Tanzania kwa maana ya mifumo ya utawala wa serikali na mifumo ya mitaa kwa ujumla. Lakini mwongozo huu unalengwa kutekelezwa katika nchi nyingine ambazo mifumo ni tofauti na tunaamini sio vigumu sana kuiga kama inavyohitajika.

## Maelekezo juu ya mfumo – sio kuhusu teknolojia mahsusi za kilimo

Mradi wa RIPAT hutafuta kuziba pengo la teknolojia za kilimo kwenye maeneo yaliyolengwa kwa utafiti shirikishi katika kubainisha ‘kapu’ la teknolojia (uchaguzi) bora kwa vikundi vya wakulima. Hata hivyo, mwongozo huu sio mwongozo wa hatua-kwa-hatua juu ya teknolojia fulani bali ni mwongozo juu ya mfumo wa RIPAT, yaani hatua za kuchukua wakati wa kuanzisha mradi wa kilimo uliojikita katika dhana ya kuwezesha vikundi ili vijimudu – jinsi ya kuanzisha na kuratibu vikundi, na hivyo kujenga uwezo wa vikundi kutoka kwenye umaskini kwa kuongeza uzalishaji katika kilimo.

Mwanzo wa mradi sio kule kutambulisha teknolojia, bali ni kuhamasisha waishio vijijini na wengine juu ya uwezekano wa wao kusimamia maendeleo yao na kuondokana na umaskini na kuwa na uhakika wa chakula kwa jitihada zao wenyewe; na kukusanya jamii na watu binafsi ili kufikia lengo hili. Teknolojia mpya zinatambulishwa kama sehemu ya mradi wa kusaidia kufikia lengo lakini hii ni baada ya wao kuamua ya kwamba wanataka na wanakusudia kufanya hivyo.

## Nyongeza kwa mwongozo huu na miongozo ya kiufundi

Teknolojia mahususi za kilimo zinazojumuishwa kwenye mradi wa RIPAT hutegemea mazingira na mifumo ya kilimo ya eneo husika. Mradi huu ambao umetekelezwa mpaka leo umejumuisha teknolojia kadhaa bora za uzalishaji mazao na mifugo, na huduma ya kuweka na kukopa vijijini. Kwa hiyo, mwongozo huu hauwezi kusimama peke yake. Shirika linalotekeleza mradi (SLM) liunganishe mwongozo huu na miongozo mingine ya kiufundi juu ya uzalishaji bora kutoka vyanzo vingine. Miongozo mingi ya kiufundi inayohusu kilimo bora inapatikana na mingine inaweza kupatikana kwenye mtandao bila malipo. Kiambatanisho na. 3 kinatoa orodha ya vitini ambavyo vinaweza kukusaidia.

## Muundo

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu tatu.

### Sehemu ya 1: Mwongozo unaolenga kimsingi shirika linalotekeleza mradi (SLM)

Sehemu hii inabaini uzuri wa mfumo wa RIPAT na kuelezea jinsi mradi unavyostahili kupangwa na majukumu ya washirika wakuu. Inaainisha pia hatua za kuchukuliwa wakati wa kuandaa mradi wa RIPAT, inahusisha kutafiti jamii husika na kutengeneza 'kapu la uchaguzi' kwa ajili ya wakulima walengwa. Mwisho inaelezea juu ya utaratibu wa kuhamasisha jamii kubadilika na kuwakusanya wakulima kuunda vikundi.

### Sehemu ya 2: Mwongozo unaoelekezwa kwa wawezeshaji vikundi

Sehemu hii inatoa mwongozo kwa wawezeshaji vikundi (WV) kwa ujumla juu ya namna ya kufanya kazi na vikundi vya wakulima. Inaainisha hatua za kupanga vikundi, kuhakikisha kwamba wana uongozi mzuri na kutengeneza katiba nzuri ya kikundi. Inaelezea jinsi ambavyo shughuli za kikundi zinaweza kupangwa na kufanikisha mchakato wa kujifunza katika kipindi cha mradi. Sehemu hii pia inaainisha jinsi ambavyo mafunzo yanaweza kushikizwa kama sehemu ya jamii kwa kuwafundisha wawezeshaji wa jamii ambao wanaitwa Wakulima Vichocheo, na pia jinsi ya kubadilishana taarifa kati ya vikundi na vikundi katika kueneza teknolojia.

### Sehemu ya 3: Mwongozo juu ya ufuatiliaji na udhibiti ubora

Sehemu hii imetoa nyenzo za ufuatiliaji wa vigezo muhimu na mwongozo juu ya kudhibiti ubora wakati wote wa mradi. Taarifa za ufuatiliaji zinatolewa na vikundi na kukusanywa na wafanyakazi wa SLM, wakati taarifa za udhibiti ubora zinakusanywa na mtu wa tatu ili kuhakikisha hakuna upendeleo.

## SEHEMU YA 1

# Mwongozo kwa shirika linalotekeleza mradi (SLM)

## SURA YA 1

# Utangulizi kuhusu RIPAT na vipengele vyake vikuu

RIPAT (Rural Initiatives for Participatory Agricultural Transformation) ni mfumo shirikishi wa kupeleka maendeleo vijijini ambao hulenga kuziba pengo la teknolojia za kilimo ili kuboresha maisha na kuleta kujitegemea kwa wakulima wadogo wadogo vijijini. Mradi wa kawaida wa RIPAT hulenga vijiji kati ya nane mpaka kumi. Vikundi viwili huundwa katika kila kijiji, kila kikundi kikiwa na wakulima kati ya 30-35 waliochaguliwa toka wenye uwezo wa tabaka la wastani wa chini katika jamii. Miradi mingi ya RIPAT mpaka sasa imefanyika katika vijiji nane na kuhusisha vikundi kumi na sita, na hii ndiyo idadi ya vikundi vitakayozungumziwa zaidi katika mwongozo huu. RIPAT hupeleka 'kapu la uchaguzi' la teknolojia za kilimo, yakiwemo mazao mbalimbali na mifugo kwa hivi vikundi katika namna ambayo huwezesha kujifunza kwa pamoja, kujaribisha na kushirikiana. Kila mkulima binafsi huchagua ni kipi achukue kwa ajili ya shamba lake. Mradi hutegemea sana ushirikiano wa karibu na viongozi wa vijiji na mamlaka za serikali za mitaa kwa kuhakikisha kuwa siyo tu uchukuaji wa haraka na teknolojia endelevu miongoni mwa wakulima wa vikundi vya RIPAT, bali pia uchukuaji wa teknolojia kwa wakulima wasio wanakikundi wa RIPAT katika jamii husika.

## RIPAT – Kuchanganya dhana ya toka 'juu kwenda chini' na 'chini kwenda juu' katika kupeleka teknolojia

Kwa muda mrefu imeonekana ni muhimu sana katika maendeleo ya kilimo kwa kuboresha utoaji taarifa, pembejeo na teknolojia mpya kwa wakulima. Mifumo miwili tofauti kidogo ilitawala hapo nyuma: Kufundisha na kutembelea Mashamba ya Darasa.

### *Dhana iliyozoeleka ya Kufundisha na Kutembelea ('juu kwenda chini')*

Mpango wa Kufundisha na Kutembelea ulikuwa mfumo wa wizara wa kupanga uenezaji. Kimsingi ulikuwa wa wima, njia moja ya mawasiliano katika kupeleka taarifa kwa wakulima. Mtiririko wa taarifa ulikuwa:

- Watafiti huvumbua teknolojia 'sahihi'.
    - Mawakala wa uenezaji hupeleka ujumbe (teknolojia).
        - Wakulima wa mfano waliochaguliwa kabla, huchukua ujumbe (teknolojia) na kufanyia kazi.
            - Jamii kwa upana wake huona na hunakili.

Kazi kubwa ya mawakala wa uenezi ilikuwa kuwafundisha wakulima wa mfano. Ilisadikika kwamba wakulima wa mfano hawa wangechukua mapendekezo ya jumla na ujumbe wa uenezi, na kwamba wakulima wengine kwenye jamii wangeiga toka kwao. Hata hivyo, matokeo ya njia ya Kufundisha na Kutembelea yamekuwa ya kuvunja moyo katika sehemu nyingi za Afrika (Anderson *na wenzake;* 2006 Gutam 2000).

Katika Afrika, udongo, tabia ya nchi na hali ya kiuchumi ya jamii inaweza ikatofautiana kwa kiasi kikubwa katika umbali mfupi tu. Hivyo, njia sahihi zaidi za kilimo na teknolojia hutofautiana kati ya kijiji na kijiji na hata kati ya shamba na shamba. Kwa hiyo, aina ya mapendekezo ya 'kipimo kimoja kinafaa kwa wote' yaliyoshabikiwa na mfumo wa Kufundisha na Kutembelea mara nyingi yalishindwa kuwanufaisha wakulima.

## Dhana ya Shamba Darasa (SD) ('chini kwenda juu')

Dhana ya shamba darasa imekuja ili kutatua mapungufu ya mfumo wa Kufundisha na Kutembelea, na imeshaenea katika nchi mbalimbali kote Afrika. Mfumo wa shamba darasa unasifika katika kutumia njia ya kipekee ya 'chini kwenda juu'. Ni njia shirikishi inayotumiwa na kikundi katika kujifunza, kuendeleza teknolojia, na kuzieneza kwa kutumia mbinu za elimu ya watu wazima.

Wakulima hufanya maamuzi yote kwenye shamba darasa, wakiongozwa na mwezeshaji. Mwezeshaji si mwalimu; yeye huchukua nafasi ya 'kiti cha nyuma', akielekeza namna ya kujifunza lakini bila kupendekeza ufumbuzi wa matatizo. Njia ya shamba darasa huwa haipigii debe upelekaji wa teknolojia ya aina fulani, bali teknolojia zitumikazo katika shamba darasa nyingi hutoka kwa wanakikundi wenyewe. Hii njia kwa kiasi kikubwa imejikita katika kupashana habari na kutoa majawabu mapya ya matatizo katika jamii husika kwa kutumia mafunzo yaliyofanyika.

Kwa kawaida, mtaalam wa shamba darasa huangalia zaidi mada moja (mfano, njia kamilifu ya kudhibiti wadudu, ufugaji, matunzo ya udongo na maji, au kilimo hifadhi). Mada ya kujifunza huchaguliwa na kikundi, na mtaala hufuata mzunguko asilia wa somo. Mara nyingi, shamba la kikundi huwezeshwa kwa msimu mmoja wa kilimo/mzunguko wa kilimo tu – wakati mwingine kwa miaka miwili. Kwa kusoma zaidi angalia Braun na Duveskog, 2008; Gallagher *na wenzake,* 2006.

### Mfumo wa RIPAT – ni muungano

Kanuni za dhana ya shamba darasa hutumika kwenye mradi wa RIPAT, ingawa katika namna iliyoboreshwa. Njia ya RIPAT kwa kiasi kikubwa ni muungano wa vipengele vya mfumo wa 'juu - chini' na 'chini - juu'. Zifuatazo ni miongoni mwa tofauti kati ya njia za RIPAT na Shamba Darasa:

- Kwenye RIPAT, mambo ya kujifunza kwa kiasi kikubwa hubainishwa kabla, si kwamba huamuliwa kipekee na vikundi binafsi. Mahali pa kuanzia kwa kila kikundi kati ya vikundi 16 kwenye mradi wowote wa RIPAT ni 'kapu la uchaguzi'. Kapu hili huundwa na teknolojia nyingi zilizoboreshwa ambazo zinapatikana kwenye vikundi. 'Kapu la uchaguzi' huundwa kwenye awamu ya maandalizi ya mradi kupitia tathmini shirikishi vijijini (PRA), na hivyo liko katika muungano wa mchango toka kwa wakulima (chini kwenda juu) na utalaam wa kiufundi (juu kwenda chini).
- Mfumo wa RIPAT hutoa mafunzo na kufundisha. Kapu la uchaguzi kwa kiasi kikubwa huwa limekusanya teknolojia mpya ambazo nyuma hazikujulikana kwa wakulima. Kuwawezesha wakulima kuelewa kwa ufasaha dhana na kanuni zinazoambatana na teknolojia hizo, ufundishaji (juu kwenda chini) huunganishwa na kazi za mikono kwa vitendo na kujifunza kwa makini kwa namna ya watu wazima (chini kwenda juu). Utaratibu huu huhakikisha kuwa teknolojia mpya zimeboreshwa kwa uzoefu wa

mahali husika na hivyo huundwa kulingana na mazingira husika. Mwezeshaji wa RIPAT huwaongoza wakulima katika kufanya majaribio shambani, lakini wakulima hufanya kazi za vitendo wao wenyewe. Kwamba, kwenye RIPAT, mwezeshaji hufanya zaidi kazi ya 'kiti cha nahodha' katika upelekaji wa teknolojia kuliko kwenye njia ya shamba la darasa – lakini hata hivyo, yeye kamwe si kiongozi wa kikundi.

- Kwa kawaida mradi wa RIPAT hufanyika kwa misimu mitatu au minne ya kilimo/mizunguko ya kilimo – yaani kwa muda mrefu kiasi kuliko shamba darasa. Kutokana na kiwango kikubwa cha teknolojia kwenye kapu la uchagua, msimu mmoja wa kilimo hautoshi kuhakikisha kwamba wakulima wamepata uwezo wa kutosha kuzifanya. Aidha, kwa maana mradi wa RIPAT hulenga kuanzisha vikundi imara na vya kudumu vyenye uongozi bora, muda zaidi huhitajika katika kuvifundisha vikundi juu ya uongozi, kufanyia kazi katiba ya kikundi, na utunzaji fedha za kikundi.

Tangu mwaka 2006, miradi minne ya RIPAT ilianzishwa kaskazini mwa Tanzania, ikilenga vijiji 34 na karibu familia 2,200. Hatua hizi za miradi ya RIPAT zimefanyiwa utafiti, na matokeo ya utafiti huo yamechapishwa kwenye kitabu kiitwacho *Chaguo la wakulima – Tathmini ya njia ya uchukuaji teknolojia za kilimo nchini Tanzania* (Lilleør na Lund-Sörensen, 2013). Kwenye kitabu, watunzi wengi wamechambua na kutathmini lengo la RIPAT katika kutambulisha teknolojia kwa wakulima wadogo, ambayo husimamia dhana kwamba 'kipimo kimoja hakifai kwa wote'. Kwa habari za kina zaidi kuhusu RIPAT, tafadhali rejea kwenye kitabu. Habari zaidi juu ya historia ya RIPAT ipo katika neno la utangulizi la mwongozo huu.

Mfumo wa RIPAT umejengwa katika misingi mikuu mitatu:

1. Uanzishaji wa maono mazuri ya baadaye kupitia *uhamasishaji* makini wa jamii, uwezekano wa mabadiliko na uandaaji wa wakulima kujiletea maendeleo yao;
2. Uanzishaji wa vikundi vya wakulima vyenye *uongozi bora* ili kuwezesha upelekaji wa teknolojia za kilimo kupitia majaribio shirikishi na mbinu makini katika kujifunza;
3. *Ushirikiano wa karibu* na mamlaka za serikali ndogo kwenye maeneo husika, viongozi wa vijiji, na maafisa wa maendeleo ya kilimo wa serikali kwa ajili ya kuhakikisha kuna uendelezwaji na uenezwaji wa mradi kwa jamii yote.

## RIPAT: wapi, kwa ajili ya nani na lini

Kimsingi, mfumo wa RIPAT unatakiwa kutumika kwenye jamii ambayo kazi zake ni za kilimo. Aidha, kupitia uzoefu imeshaonekana kwamba mfumo wa RIPAT hufanya kazi vizuri zaidi kwenye maeneo na kwa watu wenye sifa zifuatazo hapa chini.

Mfumo wa RIPAT hufanya kazi vizuri zaidi kwenye maeneo

- *Kule ambapo wakulima huishi karibu karibu* – kaya zilizotawanyika na umbali mrefu toka nyumbani kwenda kwenye shamba la kikundi inaweza kuleta ugumu kwa baadhi ya wakulima kuhudhuria mikutano ya kikundi kila juma. Inafaa umbali toka nyumbani kwenda shamba la kikundi usizidi kilometa 5.
- *Kukiwa na hali kidogo ya kuridhisha ya kilimo* – maeneo yenye hali ngumu, tabia nchi kavu na fursa mbaya za uvunaji maji ya mvua na/au umwagiliaji ni tishio.

- *Mahali ambapo watu wana makazi ya kudumu*– wakulima washiriki wawe wakazi wa kudumu na wana uzalishaji mazao na mifugo kama sehemu ya maisha yao.

## Mfumo wa RIPAT hufanya kazi vizuri kwa watu ambao

- *Wana ardhi* – watu wanatakiwa kuwa na uwezo wa kufanyia mazoezi kile walichojifunza kwenye shamba la kikundi katika mashamba yao binafsi. Watu wasio na ardhi hawatafaa vizuri kwenye mpango huu.
- *Wale wenye ari ya kufanya kazi* – upunguzaji wa makali ya umaskini huhitaji nia thabiti na endelevu ili kuleta mabadiliko.
- *Wenye fikra sahihi ya ushirikiano* – washiriki lazima wawe tayari kushirikiana katika kikundi, kujifunza toka kwa wenzao, na kushirikishana mawazo na taarifa.

Vigezo vya kina vya uchaguzi vimefafanuliwa katika Sura ya 4, Hatua ya 4. Hitaji la kwamba wanakikundi lazima wawe na ardhi kwa ajili ya matumizi laweza kufanya kaya maskini wote kijijini wasipate uwakilishi kwenye mradi. Kadhalika wakulima matajiri sana kijijini wasiwakilishwe sana kwani hawahamasiki kufanya kazi katika vikundi.

## *Ni wakati gani wa kuanzisha mradi wa RIPAT*

Kulenga majira sahihi ni kipengele muhimu sana katika miradi ya kilimo. Maeneo yenye tabia nchi ya pepo za msimu (misimu ya kiangazi na masika), ni vizuri kuanzisha mradi wa RIPAT miezi 2-3 kabla ya msimu wa mvua na kazi nyingi za kilimo kuanza. Hii huwapa wafanyakazi wa mradi muda mzuri wa kupanga vikundi, kufundisha masomo ya mwanzo na kuandaa eneo/ardhi kwa ajili ya kazi za kikundi. Pia hutia moyo na kukipa kikundi na jamii hamasa kama mwisho wa msimu wa masika kutakuwa na ushahidi wa kuonekana wa kazi za mradi kwa maana ya mavuno. Hivyo, mradi hautakiwi kufanya kazi kwa muda mrefu sana kabla ya kazi za mikono kuanza na matokeo tarajiwa kuonekana.

Katika miradi ya RIPAT hadi sasa, dhana ya kuweka na kukopa imetambulishwa kuelekea mwisho wa muda wa mradi. Lakini inaweza kuwa na manufaa kuhusisha dhana hii katika hatua za mwanzo za mradi – au hata kuanza nayo. Kupitia akiba zao, wanakikundi huweza kulimbikiza fedha kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo kwa namna walivyojifunza wakati wa mafunzo.

## Vipengele na sifa muhimu za mfumo wa RIPAT

### *1. Kikundi*

Ujuzi, teknolojia na pembejeo vyote hupelekwa kupitia kikundi. Kikundi ndicho jukwaa la kufikisha mafunzo na upashanaji habari. Kikundi huwa na watu 30 – 35 wote toka kaya tofauti ambao wana nia za kufanana. Kwenye kujifunza na kujaribu vitu vipya, mara nyingi ni vizuri kufanya kazi kwa pamoja na watu wengine ambao wako kwenye hali sawa na ya kwako. Hali hii huleta nguvu ya pamoja na kutiwa moyo. Vikundi hukutana kila juma wakati wa mwaka wa kwanza kwa ajili ya masomo ya nadharia na kujifunza kwa vitendo na huongozwa na viongozi waliochaguliwa kidemokrasia ambao kazi yao ni kupanga na kuongoza kazi za kikundi na kusimama kama waangalizi wa mali za kikundi. Maarifa ya uongozi huendelezwa; vikundi huelewa vizuri sifa za kiongozi, na maarifa



Kikundi cha RIPAT kikiwa kazini

haya pia hutumika kuwasaidia kuchagua viongozi kwa mitazamo mingine. Vikundi hufundishwa na kusaidiwa namna ya kufanya kazi, kutatua matatizo na kufanya maamuzi ya pamoja. Mafunzo juu ya ukuaji wa kikundi hukuza hali ya umoja na ushirikiano, na wanakikundi hujifunza kufanya kazi kwa pamoja na kwa maelewano. Imekusudiwa kuwa vikundi vinatakiwa kuamsha ari na nia ya maendeleo ndani na nje ya kijiji chao. Wanafundishwa namna ya kuwa na sauti na uwezo wa kujadiliana ndani ya jamii, na kufanya kazi ya utetezi kijijini mwao kwa niaba ya jamii yao.

*2. Shamba la kikundi*

Shamba la kikundi ni darasa na kituo cha kujifunzia. Wanakikundi hupata shamba la kikundi, na hujifunza kwa mazoezi ya vitendo ndani ya usimamizi wa mwezeshaji. Wakulima hugundua, hujadili, huchambua na hufanya maamuzi kutokana na kila teknolojia, na hulinganisha kilimo chao cha kawaida walichozoea na teknolojia zilizoboreshwa ambazo zinashauriwa zitumike.

Mtaala hufuata mzunguko wa asili hatua-kwa-hatua kwa kila teknolojia. Mtaala wa kila teknolojia huwa umekamilika pale wakulima wanapokuwa tayari wameshafanya vipindi vyote vya vitendo wakati wa mzunguko wa uzalishaji. Uwepo wa mazao ya kudumu na wanyama kwenye kapu la uchaguzi huhitaji kuwe na uwezeshaji wa muda wa zaidi ya mwaka mmoja. Jamii hualikwa kutembelea shamba la kikundi mara moja kwa mwaka.

3. *Umiliki wa washiriki na mamlaka*

Umiliki wa jumla wa mradi kwa jamii na wakulima wanaohusika unasisitizwa kupitia uhamasishaji makini wa jamii na uwezekano wa mabadiliko, pia kupitia uandaaji wa wakulima ili waweze kujiletea maendeleo yao wenyewe. Ari ya 'ndiyo tunaweza' hujengwa tangu mwanzo na kuendelea hadi mwisho wa mradi ili kuwatia moyo wanakikundi na kuwaandaa kwa ajili ya mabadiliko. Kukubali kwa wakulima wazo la kulipia pembejeo, matumizi ya mnyororo wa kugawana/kupeana mifugo, na jukumu lililowekwa kwa wakulima la kugawa upya vipando kwa wakulima wengine kijijini, yote hukuza mtazamo wa umiliki wa mradi, na dhana yakusaidiwa ili ujimudu, na vipengele vyote hivi pia huongeza uwezekano wa gharama za mradi kuwa sawa na zilizotarajiwa. Mafunzo kwa wakulima vichocheo (WV) na uhusishaji wa serikali ya kijiji na maafisa wa kilimo vijijini yote hukuza uenezaji wa mradi kwa wakulima wengine.

4. *Uchambuzi wa hali halisi*

Uchambuzi makini wa hali halisi ya eneo (PRA) ni utangulizi katika kutoa mwongozo sahihi wa kimaendeleo. Kwa kuwa RIPAT hulenga kwenye kilimo, ni muhimu sana kuwa na uelewa wa ndani juu ya shughuli za kilimo zinavyofanyika, misimu na kazi zake muhimu, na udongo wa eneo husika, maji, na hali za tabia nchi, ili kutambua majawabu sahihi. Taarifa hukusanywa kwa kutembelea vijiji na kuwa na majadiliano ya kikundi na wakulima na viongozi wa kijiji, maafisa kilimo, na watu maarufu wenye taarifa muhimu.

5. *Kapu la uchaguzi*

Kwa kuzingatia uchambuzi wa hali halisi na mchango toka kwa wakulima na wataalam, kapu sahihi la uchaguzi linaundwa ambalo huwa na teknolojia mbalimbali ambazo huaminika kuboresha uhakika wa chakula na kupunguza umaskini. Matumizi ya rasilimali zipatikanazo kwenye maeneo husika husisitizwa katika uchaguaji wa teknolojia. Wakulima huchagua wenyewe teknolojia zifaazo kutumika katika mashamba yao wenyewe. Vipengele mbali mbali kuhusu kila teknolojia huwasilishwa na kujadiliwa na wakulima, ikiwemo uchambuzi wa kiuchumi, ili kuwasaidia wakulima kubaini chaguo linalowezekana kufanyika toka katika mapendekezo yaliyowasilishwa.

6. *Ufundishaji, mafunzo na uwezeshaji*

RIPAT huhamisha maarifa toka kwa wawezeshaji hodari kwenda kwa wakulima. Maarifa mapya ya kitaalam huongezwa kwa maarifa yaliyoko kwa wakulima. Ili kuziba pengo la kiteknolojia, mwezeshaji wa kikundi (MK) hufundisha na kuwapa ujuzi wakulima, na huwezesha kujifunza kwao na kuelewa mambo mbalimbali ya msingi. Mafunzo kwa kawaida huwa ni ya nadharia na vitendo. Kwanza, mwezeshaji hufundisha kikundi kanuni za kitaalam, na msingi wa sayansi uliopo, na hatua katika kutekeleza mbinu. Halafu huongoza wakulima kwa kufuata hatua za vitendo, na hivyo huwapa uelewa na ujuzi. Uzoefu wa wakulima hutumika pamoja na maelezo ya kanuni za kisayansi zilizotolewa juu ya kila namna ya kufanya, na upungufu wowote wa maarifa kwa upande wa wakulima hufanyiwa masahihisho wakati wa mafunzo. Matatizo na changamoto hushughulikiwa katika msimu wa kawaida wa kilimo kadiri zinapojitokeza; wakulima hujifunza jinsi ya kufanya maamuzi ya uongozi, na inapobidi, teknolojia hubadilishwa kuendana na hali za eneo.

7. *Shirika linalotekeleza mradi - SLM*
   SLM lina ufahamu wa kutosha kuhusu mpangilio wa mradi, na lina jukumu la kuhakikisha ushirikiano na usimamizi toka taasisi ndogo za serikali – hasa toka kwa maafisa ugani na shirika lolote lifanyalo kazi katika eneo hilo. SLM huhakikisha uwezeshaji utolewao ni bora na upatikanaji wa pembejeo kwa muda sahihi (mbegu, vifaa, wanyama, n.k).

8. *Ufuatiliaji huru na udhibiti wa ubora*
   Ni lazima mradi wa RIPAT uhusishe chombo huru ambayo itadhibiti ubora wakati wote, ili kuona kama viwango vilivyowekwa kwenye mpango vinafikiwa kwa kutenda. RECODA ambayo ni shirika lisilo la kiserikali (NGO) la Kitanzania lililopo Arusha, lipo kusaidia kama mwangalizi. Aidha, wanakikundi, meneja wa mradi, na SLM ni lazima wafanye ufuatiliaji na tathmini mafunzo, kuakisi kwa, na kushughulikia mapungufu yoyote kati ya malengo na mafanikio juu ya kazi zilizotekelezwa.

9. *Jina la RIPAT na nembo*
   Jina la RIPAT litumike pale tu miradi inayotekelezwa inaendana na mwongozo huu. Miradi yote ya RIPAT lazima ijumuishe ufuatiliaji na mchakato wa uhakiki wa ubora ulioainishwa katika sura ya 6 kuhakikisha kiwango cha juu cha utekelezaji. Shirika linalotekeleza na linazingatia ubora ulioainishwa linaweza kutuma jina na nembo ya RIPAT.

*Ninaposikia, Ninasahau*



*Ninapoona, Ninakumbuka*



*Ninapofanya kwa vitendo, Ninamiliki kwa ajili ya maisha yangu*



## SURA YA 2

# Mpangilio wa mradi wa RIPAT na majukumu ya watendaji wakuu

## Mpangilio wa mradi

Mradi halisi wa RIPAT hulenga vijiji nane. Vikundi viwili huanzishwa katika kila kijiji, kila kikundi kikiwa na wakulima 30-35. Hii hufanya kuwa na jumla ya vikundi 16 kwa mradi mzima vikihusisha karibu wakulima 500. SLM linaweza kutekeleza miradi kadhaa ya RIPAT kwa wakati mmoja, labda kwa tarehe tofauti za kuanzisha miradi. Kila mradi una meneja aliyewekwa, na wawezeshaji wa kikundi wawili au watatu. Meneja wa mradi (MM) na wawezeshaji wa kikundi hutoa mafunzo kwa vikundi. Mwanzoni kutakuwa na wawezeshaji watatu wa kikundi, lakini baadaye idadi inaweza ikapunguzwa na kuwa wawili. Wawezeshaji wa kikundi walioajiriwa na SLM ni lazima wawe na sifa za ziada za kiufundi na uwezo wa kufundisha kwa vitendo ili waweze kufanya kazi kama timu kuwezesha vipengele mbali mbali vya mradi. Na hivyo, kikundi kitatembelewa na wawezeshaji tofauti tofauti katika kipindi cha miaka mitatu ya mradi ili kuhakikisha kuwa vipengele vyote vinavyohusu maendeleo ya kikundi, kujengea uwezo, na teknolojia za kilimo kuwa zimefundishwa barabara. Mchoro 2.1 ni muundo halisi wa shirika ulivyo.




Kielelezo 2.1 Uhalisia wa muundo wa taasisi

## *Kazi na majukumu*

*Mkurugenzi Mtendaji*

Mbali na kuwa ndiye kiongozi wa SLM – na kuwa mtu anayehusika moja kwa moja na waajiriwa na kazi za mradi, Mkurugenzi Mtendaji lazima kwa nyakati zote awe na muda wa kuhuisha uhusiano wa shirika na mamlaka za serikali za mitaa kwenye wilaya ambamo miradi ya RIPAT ya shirika inatekelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji lazima atafute namna ya kushawishi sera zinazopitishwa na wakuu wa serikali kwa kueleza maendeleo ya RIPAT kwa watunga sera na watendaji. Kazi hii kwa sehemu kubwa ni kutangaza habari za RIPAT kwenye majukwaa muhimu kama ya wilaya na kamati ya ushauri ya mkoa na mabaraza ya wilaya, kupanga kutembelea mashamba, na kuwaalika wawakilishi wa mamlaka za mitaa kwenye matukio ya RIPAT na mikutano. Kazi hizi zitakuwa ni nyongeza ya kazi ya utetezi inayofanywa na viongozi wa programu, (KP), MM na MK.

*Kiongozi wa Programu (KP)*

Kiongozi wa programu ana jukumu la jumla katika miradi ya RIPAT. Kazi muhimu kwa kiongozi wa programu ni kuwaelimisha na kuwaelekeza mameneja na wawezeshaji wa kikundi ili kwamba waweze kutoa mafunzo yenye ubora kwa vikundi. Zaidi ya hayo, kiongozi wa programu ana kazi ya kufuatilia maendeleo ya miradi na kazi ya mameneja wa miradi, na ya wawezeshaji wa kikundi, kupandisha daraja uwezo wao kama inavyotakiwa, na kufuta kazi mtumishi yeyote ambaye hafanyi vizuri. Kiongozi wa programu moja kwa moja anahusika na ufuatiliaji wa manunuzi ya pembejeo za mradi (mbegu, vifaa, wanyama), kuwapanga wawezeshaji wa vikundi wenye maarifa sahihi kwenye kazi tofauti tofauti, na kupanga utembeleaji na vipindi vya mafunzo kwenye vikundi vyote vya mradi. Hufanya mafunzo na mikutano ya mara kwa mara na mameneja wa miradi, pia ana wajibu wa kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa sera za mradi, na kuhakikisha kuwa fedha za mradi zinapatikana katika muda muafaka.

*Mameneja wa miradi* ***(MM)***

Meneja wa mradi ana jukumu la jumla la siku hadi siku kusaidia mradi na kutoa mafunzo kwa vikundi 16 ndani ya vijiji 8 kwenye mradi. Hufanya kazi kama meneja wa kituo kama mradi unatekelezwa kutoka ofisi ya tawi. Meneja wa mradi husimamia kazi ya wawezeshaji wa vikundi ambao wamewekwa katika mradi. Husimamia kazi za mradi na watumishi, huendesha mikutano ya mara kwa mara na wawezeshaji wa vikundi ama kwa juma, huandaa taarifa za mradi kwa ajili ya kiongozi wa programu, hutoa bajeti ya mradi, kwa mfano, safari na mikutano, huhakikisha mrejesho wa kila siku kuhusu kazi za mradi umefanyika, huzungumza na kiongozi wa programu juu ya vijiji vinavyofaa kwa ajili ya uenezaji wa mfumo wa RIPAT, akifanya kazi kwa karibu na Halmashauri ya kijiji na maofisa ugani.

*Wawezeshaji wa kikundi* ***(MV)***

Wawezeshaji wa vikundi ni watu wakutanao moja kwa moja na wakulima washiriki. Kazi yao ni kutoa mafunzo ya vitendo juu ya teknolojia mpya za kilimo, na kuwezesha kujifunza kwa ushiriki kati ya wanachama wa vikundi vilivyoundwa kwa ajili ya mradi. Siyo rahisi kutoa maelezo mafupi juu ya mwezeshaji wa kikundi. Kuwa na utu na mtazamo sahihi

mara nyingi ni muhimu zaidi kuliko kuwa na historia nzuri ya elimu na ngazi ya uwezo aliyonayo mtu. Baadhi ya wawezeshaji wa vikundi wanaweza kuwa na shahada ya chuo kikuu; wengine wanaweza kuajiriwa toka mashirika ya maendeleo au kutoka katika huduma za ugani za serikali. Kwa kawaida, mwezeshaji wa kikundi anatakiwa kuwa na stashahada katika fani husika ya maendeleo kama vile ugani, sayansi ya jamii, kilimo au maendeleo vijijini. Mwezeshaji wa kikundi (MM) anatakiwa kuwa na uzoefu katika kufanya kazi na jamii vijijini na shauku ya kusukuma mbele maendeleo vijijini kwa kusaidia watu ili waweze kujimudu wenyewe. Wanatakiwa kuwa na umahiri na ustadi katika kufundisha.

- *Utaalam.* Kwa kuwa RIPAT huwapa wakulima kapu la uchaguzi; vikundi huhitaji uwezeshwaji katika kutumia fani mbalimbali za utaalam juu ya mifugo na kilimo. Mradi wa RIPAT pia huhusisha mafunzo ya uongozi wa kikundi, usimamizi wa fedha za kikundi na mfumo wa kuweka na kukopa wa kikundi. Mtu mmoja hawezi kuwa na utaalam juu ya mada zote hizi, hivyo safu ya wawezeshaji na meneja wa mradi kwa kawaida watatimiza hili wao kwa wao kwenye kuwezesha vikundi hivi 16 ndani ya mradi wa RIPAT. Kwa kawaida kila kikundi kitatembelewa na wawezeshaji mbalimbali na meneja wa mradi katika mradi wa muda wa miaka mitatu ili kuhakikisha kuwa masomo yote yamefundishwa kwa usahihi.

- *Ufundishaji.* Mwezeshaji wa kikundi (MM) siyo tu ni mtaalam hodari bali pia ana ujuzi mzuri wa ufundishaji. Hii itamsaidia kutengeneza mazingira mazuri ya kujifunzia na kubadilishana mawazo, na mahali ambapo kila mmoja hujisikia yeye ni wa muhimu na anathaminiwa. Mwezeshaji lazima apewe mafunzo juu ya elimu kwa watu wazima na mazingira yatakiwayo kwa kujifunzia. Ni muhimu pia mwezeshaji aelewe hatua mbalimbali za maendeleo ya kikundi na ndipo ataweza kuhakikisha kuwa vikundi vimekua na kuendelea vizuri. Mwezeshaji anatakiwa kugundua kikundi kinapokuwa hakijatulia katika kazi fulani na wakati kukiwa na uwezekano wa kutokea migogoro kwenye kikundi ili kuzuiwa kabla ya kutokea. Ni muhimu kwa mwezeshaji kuelewa utamaduni wa eneo ambamo mradi unatekelezwa, na kujua namna ya kufanya kazi na watu binafsi tofauti tofauti katika jamii.

## Kuhusisha mfumo wa serikali ya mtaa na maafisa ugani

Serikali ina wajibu wa kutengeneza mazingira ambayo ni mazuri kwa ajili ya maendeleo ya jamii na ambayo yanawezesha kazi za mradi. Mipango na sera zimeundwa ili kupambana na umaskini na hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula, miundo, na watumishi wafanye kazi na jamii za vijijini, zipo katika wilaya nyingi. Ni lazima iwekwe wazi kwa mamlaka za serikali husika kwamba RIPAT hufanya kazi ili kusaidia jitihada za serikali. Lengo ni uhakika wa mwendelezo wa maendeleo ya kiuchumi yafaayo kuwepo baada ya muda wa mradi.

Mradi wa RIPAT lazima ufanye kazi kwa karibu na afisa wa maendeleo ya kilimo na mifugo wa wilaya (AKMW). Katika ngazi ya kijiji, ushirikiano unaweza kutofautiana kati ya kijiji na kijiji, kutegemeana na upatikanaji wa maafisa ugani wa serikali. Katika baadhi ya maeneo kuna maafisa ugani wanaokaa katika kila kijiji, lakini mara nyingi huwa kuna afisa ugani mmoja ahudumiaye kata nzima (kawaida ikiwa na vijiji viwili hadi vinne). Mtazamo wa maafisa ugani kuhusu ushirikiano na RIPAT unaweza kutofautiana kati ya wale wenye shauku ya kushiriki wale wasio tayari.

Kimsingi, maafisa ugani wanatakiwa kufanya kazi na wanakijiji katika masuala yote yahusuyo maendeleo ya kilimo. Wanatakiwa kupeleka teknolojia mpya kwa wakulima. Aidha, mara nyingi maafisa ugani hawafundishwi vya kutosha kuhusu teknolojia mpya, au maarifa yao yanakuwa yamepitwa na wakati. Na kama ilivyotajwa kwenye utangulizi, RIPAT hukutanisha mifumo ya muungano wa 'juu kwenda chini' na 'chini kwenda juu' ili kuweka daraja litakaloziba pengo ya kiteknolojia - mfumo ambao maafisa ugani wanaweza kuwa hawaufahamu. Kwa kuwa mradi wa RIPAT hugusa takribani 10% tu ya kaya zote kijijini, ni muhimu kuwashirikisha maafisa ugani kwa kadri itakavyowezekana kwenye utekelezaji ili kwamba waweze kujifunza kuhusu teknolojia na waweze kuendeleza utekelezaji wa ile 90% ya kazi baada ya mradi kufika mwisho. Kwa sababu hii, maafisa ugani hukaribishwa kwa wingi kadri iwezekanavyo kushiriki kwenye mikutano ya kila juma ya kikundi. Lakini mradi huwa hauna madaraka ya kusimamia kazi za kila siku za maafisa ugani, maana wanawajibika kwa mamlaka za serikali.

Kwa kawaida, maafisa ugani wanahudhuria mikutano ya kikundi cha RIPAT, hujifunza, husikiliza na kuchangia michango yao pale inapohusiana nao. Maafisa ugani huwa hawaingilii maamuzi ya kikundi, maana wao si wanakikundi. Maafisa ugani hawawezi kuamrisha kikundi. Wakati wa utekelezaji wa mradi, kikundi hufundishwa na kushauriwa na mwezeshaji wa kikundi na maafisa ugani. Uhusishaji wowote wa moja kwa moja wa afisa ugani kwenye vikundi vya RIPAT siku zote utatakiwa kuratibiwa na kukubaliwa na mwezeshaji na/au meneja wa mradi. Ili kuepusha kutoelewana, ushirikiano na serikali ya kijiji lazima upangwe vizuri tangu mwanzo, na mfumo wa maamuzi na mtiririko wa mawasiliano uwe wazi. Pia inatarajiwa kwamba maafisa ugani watashirikiana na wakulima vichocheo (WV) katika kuongoza zoezi la uenezaji wa teknolojia za RIPAT kwenda vijiji vingine. Maeneo maalum ambamo maafisa ugani huhusishwa kwenye mradi wa RIPAT yameorodheshwa kwenye sanduku 2.1.

Sanduku 2.1 Maeneo maalum yawahusishayo maafisa ugani katika miradi ya RIPAT

- *Uchambuzi wa hali halisi*. Afisa wa maendeleo ya kilimo na mifugo wa wilaya (AKMW) anahusishwa kwenye kuchagua vijiji kwa ajili ya miradi ya RIPAT, na hushiriki kwenye uchambuzi wa hali halisi kama mtoa habari muhimu na mtoa habari zilizofanyiwa utafiti.
- *Uzinduzi rasmi wa mradi*. Maafisa ugani hushirikishwa kwenye uhamasishaji na uandaaji wa jamii na ushiriki kwenye uundaji wa vikundi.
- *Kazi za ufuatiliaji*. Maafisa ugani hushiriki kwenye mikutano ya vikundi na vipindi vya mafunzo kwa kiasi kikubwa kadri iwezekanavyo ili kujifunza. Wakati mwingine huombwa na meneja wa mradi kufuatilia vipengele muhimu vya mradi kama vile maendeleo ya mnyororo wa ugawanyaji mifugo, mafunzo ya mkulima kwa mkulima, na uenezaji wa teknolojia vijijini (kwenye mradi wa RIPAT, wakulima wote hukubali kufundisha wakulima wengine watatu katika vile walivyojifunza kwenye mradi).
- *Huduma za ushauri*. Kama sehemu ya kazi zao, maafisa ugani hutoa ushauri wa huduma za kilimo kijijini; kazi hii hukamilisha na kukuza utumiaji wa mbinu za kilimo zilizoboreshwa kupitia mradi wa RIPAT.
- *Uenezaji wa mradi baada ya muda wa mradi kuisha*. Kwa sababu wameshajifunza na kupata uzoefu kutoka miradi ya RIPAT, inatarajiwa kwamba maafisa ugani wataongoza uenezaji wa utekelezaji kwa wakulima ambao hawakuguswa na mradi wa RIPAT na kwa vijiji vingine. Kazi hii inaweza kufanywa kwa ushirikiano na wakulima vichocheo wa RIPAT.

**SURA YA 3**

# Shughuli za awali kabla ya mradi

Kabla ya kuanza mradi kuna kazi mbali mbali za kupanga mipango ya kazi zinazotakiwa kufanyika. Upo usemi usemao kuwa “anayeshindwa kupanga amepanga kushindwa.” Mradi ni lazima upangiliwe vizuri ili kuhakikisha kuwa unachukuliwa na jamii na viongozi wa serikali za mitaa. Kwa hiyo, SLM lazima lifuate hatua zote zilizoainishwa katika sura hii (tazama Jedwali 3.1 kupata maelezo). Kimsingi, wawezeshaji wa vikundi lazima wahusike katika kufanya mchakato mzima wa maandalizi ya mradi lakini wakati mwingine wanaajiriwa na kufundishwa baada ya fedha za mradi kutolewa.

## Hatua ya 1: Uchaguzi wa maeneo yanayofaa kwa mradi

Hatua ya kwanza katika kupanga kufanya mradi wa RIPAT ni kuainisha maeneo yanayofaa kufanyia mradi. Ingawa mfumo wa RIPAT unafaa katika jamii nyingi zinazojishughulisha na kilimo, hali na mazingira fulani yanafanikiwa zaidi kuliko mengine kama ilivyoainishwa kifupi katika sura ya kwanza.

Eneo lililokusudiwa kwa mradi wa RIPAT linapendekezwa kuwa na vijiji 10-20 vinavyokaribiana kwa umbali. Vijiji kama vinane vitahusishwa moja kwa moja katika mradi wa miaka mitatu. Hata hivyo, vijiji vinavyozunguka vitahusishwa katika uenezi wa mradi baada ya kutekelezwa katika vile vilivyotangulia. Uenezi wa mradi unategemea zaidi kazi za wakulima vichocheo –wakulima waliofanya vizuri katika vikundi – na za maafisa ugani wa serikali. Wazo la uenezi wa mradi limefafanuliwa zaidi katika Sura ya 5, Hatua ya 9. Katika hatua hii, SLM lazima lifikirie uhitaji wa kuainisha vijiji kadhaa vya uenezi wa mradi vitakavyofikiwa baada ya RIPAT kutekelezwa katika vijiji nane vya mwanzo.

Katika mchakato wa kuchagua eneo, SLM lifanye mchanganuo wa wadau na kubainisha wahusika mmoja mmoja, vikundi vya watu, taasisi au mashirika yatakayoonesha uhitaji katika kufanikiwa au kushindwa kwa mradi wa RIPAT. Pindi eneo zuri la kufanyia mradi likiainishwa, hatua itakayofuata ni kukutana na mamlaka husika za serikali.

## Hatua ya 2: Mikutano ya utambulisho kwa viongozi wa serikali

Mikutano ya utambulisho na viongozi wa serikali inalenga kuweka au kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi husika za serikali kwa kuhakikisha kuwa wanahusishwa kikamilifu na miradi kuwa na baraka zao. Kuhusika kikamilifu kwa viongozi husika wa serikali katika ngazi ya mkoa, wilaya na kata ni muhimu katika kuhakikisha kuwa mradi unapokelewa kikamilifu na jamii na wanakijiji na msaada huu unapatikana kutoka katika mamlaka zinazohusika katika uenezi nje ya vikundi vya awali.

Kama SLM limeshaainisha eneo ambalo limeona kuwa litafanyia kazi, lengo la mikutano na mamlaka za serikali ni kufanya utambulisho wa wazo la mradi, kuthibitisha uzuri wa eneo lililochaguliwa na kuomba ushirikiano wa mamlaka katika kufanya mchakato wa utafiti wa awali. Kama shirika bado halijaainisha eneo linalofaa kufanyia mradi, mkutano na

**Jedwali 3.1** Hatua za kufuatwa katika kuanzisha mradi

| *Hatua* | *1. Uchaguzi wa maeneo ya mradi* | *2. Mikutano ya utambulisho na viongozi wa wilaya* | *3. Uchanganuzi wa hali halisi na andiko la kapu la uchaguzi* | *4. Mchanganuo na maandalizi ya mradi* |
|---|---|---|---|---|
| Chakufanya | Shirika linalotekeleza linatembelea na kuainisha maeneo ya mradi | SLM linakutana na uongozi wa wilaya kwa ajili ya yafuatayo:<br>• Kulitambulisha SLM.<br>• Kuutambulisha mfumo wa RIPAT<br>• Mjadala kuhusu maeneo na makundi yanayolengwa<br>• Kujadili nafasi ya SLM na viongozi wa maeneo husika na kujadili utawala na uratibu | Timu ya wachanganuzi wa hali halisi:<br>• Kutembelea vijiji vilivyolengwa na kufanya mbinu shirikishi ya tathmini (PRA)<br>• Kuandaa kapu la uchaguzi linalofaa kwa maeneo hayo<br>SLM<br>• Litaendesha mkutano wa mpango mkakati kukubaliana juu ya kapu la uchaguzi | SLM<br>• Linaandaa mpango wa mradi na bajeti kulingana na mahitaji ya wafadhili<br>• Linaandaa uzinduzi wa mradi ikiwa ni pamoja na kuajiri na kutoa mafunzo kwa meneja wa mradi na wawezeshaji wa vikundi na maandalizi ya vifaa vya kufundishia vikundi kulingana na kapu la uchaguzi lililokubaliwa |
| Maoni | Mambo muhimu ya kuzingatia ni<br>• Umbali kati ya kaya na nyingine<br>• Hali ya hewa inayofaa kwa kilimo<br>• Utamaduni na mipango ya maisha | Hii inaweza kuchukua mikutano zaidi ya mmoja na inahusisha uongozi wa mkoa na wilaya | Timu ya wachanganuzi wa hali halisi kwa kawaida inajumisha KP, wataalamu na wawakilishi wa wilaya ikiwa ni pamoja na maafisa ugani wa maeneo husika | Muundo halisi na namna ya andiko la mradi lazima yalenge mahitaji ya mfadhili |

mamlaka husika unaweza kuwa wa msaada katika kuorodhesha majina ya vijiji vinavyohitaji kufanyia mradi.

Ni muhimu wazo la uenezi likajadiliwa na serikali za mitaa ili kueleweka. Inatarajiwa kuwa mwendelezo wa kazi za mradi wa RIPAT ni jukumu la mamlaka za vijiji na serikali. Mfumo wa ugani utahusika zaidi. Matarajio haya lazima yawasilishwe na yajadiliwe kutoka mwanzoni kabla shughuli zozote za miradi kuzinduliwa. Hii inahitaji uhusishwaji wa mamlaka za serikali za mitaa (kutoka wilaya hadi kwa jamii) kupitia mikutano mbalimbali.

## *Mikutano na mamlaka za mkoa na wilaya*

Kama shirika halikuwahi kufanya kazi katika mkoa au wilaya husika, inashauriwa kwanza kukutana na uongozi wa mkoa. Viongozi hawa wanaweza kuwa Katibu Tawala wa Mkoa (KTM) au Mshauri wa Kilimo wa Mkoa (MKM). Kama ikiwezekana MKM ahudhurie mkutano wa kwanza utakaowahusisha viongozi ngazi ya wilaya.

Katika ngazi ya wilaya, ni muhimu sana kuonana na Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya (TMHW). Mlango wa kuingilia hapa ni Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya (AKMW - DALDO). AKMW atalitambulisha shirika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya (MHW) ambaye atapanga mkutano na TMHW.

Mojawapo wa mambo yatakajadiliwa katika mkutano huu wa TMHW ni pamoja na: -

- Kulitambulisha shirika litakalotekeleza mradi
- Umuhimu na malengo ya RIPAT, yaani kupunguza umaskini na kuongeza uhakika wa chakula katika kaya kwa kuainisha kapu la uchaguzi linalofaa kulingana na hali ya hewa katika maeneo yaliyolengwa, na uhalisi wa RIPAT
- Maeneo yaliyopendekezwa katika kutekeleza mradi na yale ambao mradi unategemewa kuenezwa
- Majukumu ya washiriki mbali mbali katika mradi, na matarajio matokeo
    * Mahusiano ya kazi kati ya shirika na wilaya; mradi utafanya kazi kwa karibu na serikali ya mtaa, na zaidi maafisa ugani wa kata na vijiji (Angalia Kisanduku 2.1 kuhusu ushirikiano na maafisa ugani).
    * Wazo la uenezi baada ya kumaliza mradi; inatazamiwa kwamba wakulima waliofanya vizuri (wakulima vichocheo) watafanya kazi pamoja na maafisa ugani katika kueneza maarifa na ujuzi uliotokana na mradi. Uenezi huu (pamoja na ufadhili wake) vitakuwa ni majukumu ya wilaya kusimamia.
- Utafiti wa hali halisi wa awali katika vijiji vilivyopendekezwa, pamoja na tarehe na uainishaji wa wahusika vitapangwa.

Baada ya mkutano kati ya TMHW na shirika, wawakilishi wataendelea mbele zaidi kwenda katika ofisi ya AKMW kupata takwimu mbali mbali za awali na kupata uelewa mzuri wa eneo, hali yake na matatizo yake. Ofisi ya wilaya siku zote huwa ina kumbukumbu iliyobeba taarifa, ramani na machapisho mbalimbali. Endapo wilaya imefanya zoezi la 'Fursa na Vikwazo Katika Maendeleo' katika vijiji itakuwa na taarifa za kutosha kuhusu vijiji na mipango ya kazi zao za maendeleo.




Wawakilishi wa shirika wakiwa katika mkutano na uongozi wa mkoa na wilaya kutafuta ushirikiano na msaada




Majadiliano katika kikundi cha wanaume na wanawake wakiwa wametengana

## Hatua ya 3: Utafiti wa awali na wasilisho ya kwanza ya kapu la uchaguzi

Utafiti makini wa awali ni muhimu sana. Matatizo na mahitaji ya jamii (yanayohisiwa na yanayoonekana) ikiwa ni pamoja na sababu na matokeo, lazima yachanganuliwe katika njia ya ushirikishwaji ya suluhisho linalofaa kupatikana na kazi kupangwa. Ni muhimu kukumbuka katika RIPAT, maendeleo hayapatiwi jamii au mtu mmoja mmoja bali maendeleo yanapatikana kwa jamii na mtu mmoja mmoja kuyafanyia kazi. Ili kufanikisha maendeleo, SLM linafanya kazi kwa karibu na jamii iliyolengwa ili kukidhi mahitaji yao.

Mbinu shirikishi ya tathmini (PRA) inatumiwa na shirika. Ni muhimu sana kwa viongozi wa wilaya pamoja na maafisa ugani kushiriki katika zoezi hili. Vijiji vilivyochaguliwa vinatembelewa na kukusanya takwimu na taarifa muhimu kwa kutumia mbinu shirikishi ya tathmini (tazama Kisanduku 3.1). Changamoto na fursa zinaainishwa na taarifa kukusanywa kwa mfumo mzuri kwa ajili ya mchanganuo. Taarifa hizi zitatumika katika mipango madhubuti na muhimu katika kazi ambazo mradi utazifanya ili kufikia malengo yake.

*Epuka kuweka matarajio makubwa kwa watu wakati wa mchakato wa mipango!*

Wakati wa kufanya mchakato wa mbinu shirikishi ya tathmini ni muhimu kuepuka matarajio mengi yasiyo ya muhimu kwa jamii. Watu wanaweza kufikiri kuwa shirika litakuwa linafanya miradi ya kugawa vitu au kama chakula au mbolea kwa ajili ya kutatua matatizo ya uhaba wa chakula walio nao.



Matembezi mkato wakati wa kufanya utafiti wa awali

## Kisanduku 3.1 Vifaa vya Uchambuzi Shirikishi (PRA)

Baadhi ya njia zinazoweza kutumika wakati wa kufanya Mbinu Shirikishi ya Tathmini (MST). Kwa taarifa zaidi juu ya MST rejea miongozo mingine (tazama Kiambatanisho 8).

*Majadiliano katika vikundi*
...Yanalenga katika kukusanya taarifa za jumla, ufafanuzi kiundani, au kukusanya maoni, imani, na tamaduni katika kikundi cha watu waliochaguliwa (mara nyingi 8-12) wanaowakilisha makundi mbali mbali ya jamii (kama vile wanawake, wanaume, vijana, wazee, n.k). Maswali huulizwa kwa njia ya ushirikiano ambapo washiriki wako huru kuzungumza na wanakikundi wengine.

*Hojaji/dodoso iliyo wazi*
...inatumika kupata taarifa za uso-kwa-uso kwa mtu mmoja mmoja au kikundi katika jamii. Baadhi ya watoa taarifa muhimu wanachaguliwa kufuatana na taaluma zao au mambo wanayoyapendelea (kama vile viongozi wa jamii, maafisa ugani, waalimu, wafanya biashara wa eneo husika, na kamati za maendeleo ya jamii).

*Matembezi mkato*
...ni matembezi mpangilio au mfululizo wa matembezi yanayopitia katika eneo lililochaguliwa pamoja na watoa taarifa wa eneo hilo yatakayoruhusu kuangalia sifa za mazingira husika au/na shughuli kuu za wakazi. Mbinu hii inasaidia kupata taarifa zinazohusu mpangilio wa hali, matatizo na fursa katika kila eneo.

*Mfumo wa kazi*
...ni mpango wa shughuli kuu zinazofanywa na wanaume na wanawake katika kaya zilizobuniwa ili kuelewa vizuri nani anafanya nini. Taarifa hizi ni muhimu katika kuweka mipango na ratiba za mradi na katika kuunda kapu la uchaguzi na zaidi katika kupangiana kazi na majukumu kati ya wanakikundi.

*Mfumo wa usimamizi wa rasilimali*
...inatumika katika kufahamu nani katika kaya ana uwezo wa/utawala wa/ umiliki wa rasilimali mbali mbali za kaya, na inaweza kutumika kuainisha nafasi ya jinsia katika kumiliki rasilimali.

*Kalenda ya msimu*
...inatumika kuunda mzunguko au mgawanyo wa kazi na matukio ndani ya jamii kwa miezi 12, na inasaidia kuelewa mabadiliko ya msimu katika mfumo wa maisha. Kalenda ya msimu inaweza kuonesha mtawanyiko wa wafanyakazi wa kaya, upatikanaji wa chakula/pengo la chakula, mtiririko wa mapato, mgawanyo wa mvua n.k.

*Kupanga kwa kuoanisha*
...ni mbinu inayosaidia wanakikundi kulinganisha na kuagiza orodha ndefu ya vitu kwa mfano orodha ya matatizo. Kupanga kwa kuoanisha imekuwa ikitumika kwa muda mrefu katika kuweka vipaumbele kukiwa na mambo mengi katika orodha.

*Ulinganishi wa utajiri*
...ni mbinu ya kuelewa utajiri linganishi ndani ya eneo fulani au jamii. Vigezo muhimu au sifa za umaskini, kipato cha kati, au matajiri katika jamii yanaangaliwa kupitia majadiliano katika vikundi au hojaji isiyopangiliwa.

au wanaweza kufikiri kuwa shirika litakuja na mradi mkubwa na kuwaambia kitu cha kufanya. Ni muhimu kuwa wazi na kwamba lengo la kuwatembelea ni kupata taarifa na kujifunza kuhusu mbinu mbali mbali za maisha katika jamii. Katika hatua hii na kwa muda huu haijajulikana kama mradi utapitishwa katika kijiji hicho au la.




Kukosa matumaini katika jamii za vijijini – watu wakisubiri mabadiliko yaletwe na watu kutoka nje. Mradi wa RIPAT unafanya kazi ya kuumba maono/dira ya maisha bora ya mbeleni na kusaidia wakulima kugundua rasilimali zinazowazunguka bila kuzingatiwa lakini zinazoweza kuwasaidia kuondokana na umaskini kwa nguvu zao wenyewe (kwa eneo hili, upatikanaji wa samadi, umwagiliaji).

Ni muhimu kueleza kuwa kama hatimaye mradi umefadhiliwa hautakuwa mradi wa kutatua matatizo kwa urahisi kwa kutoa vitu bure au zawadi/msaada. Maendeleo siku zote yanaanzia katika kujitoa, mikakati na bidii ya washiriki.

### *Uainishaji wa utoaji kapu la uchaguzi*

Ni muhimu hasa kwa zoezi la MST kutoa matokeo ya uelewa wa ndani wa kilimo cha kisasa na la udongo wa mahali husika, maji, na hali ya hewa. Hii itasaidia kupatikana kwa taarifa muhimu katika kupata kapu la uchaguzi.

Matatizo yaliyoainishwa wakati wa MST yanachanganuliwa zaidi kwa kutengeneza mti wa matatizo utakaoonesha na kufafanua chanzo na athari kwa kuzingatia uhakika wa chakula na masuala ya maendeleo ya kilimo (mfano wa mti wa matatizo utaonekana baadaye katika sura hii). Mchanganuo halisi wa matatizo unatakiwa uhusishe juhudi za pamoja ikizingatia maoni kutoka pande zote mbili za wataalamu na wakulima. Timu ya uchanganuzi wa hali halisi inaainisha vikwazo na mizizi ya matatizo inayohusiana na uhakika wa chakula na maendeleo. Kwa hiyo sasa uchanganuzi wa matatizo ulio sahihi unatoa msingi ambao utasaidia kuunda mkusanyiko wa malengo na matarajio ya mradi, na itakuwa ni nyenzo muhimu katika kuweka vipaumbele vya kazi inayohitajika. Ni kawaida kuona mara nyingi wakulima wadogowadogo katika maeneo ya vijijini wakiwa na orodha ndefu ya matatizo katika kuendeleza maisha.

Kutokana na taarifa za utafiti wa awali zilizopatikana na kuchanganuliwa; orodha inayostahili ya kapu la uchaguzi-teknolojia na kilimo kinachofaa katika vijiji eneo husika lenye uwezo wa kuboresha kilimo cha kienyeji – inaandikwa. Kwa hiyo, kapu la uchaguzi linategemea sana mawazo kutoka kwa wakulima na wataalamu walioko katika timu ya uchanganuzi wa hali halisi.

### Kisanduku 3.2 Kapu la uchaguzi

Kapu la uchaguzi katika teknolojia lililokuwa likipewa vikundi vya RIPAT na wanakikundi mmoja mmoja linatengenezwa kutoka katika orodha ifuatayo

1. Kilimo bora cha migomba kwa kutumia mbinu bora
2. Kilimo hifadhi ambacho kinasisitiza kanuni tatu za msingi:
   - Kutifua/kugeuza udongo kwa kiwango cha chini, inayofanyika kwa kutumia ripa au majembe maalum ya mkono (Jembe la Zambia) badala ya kutumia jembe la kawaida
   - Kufunika udongo kwa matandazo na kupanda mazao yanayofunika ardhi
   - Mazao mchanganyiko na kufanya mzunguko wa mazao, kwa mfano kupanda au kuzungusha mahindi na mikunde. Mtawanyiko wa mazao unasisitizwa kwa kufanya kilimo cha mihogo bora, viazi vitamu na mbogamboga kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji pale inapowezekana na inastahili
3. Teknolojia baada ya uvanaji; kama uhifadhi, usindikaji, kuongeza thamani, matumizi katika kupata bidhaa mbalimbali na masoko
4. Ufugaji bora wa wanyama (ng’ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku) kwa upande wa aina zinazofugwa, mabanda, lishe na matibabu
5. Miti kwa ajili ya malisho, kivuli, kukinga upepo, mbao, kuni, rutuba katika udongo, mmomonyoko wa udongo na chakula (miti ya matunda-parachichi, machungwa, na maembe)
6. Udongo na uhifadhi wa maji, ikiwa ni pamoja na makinga maji na mbinu za uvunaji wa maji ya mvua
7. Mafunzo ya usimamizi wa fedha yanayolenga katika kuweka na kukopa kijijini

### *Mkutano wa kuweka mpango kazi wa mradi*

Ili kupata ushauri zaidi na kuhakikisha orodha ya vitu vilivyomo katika kapu la uchaguzi, SLM lifanye mkutano wa mpango kazi wa mradi. Katika washiriki lazima wawepo wafanyakazi kutoka wilayani, wataalamu, viongozi wa vijiji, viongozi wa kata, maafisa ugani, na wadau wengine muhimu katika maendeleo ya eneo husika.

Matokeo ya mchanganuo wa hali halisi yanawasilishwa katika mkutano wa mpango kazi wa mradi. Matokeo haya yatahusisha ufafanuzi wa mbinu za kilimo zinazotumika kwa sasa na teknolojia, uchanganuzi wa matatizo na orodha ya kwanza ya kapu la uchaguzi. Washiriki katika mkutano huu watajadili matokeo na kutoa maoni yao. Yatokanayo na mkutano ni makubaliano ya kapu la uchaguzi litakalotumika katika mradi wa RIPAT.

Kufuatia mkutano huu, taarifa ya mchanganuo wa mwisho wa hali halisi itaandaliwa. Taarifa hii itatumika katika kuandaa andiko litakalowasilishwa kwa mfadhili ili kuomba ufadhili wa mradi.

Katika kutekeleza miradi ya RIPAT mpaka sasa, kapu la uchaguzi lililopewa vikundi vya mradi limekwenda sawia, kila moja likihusisha aina tofauti za teknolojia ya mazao/mifugo ambazo zinawakilisha uboreshaji wa mbinu zinazotumika sasa (tazama kisanduku 3.2)

Mti wa matatizo uliooneshwa katika kielelezo 3.1 unafafanua kiundani chanzo na athari ambazo mradi wa RIPAT umezionesha. Mti huu husomwa kuanzia chini kuelekea juu.




Kielelezo 3.1 Mti wa matatizo

## Hatua ya 4: Mchanganuo wa mradi na maandalizi ya mradi

*Andiko la mradi* ni maandishi yanayolisaidia SLM kupata fedha za mradi. Wafadhili wengi wana muundo wa andiko na mambo muhimu yanayotakiwa kufuatwa. Uandishi wa mradi (andiko na mbao mantiki, chati ya shirika, mpango kazi na bajeti) yatasaidia utekelezaji wa mradi, na kwa hiyo andiko lazima lielezee kwa usahihi jinsi ambavyo mradi utatekelezwa.

### *Maandalizi ya kazi za mradi*

Wakati ambapo andiko limeshapelekwa kwa mfadhili kuna mlolongo wa kazi zinazohitajika kufanyika kabla ya shughuli za mradi kuanza:

### *Kuwapa mafunzo wawezeshaji wa vikundi*

Washiriki wenye sifa na misingi ya ujuzi muhimu katika nafasi ya uwezeshaji wanaweza wasiwe na uzoefu katika kufundisha watu wazima. Watakapoajiriwa, wawezeshaji hawa lazima wapate mafunzo ya namna ya kufundisha watu wazima kupitia kozi za nadharia na vitendo katika uwezeshaji wa vikundi vya RIPAT. ”akademia” ya RECODA inatoa mafunzo haya pale yanapohitajika (Tembelea www.recodatz.org). Kuongezea hili, inapendekezwa kuwa waajiriwa wapya baada ya mafunzo ya kitaaluma wajiunganishe na wawezeshaji wazoefu wa vikundi vya mwanzo ili wapate maarifa ya kivitendo.

### *Maandalizi ya vifaa vya kufundishia na mabango*

Baada ya kuainisha kapu la uchaguzi litakalotumika, SLM lazima lianze kuandaa vifaa vya kufundishia na mabango yatakayotumiwa na wawezeshaji wa vikundi wakati wa kufanyika kwa programu. Makaratasi ya kitaalamu juu ya mifumo na mbinu za uzalishaji wa mazao na mifugo yanapatikana kutoka katika vyanzo tofauti. Pia, miongozo ya uundaji na maendeleo ya vikundi na kuweka na kukopa inapatikana. Kiambatanisho na. 3 kina orodha ya vifaa muhimu na rahisi kupatikana.

Mabango yanayoonesha kapu la uchaguzi na michoro ya mambo ya kitaalamu ya miradi kama vile mnyororo wa mgawanyo wa wanyama na taratibu za jinsi ya kulipa mbegu na kupeleka utaalamu kwa wengine pamoja na vipando kwa wengine katika jamii, na vinginevyo, lazima viandaliwe vitumike katika mikutano ya vikundi.

**SURA YA 4**

# Kuanzisha mradi: Kuhamasisha na kukusanya jamii na kuanzisha vikundi vya wakulima

Mara baada ya fedha kupatikana, ndipo mradi utakuwa tayari kuanzishwa. Mbinu ya RIPAT inahitaji nguvu ya pamoja. Umiliki wa mradi kwa washiriki, mamlaka za serikali, (ni pamoja na maafisa ugani) na viongozi wa kijamii ni muhimu sana sio tu kwa mafanikio ya mwanzo ya utekelezaji, lakini pia kwa kuenea kwa teknolojia kwa kata zingine na vijiji ndani ya wilaya hiyo. Mipango ni mchakato wa mwanzo ambao ni taarifa ya muhimu ili kuhakikisha kuungwa mkono na kupata ushiriki sahihi kutoka kwa wadau wa nje na kuhitaji ushiriki wa ofisi za serikali kutoka ngazi ya wilaya hadi kwenye ngazi ya kata na vijiji. Jedwali la 4.1 hapo chini linaonesha namna ambavyo mikutano inatakiwa kufanyika na mambo muhimu ya kuongelewa. Kiongozi wa programu na meneja wa mradi watakuwa ndio viongozi wa msingi katika hatua hizi. Hata hivyo kwa kadri inavyowezekana ni muhimu kwa wawezeshaji wa vikundi kushiriki. Inashauriwa kuwa shughuli hizi za mwanzo zifanyike miezi miwili au mitatu kabla ya kuanza rasmi kwa utekelezaji wa mradi.

## Hatua ya 1: Kukutana na maafisa wa wilaya katika ngazi ya makao makuu ya wilaya

Watekelezaji wa mradi wanatakiwa kuandaa mkutano na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya (MHW) na wafanyakazi wengine muhimu wa wilaya. Mahali pa kuanzia ni kwa Afisa Maendeleo wa Kilimo na Mifugo wa Wilaya (AKMW) kupitia kwa Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya (MHW). Lengo kuu la mkutano huu ni kuwajulisha kuwa mradi uliopangwa umefadhiliwa na kufanya makubaliano ya mwisho juu ya utaratibu wa namna ya kushirikiana. Mapatano na wajibu wa kila mmoja vinahitajika kujulikana mapema ili kuepuka kutokuelewana kokote wakati wa utekelezaji na kwa sababu hiyo ni vema kuandikiana mkataba wa makubaliano (MwM) (angalia kiambatanisho cha 4D)

Wilaya lazima iteue Mratibu wa Mradi wa Wilaya (MMW) ambaye atakuwa ndio kiungo cha mawasiliano kati ya SLM na serikali. Katika mkutano huo orodha ya mwisho ya vijiji nane ambavyo vitafikiwa na mradi ndani ya miaka mitatu itakuwa imeshakubaliwa. Kutakuwa na orodha ya vijiji vya nyongeza vinavyolengwa kwa ueneaji wa mradi kwa kuwatumia wakulima vichocheo na maafisa ugani.

Maafisa wa wilaya na kata wanatakiwa kushiriki kikamilifu kwenye mkutano wa kijiji huu ni mkutano mkubwa wa kijiji unaofanyika ambapo RIPAT inatambulishwa kwa jamii yote na wakulima wanajiandikisha kwenye mradi.

Uwepo wa maafisa wa serikali na kuidhinisha kwao mradi wa RIPAT ni alama ya kuonesha umuhimu wa mradi na kutambulika kwake kiofisi na watekelezaji wake. Kutambulika kwa mradi kiofisi kunasaidia kupanda mbegu ya kwanza ya uaminifu ili kutengeneza matokeo mazuri ya baadaye kijijini. Ikiwezekana ni vema kumwomba Mshauri wa Kilimo wa Mkoa (MKM) kushiriki kwenye mkutano huo.

Sanduku 4.1 inatupa orodha ya mada zitakazofundishwa wakati wa mikutano kwa Makao Makuu ya Wilaya na kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata.

**Jedwali 4.1** Hatua zinazohusika wakati wa kuanzisha mradi

| *Hatua* | *1: Kukutana na mamlaka ya wilaya* | *2: Kukutana na kamati ya maendeleo ya kata* | *3: Mkutano wa kijiji wa uhamasishaji* | *4: Kuunda vikundi* |
|---|---|---|---|---|
| Chakufanya | • Tangaza kuwa mradi umefadhiliwa<br>• Mtambulishe mkuu wa mradi na wafanyakazi wengine<br>• Kuhakikisha vijiji vilivyochaguliwa<br>• Marudio ya hatua za utekelezaji<br>• Patana kuhusu wajibu wa viongozi na watawala<br>• Saini mkataba wa makubaliano | • Marudio kuhusu RIPAT na hatua za utekelezaji<br>• Elezea umuhimu wa msaada wa KMK wakati wa kuanzisha mradi kwenye mkutano wa kijiji na uundwaji wa vikundi kwa kila kijiji | • Tambulisha shirika na utoe maelezo yahusuyo wazo la RIPAT<br>• Kuweka sawa matazamio; kama vile kapu la uchaguzi.marejesho ya pembejeo, n.k.<br>• Hakikisha kuwa kila kitu kiko sawa kama vile;kazi, wajibu, matazamio,<br>• Kuwatambua wanaohitaji kujiunga na vikundi | • Eleza hatua kwa hatua jinsi RIPAT inavyofanya kazi<br>• Weka sawa matarajio kuwa washiriki watakuwa wanavikundi wazuri na eleza hii itahusisha nini<br>• Weka ratiba ya mpango kazi wa mradi<br>• Watangazie wanakikundi siku na mahali pakukutania |
| Maoni | Mkutano huu utamhusisha Mkurugenzi mtendaji wa wilaya na wahusika wengine muhimu baraza la utawala (TMHW) | | Mkutano huu wa hadhara ni msingi wa mafanikio wa kuunda vikundi na mwanzo mzuri wa mradi. Unaongozwa na viongozi wa vijiji. Wawakilishi kutoka KMK na wilayani lazima washiriki kikamilifu | Unahudhuriwa na watu ambao wameshachaguliwa na ambao wamejitoa kwa hiari yao wenyewe kushiriki kwenye vikundi |

Sanduku 4.1 Orodha ya mada zitakazoongelewa wakati wa mikutano ya Halmashauri ya Wilaya na KMK

1. Kuthibitishwa kwa kupitishwa kwa mradi
2. Marudio ya wazo la RIPAT na hatua za utekelezaji
3. Kuwahakikisha wanakijiji waliochaguliwa
4. Uteuzi wa msimamizi wa mradi wa wilaya na kuweka wazi wajibu wake kwa mawasialiano
5. Mapatano juu ya mahusiano kwa wilaya/kata; kazi na wajibu wao ikiwahusisha maafisa ugani wa serikali
6. Mazungumzo juu ya hatua za uenezaji wa mradi kwenye vijiji vingine
7. Kukubaliana juu ya maelewano yaliyoandikwa kati ya SLM na wilaya
8. Kupanga mikutano ya vijiji na jinsi wilaya na kata vitakavyohusika.

## Hatua ya 2: Kukutana na Kamati ya Maendeleo ya Kata kwenye makao makuu ya kata

Hatua inayofuata ni kukutana na Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK) kuwajulisha wajumbe wake wote juu ya ujio wa mradi wa RIPAT. Kwa wajumbe wengi wa KMK hii itakuwa mara yao ya kwanza kusikia kuhusu mradi wa RIPAT. Mara nyingi mkutano huu unafanyika asubuhi siku ambayo mkutano wa kijiji utafanyika. Msimamizi wa mradi wa Wilaya ndiye anayepaswa kuitisha mkutano wa KMK na pia kuwajulisha viongozi wa vijiji tarehe na muda ambapo mkutano wa kijiji utafanyika. Halmashauri ya kijiji ni lazima ijulishwe muda mapema, ili kuwawezesha kutangaza mapema kuhusu mkutano wa kijiji ili habari ziweze kuenea vizuri.

Lengo la mkutano wa KMK kufanyika kabla ya mkutano wa kijiji ni kuhakikisha kuwa viongozi wa kata wanaelewa vizuri malengo ya mradi, hatua za utekelezaji, na namna ya kushirikiana na jinsi wanavyotegemewa kujitoa kikamilifu. KMK ni kiungo muhimu sana, kinayo mamlaka ya kupanga na kusimamia miradi yote ya maendeleo ndani ya kata yake (kwa kawaida kata ina vijiji viwili mpaka vinne) viongozi wa kata wanatokana na asili mbali mbali ambazo ni Halmashauri ya kata, viongozi wa kata viongozi wa vijiji, maafisa ugani, viongozi wa kitaalamu kutoka idara mbali mbali, viongozi wa kidini, wawakilishi wa viongozi wa kisiasa, viongozi kutoka kwenye asasi zisizo za kiserikali na wadau wa maendeleo.

## Hatua ya 3: Uhamasishaji na ukusanyaji wa jamii kwenye mkutano kwa kila kijiji

Mkutano huu ndio chanzo cha kupata vikundi vyenye mafanikio na mwanzo mzuri wa mradi. Ni muhimu kwa viongozi wa kijiji kuwa wasimamizi wa mkutano wa kijiji na wawakilishi kutoka KMK na wa wilaya washiriki kikamilifu. Kila inapowezekana juhudi zote

zifanyike kuhakikisha kaya nyingi kwenye jamii zinahudhuria mkutano na ni muhimu SLM wilaya, kata na viongozi wa vijiji wanafanya kazi pamoja kuhakikisha kuwa hatua zote za uhamasishaji na ukusanyaji wa jamii zinafanikiwa. Kwa kawaida tukio hili linafanyika sehemu ya wazi ya serikali kama vile nje ya ofisi za serikali, shule au eneo la kanisa.

*Mkutano wa kijiji*




Mradi wa wa RIPAT unatambulishwa kwa jamii katika mkutano wa kijiji. Mkutano unasimamiwa na viongozi wa vijiji, na shirika linalotekeleza mradi na kata wote wakifanya kazi kwa pamoja kuhakikisha vikundi vimeundwa kwa ukamilifu na mradi mzuri unaanza.

Malengo makuu matatu ya mkutano huu ni:

1. Kuwasilisha mradi wa RIPAT kwa viongozi wa kijiji na kwenye jamii kwa namna ambavyo washiriki wanapata habari sahihi na kujua kwa wazi kinachotegemewa kutoka kwao;
2. Kukuza moyo/ari na nia ya 'ndiyo tunaweza' miongoni mwa wanakijiji; na
3. Kuunda vikundi viwili vyenye watu 35 kwa kila kimoja.

Viongozi wa kata na Msimamizi wa Mradi wa Wilaya (au mwakilishi kutoka wilayani) wanatarajiwa kuutambulisha mradi na SLM kwenye mkutano huo wa hadhara. Uumbaji wa maono bora ya baadaye kupitia uhamasishaji wa makini kwa jamii kwa uwezekano wa mabadiliko na kuwahamasisha wakulima kuchukua hatua ya kujiletea maendeleo yao wao wenyewe ni muhimu kwa mafanikio ya mradi. Katika mkutano huu hali ya umaskini na usalama wa chakula katika kijiji unachambuliwa kwa pamoja na ushiriki wa wale waliopo. Hii inafuatiwa na majadiliano kuwa ni kwa jinsi gani mradi wa RIPAT utasaidia kurekebisha hali hiyo kupitia juhudi za washiriki wao wenyewe, licha ya kushindwa kokote kulikotokea kwa miradi mingine iliyopita huko nyuma. Kuwaleta wakulima wengine mmoja au wawili kutoka kwenye miradi mingine ya RIPAT iliyopita kwaweza kusaidia, maana wanaweza kushuhudia mabadiliko yaliyotokea kwenye maisha yao ambapo RIPAT imewasaidia kuyafikia.




Ni sharti kuamini kuwa hali ya baadaye itakuwa bora ili kupata kuanza safari ya maendeleo. Ni muhimu kwa wakulima waweze kupiga taswira ya matokeo ya mafanikio yanayotokea. Vipengele na shughuli za mradi ni lazima vielezewe wazi ikiwa ni pamoja na teknolojia mpya ambazo zitatolewa ndani ya 'kapu la uchaguzi,' mfumo wa kurejesha pembejeo (angalia Sanduku 4.2) kazi na wajibu kwa wadau mbali mbali (SLM, viongozi wa kijiji, na maafisa ugani). Ni muhimu sana mkutano huu uwe shirikishi—epuka kuhutubia.

Maafisa ugani wanategemewa kuhusika kwenye mkutano wa kijiji na kwenye mchakato mzima wa ukusanyaji wa jamii na uhamasishaji ili kurahisisha upokelewaji wa mradi, kama vile kujisikia kumiliki na uenezaji wa jambo hili kwenye maeneo yao ya kazi.

Ndoto ya 'kaya bora' pia itawasilishwa. Mara nyingi wakulima hawana maono ya wazi ya nini maana ya maendeleo; kielelezo au mifano mara nyingi vinaweza kuwasaidia kufahamu wazo kwa ufasaha. Ni muhimu ieleweke wazi kwa watazamaji katika mkutano kuwa hatua ya maendeleo inayowakilishwa na kaya bora haitafikiwa ndani ya kipindi cha mradi kwa miaka mitatu lakini mradi utakuwa umepiga hatua katika mwelekeo huo. Uwe makini usiahidi sana usije ukawajengea matumaini makubwa ya kupata utajiri mkubwa ndani ya kipindi cha mradi. Hata hivyo tangu RIPAT ilipoanza mwaka 2006 wakulima wa RIPAT kadhaa wamepokea maono haya ya kaya bora na wamefanikiwa katika kuchukua hatua muhimu kuelekea huko.

Suala la 'pembejeo' linajadiliwa ndani ya sanduku 4.2. Sanduku 4.3 linatupa orodha kwa ajili ya mkutano wa kijiji.

## Sanduku 4.2 Pembejeo

RIPAT inalenga kuepuka dhana ya utegemezi kwa wafadhili, na kwa hiyo mradi hautoi zawadi ya bure au takrima. Kuna uvumi kuwa ikisikika kwenye jamii maskini kuwa mtu amepokea pesa au zawadi kutoka kwa mfadhili au kutoka serikalini, watu watatumia nguvu zao kujaribu kupata zawadi, wanaacha au wanapunguza juhudi zao za kupata maisha yao wenyewe.

Vikundi vitapewa pembejeo zinazohitajika ili kujaribu kapu la uchaguzi (kama vile aina ya mbegu bora, zana, na wanyama kwa ajili ya uboreshaji). Kwa baadhi ya pembejeo wakulima watarejesha gharama kamili kwenye SLM. Kwa pembejeo zingine malipo hufanyika kwa njia ya kutoa mazalio au watoto waliozaliwa na hao wanyama na kuwapa wakulima wengine ambao hawakupata mwanzoni. Kanuni zote zinaorodheshwa hapa chini wakati maelezo zaidi yanatolewa katika Sura ya 5, Hatua ya 9.

- Shamba la kikundi:
  Pembejeo (mbegu/vifaa vya kupandia, zana na madawa ya kilimo) kwa ajili ya matumizi ya mashamba la kikundi zinatolewa bure, hii inachukuliwa kama sehemu ya kujifunzia na mpango wa mafunzo unaohusiana na kapu la uchaguzi.

- Mwanakikundi binafsi:
  Wakulima wanaopenda kuchukua teknolojia hizi kutoka kwenye kapu la uchaguzi kwa ajili ya mashamba yao binafsi wanaweza kuomba SLM liwaletee pembejeo hizo. Hata hivyo mkulima anatakiwa kurejesha gharama zote kwa hiyo atarejesha asilimia 50 ya gharama kabla ya kupokea mbegu na asilimia 50 iliyobaki atarejesha baada ya kuvuna.

Kwa baadhi ya pembejeo, marejesho yanafanyika kwa kuwapa wakulima wengine kwa njia ya 'mnyororo wa mgawanyo'.

- Migomba:
  Wakulima wanaopenda kulima migomba wanapewa miche 10-20.
  Kwa marejesho yake kila mkulima lazima atoe mara tatu ya kiasi cha miche ya migomba alichopokea kutoka kwenye mradi kwa wakulima wengine nje ya kikundi, na lazima awafundishe kilimo bora (sehemu ya dhana ya 'kufundisha wengine watatu')

- Mbuzi, kondoo, nguruwe:
  Wakulima wanarejesha kwa kuwapa wanakikundi wengine majike wawili wa mwanzo kwa kufuata orodha iliyokubalika. Asilimia 100 ya madume na majike kutoka kwenye mifugo bora inatolewa kwenye kikundi.
  Jamii kwa ujumla wanaruhusiwa kutumia madume haya ili kuboresha mifugo yao ya asili, kwa hiyo inaongeza ueneaji wa mifugo iliyoboreshwa na kuigusa jamii kwa ukubwa zaidi.

Kama mazao yatakuwa yameharibika kwa sababu ya ukame, wakulima watasamehewa kurejesha mbegu walizopokea kama itakuwa imekubaliwa na SLM.

## Sanduku 4.3 Orodha kwa ajili ya mkutano wa kijiji

1. Baada ya kufika Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK), Msimamizi wa Mradi wa Wilaya na watekelezaji wa mradi (kiongozi wa mradi au meneja wa mradi – angalia Sura ya 2) wafanye mkutano mfupi na baraza la kijiji ili kuweka wazi mradi wa RIPAT na kanuni zake. Baadhi ya wajumbe wa baraza la kijiji watakuwa wameshiriki katika uchambuzi yakinifu wakati wa maandalizi ya mwanzo, kwa hiyo halitakuwa jambo jipya sana kwao.
2. SLM wataeleza kazi na wajibu unaotegemewa kutoka kwa uongozi wa kijiji mradi unakotekelezwa.
3. Baada ya utambulisho kwenye Baraza la Kijiji, Kamati ya Maendeleo ya Kata na Baraza la Kijiji watakwenda kwenye mkutano wa kijiji.
4. Mwenyekiti wa Kijiji atafungua mkutano na kumkaribisha Msimamizi wa Mradi wa Wilaya kumtambulisha kwenye hadhara.
5. Msimamizi wa Mradi wa Wilaya atautambulisha mradi kwa wanakijiji na kumkaribisha mwakilishi wa SLM kuelezea kwa undani habari za mradi.
6. Mwakilishi wa SLM lazima ajadili baadhi ya vikwazo vya maendeleo katika eneo hilo ambavyo vilifahamika wakati wa zoezi lililofanyika la utafiti wa awali.
7. Wakulima kutoka kwenye miradi mingine ya RIPAT iliyopita wanakaribishwa na kutoa ushuhuda wao.
8. Vikwazo ambavyo wakulima wa eneo hilo wanakutana navyo lazima vifanane na shughuli za RIPAT ili kuhakikisha usalama wa chakula na kuondokana na umaskini.
   - Wakulima wanaulizwa maswali rahisi ya moja kwa moja yahusuyo maendeleo ili kutambua fursa na vikwazo vya maendeleo katika kijiji chao.
   - Wanaulizwa tena uwezekano wa kuleta suluhisho ambalo wanafikiri litawasaidia.
   - Majibu yatakayotolewa yanatumika kuwasaidia wakulima kuelewa kile ambacho kimekuwa kikikosekana.
   - Uwakilishi unawekwa wazi kwa namna ambavyo dhana ya RIPAT inafanya kazi:
     * Kapu la uchaguzi
     * Kufanya kazi katika vikundi
     * Urejeshaji wa pembejeo
     * Kueneza mgawanyo wa mnyororo, yaani kwamba wanakikundi wa RIPAT wao ni 'mabalozi wa maendeleo' hapo kijijini na kila mmoja anatakiwa kuwafundisha wengine watatu.
     * Hata hivyo kuenea na kuendelea kupitia wakulima vichocheo na maafisa ugani.
9. Kazi inayotegemewa kwa kila mdau inawakilishwa (msisitizo unakaziwa kwa kazi ya serikali ya kijiji na jamii).
10. Meneja wa Mradi ni budi aeleze umuhimu wa kufanya kazi kwenye vikundi na aeleze kanuni za uundwaji wa vikundi na vigezo vya kuchaguliwa.
11. Muda wa kutosha kwa maswali uruhusiwe, na majibu kamili yatolewe.



Kaya bora ya mfano

## Hatua ya 4: Kuunda vikundi vya RIPAT

Ni muhimu kwa wakulima kuelewa habari zote za mradi kabla ya kujiandikisha. Ni wale walioelewa vizuri mradi ndio tu wanaoweza kujitoa kikamilifu. Sababu na faida za kuunda vikundi zielezewe: Vikundi vinaweza kutengeneza uchaguzi wa pamoja na kujiamini, kushirikishana ujuzi na kutetea haki zao katika jamii. Vikundi vinaweza kuboresha ufanisi wa mradi kwa ujumla kama wanaweza kuwa na uongozi mzuri wenye ushirikiano.

Mara baada ya kila kitu kuwa wazi viongozi wa kijiji wanatakiwa washirikiane na SLM kuunda vikundi viwili hapo kijijini. Kila kikundi kiwe na wanachama kati ya 30 na 35. Uongozi wa kijiji utawajibika kuandika majina ya wanachama wa vikundi hivi viwili. Uchaguzi wa vikundi hivi utafuata kanuni kadhaa.

Vigezo vya kuchagua washiriki:

- Ushiriki uwe wa hiari, na washiriki lazima wawe wamejitoa kikamilifu kwenye mradi.
- Mshiriki asiwe tajiri kufuatana na vigezo vya utajiri hapo kijijini.
- Mshiriki lazima awe mkulima na awe na ekari kati ya moja mpaka tano (hekta 0.4 - 2) ya eneo lake ili aweze kulitumia kwa njia bora kwa vitendo.

- Mshiriki awe na utayari na aweze kushirikisha mawazo yake mapya kwa wenzake na pia aweze kujifunza kutoka kwa wengine. Hii ina maana kuwa mshiriki awe na msimamo mzuri kwenye jamii.
- Kuwe na idadi sawa kati ya wanaume na wanawake kwenye kikundi, au wanawake wanaweza kuwa wengi zaidi.
- Kila kaya itoe mshiriki mmoja tu ambaye lazima awe na umri zaidi ya miaka 18. Wanakikundi lazima watoke hapo kijijini na ni vizuri wawe wanafahamiana.
- Wanachama wa vikundi ni lazima watoke ndani ya kijiji cha mradi na ikiwezekana wawe wanafahamiana.

Kufuatia uundwaji wa vikundi vyote viwili, uongozi wa kijiji, meneja wa mradi, mwezeshaji wa kikundi na wanakikundi waliochaguliwa watatengeneza utaratibu wa kikundi kukutana kwa mara ya kwanza, ikiwezekana iwe juma linalofuata.

# Sehemu ya 2

## Mwongozo wa Mwezeshaji wa Kikundi

**SURA YA 5**

# UTEKELEZAJI

Sura hii ifuatayo inahusiana na utekelezaji halisi wa shughuli za mradi wa RIPAT. Watu ambao wanahusiana na utekelezaji, mafunzo na kufundisha wahusika wa mradi ni wawezeshaji wa vikundi na Meneja wa Mradi. Sura hii inaelezea misingi ya mwezeshaji wa kikundi na hatua za kufuata kama mwezeshaji wa kikundi, ambazo zitasaidia katika utekelezaji. Hatua za Utekelezaji zinakuwa kwa mpangilio unaokupa mfumo mzima. Lakini kiukweli miradi mingi inahusiana na kazi za uwezeshaji wa vikundi ambavyo vinafanyika kwa pamoja na hivyo hatua za utekelezaji huingiliana. Kabla ya kuanza tunahitaji kukupa ushauri jinsi utakavyoweza kufanya kazi kama Mwezeshaji wa Kikundi (MK).

## Hatua ya 0: Kazi yako kama mwezeshaji wa kikundi

Kazi kubwa ya miradi ya RIPAT ni kuendeleza wakulima kupitia vikundi vyenye uongozi bora na kutoa/kuipeleka teknolojia ya kilimo bora kupitia vikundi. Kupeleka huku kunafikiwa kupitia uoneshaji shirikishi kupitia mashamba la kikundi kwa kutumia uzoefu na mbinu nzuri. Kama mwezeshaji wa kikundi wewe ni mtu muhimu sana. Yakupasa uwe na ushirikiano wa karibu na viongozi wa vijiji na maafisa ugani ili kufanya kikundi kiweze kumiliki mradi, muendelezo wa kazi za vikundi hata baada ya mradi kuisha na uenezaji wa teknolojia kwa jamii kubwa zaidi.

Kazi yako kubwa ni kushiriki kwenye mikutano ya kila wiki na wakulima kwenye vikundi vyao. Hakuna kanuni maalum ya jinsi ya kuviwezesha vikundi, lakini lengo lako linapaswa kuwa kusaidia wanakikundi kutekeleza mipango ya kikundi na kufikia malengo kupitia majadiliano, kutiana moyo, na kusaidiana kupanga na kufanya mambo mbalimbali. Utasaidia kubuni jukwaa la majadiliano ambalo wanakikundi wanajifunza na kupata elimu kwa pamoja. Jedwali 5.1 linaelezea kivitendo ushauri wa kuwaelimisha watu wazima. Kazi yako imegawanyika kwenye maeneo matatu:

- Mwalimu na mwelekezaji kwa ufundishaji shirikishi
- Mshauri wa kikundi
- Kuunganisha, kuratibu na kuwasiliana

### *Mwalimu na mwelekezaji kwa ufundishaji shirikishi*

Mradi wa RIPAT unahusisha 'kapu la uchaguzi' la teknolojia bora za kilimo ambazo kazi yake kubwa ni kuweka daraja la teknolojia. Ni muhimu kwa teknolojia hizi kufikishwa kwa vikundi vya wakulima kwa njia iliyo bora zaidi, na kwa ushiriki mkubwa wa wahusika, vilevile, ambazo zinafaa kwa mazingira na hali za wakulima hao. Yakupasa uwe tayari kuwafundisha wakulima teknolojia mpya na kuwaelekeza kwa vitendo kumudu njia mpya.

Yakupasa kuwa tayari kuwapelekea habari mpya wanakikundi, kwa nadharia na vitendo. Lakini la muhimu zaidi, inabidi uwe tayari kuwezesha na kufundisha mfumo wa elimu ya watu wazima ambao wakulima wanaufahamu, wenye kuleta maana, shirikishi na ambao unaifanya teknolojia kuendana na maeneo yao. Badala ya kutatua matatizo kwa niaba ya

kikundi na mtu binafsi kwa kuwapa suluhisho lililo bora kupitia vigezo au mbinu, waweza kuwapa taarifa mpya, kuwafundisha wakulima jinsi ya kuzitumia, kuwaongoza, kupata uzoefu wao, hatua ya maendeleo ya kikundi, kufikia muafaka na uongozi bora. Jedwali 5.1 linaelezea na kutoa ushauri jinsi ya kuwezesha watu wazima.

Utawaongoza wakulima kupitia mfumo ambao watajifunza jinsi ya kuchanganua mfumo wa kiikolojia wa kilimo ili waweze kujua kanuni zake, na utawaongoza wakulima kuanzisha mashamba ya vikundi rahisi lakini yenye ubora wa mazao mapya na kuonesha njia bora na mfumo mzuri wa ulimaji huku wakilinganisha na njia za kienyeji.

### *Mshauri wa Kikundi*

Ujuzi wote, teknolojia na pembejeo zinapitia katika kikundi, ambapo ndipo eneo la kujifunzia na kupashana habari. Mwezeshaji wa kikundi anatakiwa awezeshe wanakikundi kujiongoza wenyewe, kuchagua viongozi wao na kupanga kazi zao. Mafanikio ya mradi wa RIPAT ni pale vikundi vinapofanya vizuri. Lakini yakubidi uelewe kwamba wewe sio kiongozi wa kikundi, kadhalika sio mwanakikundi. Maamuzi yote yanafanywa na wanakikundi wenyewe. Kazi yako ni kuwezesha mafunzo na jinsi ambavyo wanaweza kufanya maamuzi.

Kutembelea kikundi kutafanyika mara moja kwa wiki mwanzoni mwa mradi. Baadaye, uwezo wa uongozi wa kikundi utakapoimarika na uwezo wa kikundi kufanya maamuzi na kujiongoza usaidizi wako kama mwezeshaji utaanza kupungua taratibu. Baada ya miaka mitatu ya utekelezaji wa mradi, wanakikundi watahitimu na hautakuwa unakiwezesha tena kikundi. Kwa hiyo, kazi yako kubwa itakuwa ni kukiwezesha kikundi kujitegemea, kuwa na hali ya umiliki, kuweza kujimudu wao wenyewe kimaisha na kuhakikisha kwamba washiriki ambao ni wanakikundi wanajiletea maendeleo yao wenyewe. Kazi yako, kwa hiyo, inabadilika taratibu kadri muda unavyokwenda baada ya kuanzisha, unachofanya ni kuongoza na kusisitiza na mwishoni kushauri na kuelekeza.

### *Kuunganisha, Kuratibu na Kuwasiliana*

Kama mwezeshaji utahakikisha uratibu na mawasiliano mazuri kati ya vikundi vya RIPAT na viongozi wa vijiji na maafisa ugani. Ni muhimu kuwa na uelewa mkubwa wa kazi za viongozi wa vijiji na maafisa ugani (angalia Sura ya 2, Kisanduku 2.1). Ni lazima vilevile kukichunga/kukiangalia kikundi kisiongozwe na mamlaka za nje na watu binafsi. Vikundi vya RIPAT vinafundishwa jinsi ya kutetea haki zao kwa manufaa ya maeneo na vijiji vyao, na kama mwezeshaji yakupasa kuwafundisha kama inavyoelezwa kwenye (Hatua ya 6 hapo chini).

Maendeleo ya vikundi vya RIPAT hayana budi kutolewa taarifa kwa viongozi wa vijiji na shirika husika kila mwezi. Utakisaidia kikundi kukusanya taarifa za maendeleo yao, na kusaidia viongozi wa vikundi kusimamia maendeleo na kuandika taarifa za vikundi (hii inaelezwa kwenye Sura ya 6). Kwa kusoma zaidi juu ya kuendeleza vikundi, soma FAO (1994).

## Sanduku 5.1 Ushauri wa jinsi ya kufundisha watu wazima

Sanduku hili linaorodhesha jinsi ya kuwafundisha watu wazima na linapendekeza jinsi linavyofanya kazi katika muktadha wa RIPAT.

### Watu wazima wanapenda kujifunza katika hali zifuatazo:

*Mafunzo yaliyojikita katika vitendo na kutatua matatizo*
RIPAT inatoa maelezo ya ujumla na mifano ya kivitendo ili kuunganisha vitendo na nadharia na kuwasaidia wanavikundi kupanga jinsi ya kutumia teknolojia mpya kwenye mashamba yao. Lengo likiwa ni utendaji kwa kiasi kikubwa na nadharia kwa kiasi kidogo. Kumbuka kwamba 'uzoefu ni mwalimu bora kuliko wengine wote'.

*Kukuza hali chanya ya kujiamini*
RIPAT inajenga mafanikio ya mtu binafsi na kikundi kwa kuhusisha shughuli ambazo ni rahisi kuzifanya, na kusaidia washiriki kufanya kazi kwa ufanisi na kwa kujiamini kupitia kazi zao za vikundi. Anza na mafanikio madogo ambayo yatakupelekea kuyafikia yale makubwa zaidi. Jenga nia na ari ya maendeleo kwa kuthubutu kufanya mambo mapya; jaribu kuondoa umaskini kwa kubadilisha uwezo wao wa kufikiria na kujitambua, na kuwa na roho ya 'ndiyo tunaweza' na mtazamo chanya wa kimaendeleo.

*Unganisha mawazo mapya na yale wanayoyafahamu*
Kwenye RIPAT uwasaidie wanakikundi kukumbuka na kuchangia mawazo ya yale wanayoyafahamu kwa uzoefu wao. Jumuisha ujuzi walionao na mazoezi wakati wa mafunzo na majaribio shambani, na ruhusu mawazo na majadiliano inavyowezekana. Anzia na vile vinavyoeleweka au kujulikana kuelekea kwenye vile visivyoeleweka. Panga kutembelea kwenye mashamba ya mwanakikundi mmoja mmoja na uwape nafasi ya kuchangia mawazo juu ya mafanikio binafsi na jambo ambalo kikundi kimejifunza. Uwe tayari kuwafanya wanakikundi kufutilia mbali tabia za kutumia kilimo kisicho bora.

*Onesha heshima kwa unayemfundisha*
RIPAT huzingatia mahitaji muhimu ya wale wanaojifunza, mfano, kukaa kwenye kivuli unapowafundisha na kupata mapumziko panapohitajika. Tambua na thamini mchango wa mawazo wa kila mshiriki. Usimtete mtu au kikundi. Kuwa mwangalifu wa maneno unayoyatumia ili kukwepa lugha ambazo zinaweza kusababisha wasikuelewe. Usipoteze muda wa wanakikundi: uwe umejiandaa vizuri na uwepo kwenye kikundi kwa wakati.

*Ruhusu wawe na uchaguzi na mwelekeo wanaoutaka*
RIPAT inalenga kuviwezesha vikundi na wanakikundi kuelezea mahitaji yao. Watu wenyewe binafsi wanaamua ni kipi cha kufanya na kipi cha kutokifanya kutoka kapu la uchaguzi. Wape muda wa kujipanga kwa hatua zingine zinazofuata. Usijaribu kuingilia au kuwa mtatuzi wa shida zao. Ongeza na ujuzi wako ambao umekosekana na kusaidia wakati wa kufanya maamuzi katika kikundi ili kufikia muafaka wa jambo.

Ushauri mwingine mzuri ni:

### Muonekano
Hakikisha haiba yako ni nadhifu unapotembelea vikundi na vijiji. Epuka kuvaa vibaya au vizuri sana kupita kiasi. Mavazi na muonekano wako uendane na jamii na utamaduni uliopo.

### Jitambulishe
Waeleze wanakikundi wewe ni nani na wategemee nini kutoka kwako na unachotegemea kutoka kwao. Jiamini na onesha upendo na nia ya dhati ya kuwasaidia katika shida zao.

### Lugha
Kuwa mwangalifu na lugha unayotumia. Usitumie lugha ya mtaani/mjini kwa wanakijiji. Wafanye wakulima wajisikie kama wewe ni sehemu yao na mkombozi wao.

1 Kutokana na uzoefu wa miradi ya RIPAT na kuvutiwa na kanuni za mafunzo ya watu wazima; mwongozo wa AIM www.ipro/index/cms.filesystem.action/hospice/2_7.pdf, ambayo inatokana na Goodlad na maandishi ya www.pent.ca.gov/trn/principlesadultlearning.pdf

## Epuka migogoro
Migogoro ni sehemu ya maisha ya kikundi. Baadhi ya migogoro yaweza kuwa ni mchakato ambao unaweza kutoa nafasi ya mabadiliko. Baadhi ya migogoro yaweza kusaidia kikundi kupitia kwenye wakati mgumu ambao utawafundisha jinsi ya kupambana nayo na kuyapatia ufumbuzi. Lakini migogoro mingine yaweza kuwa hatarishi, inayosababisha kutokuelewana, hasira, kuumiza, maamuzi mabaya na inayoweza kusababisha kikundi kuvunjika. Kitu muhimu ni kusaidia vikundi kusimamia na kujinufaisha na migogoro inayojenga huku wakijiepusha na migogoro hatarishi ama kukabiliana nayo haraka kabla haijajitokeza.

Kuhakikisha kuwa kuna umoja kwenye kikundi ili kupunguza migogoro. Wanakikundi ambao wanatoka kwenye jamii moja wanaweza kuaminiana na wanaweza kutekeleza majukumu yao kwa pamoja. Watu walio na mafanikio kama vile wafanyabiashara na wakulima wakubwa, wanaweza kuwa na amri kwenye vikundi na wakatumia nafasi hiyo kwa manufaa yao, kwa mfano kununua na kuuza kwa bei ya jumla, kutoa mikopo isiyofaa au kuwashawishi wanakikundi kuwafanyia wao kazi. Kuhakikisha kwamba wanakuwa na katiba na sheria ndogo ndogo ili kuepuka migogoro ya ndani na kila mwanakikundi kufahamu haki na majukumu yake.

## Kuanza mafunzo
Vikundi viwili kwa kila kijiji vitaanzishwa kwenye mkutano wa kijiji na huu utakuwa wakati wa kukutana na vikundi kwa mara ya kwanza. Ni muhimu kuwa na vikundi vyenye mshikamano tangu mwanzo. Kwa hiyo mafunzo ya hatua mbali mbali za maendeleo ya kikundi, kuandika katiba ya kikundi, na uongozi bora ni vitu ambavyo vinapewa kipaumbele tangu mwanzo. Mambo mbali mbali yanahitajika kufahamika kabla ya mafunzo ya kapu la uchaguzi hayajaanza kwenye vikundi. Malengo na mategemeo yafahamike wakati wa vikao vya mwanzo na wanakikundi wapewe kazi za kufanya wakati

wanasubiri teknolojia za kilimo kuanza. Bila kuwa na vikundi vyenye umoja na mshikamano, mafunzo ya teknolojia mpya za kilimo hazitakuwa na ufanisi. Vikundi vyote vinaweza kusambaratika au watu wengi kuacha vikundi kabla ya mwaka wa kwanza wa mradi kuisha. Hivyo, uwezeshaji kuhusu mshikamano kwenye kikundi ni muhimu sana tangu siku ya kwanza.

Walau kikundi kitakuwa tayari kimejipanga, kimechagua uongozi na kimeshatengeneza katiba yake, kabla ya shughuli za kilimo kuanza. Hata hivyo, ni muhimu maamuzi kama hayo ya kikundi kutokuharakishwa, lakini kikundi kipewe muda wa kuelewa suala zima la uongozi bora, kazi na majukumu ya viongozi na wanakikundi. Vikundi pia vinahitaji muda na uwezeshwaji mzuri ili kupata katiba iliyo nzuri ambayo itakuwa na misingi inayohitajika kutekelezwa kwenye kikundi na fursa zinazotolewa na mradi. Mchakato huo waweza kuchukua miezi kadhaa kumalizika na unahitaji msaada mkubwa wa mwezeshaji.

## Hatua ya 1: Mchakato wa Kuzoeana: Siku ya kwanza pamoja na kikundi

Kusudi la hatua hii ni kwa kikundi kukujua wewe kama Mwezeshaji na wewe kuwajua wanakikundi. Ni muhimu sana kwa wanakikundi kujua kuwa wewe sio kiongozi wala mwanakikundi. Kazi yako kama Mwezeshaji ni kusaidia na kuongoza kikundi kwenye suala zima la maendeleo.

Kwa sababu wanakikundi wanatoka kijiji kimoja wanaweza kupashana habari, ingawa wanaweza kuwa hawafahamiani vizuri. Waweza kuwawezesha kwenye suala zima la kufahamiana na ni vizuri Mwenyekiti wa Kijiji na Meneja wa Mradi wawepo kwenye mkutano wa kwanza pamoja na kikundi. Mchakato wa kufahamiana unaweza kufanyika kwa njia mbali mbali. Hapa ni baadhi ya mazoezi ya kivitendo ambayo waweza kuyatumia:

- Waambie wanakikundi wajitambulishe kwa kila mmoja kumtambulisha mwenzake ambaye anamjua, amtaje jina lake, analima nini kwake, na atoe taarifa fupi za huyo mwenzake. Hii inatoa picha ya umoja na inaondoa hali ya kutokufahamiana kati ya wanakikundi. Njia nyingine unaweza kuwaambia wanakikundi wakae kwenye mduara, na unawapa dakika tano za kuulizana maswali wakiwa wawili wawili na baada ya hapo kila mtu atamtambulisha mwenzake kwenye kikundi.
- Kukaa kwenye mduara. Mwezeshaji ampe mwanakikundi mmoja mpira mdogo chenye kamba au uzi, na mwanakikundi huyo atamtambulisha mmoja wapo anayemfahamu (anamfahamu vipi, anajishughulisha na kilimo gani n.k.). Baada ya kumtambulisha mtu wa kwanza anayefuata naye atafanya hivyo hivyo na kuendelea mpaka mwisho. Zoezi hili litafanya umbo kama la utando wa buibui na hii itaonesha kwamba sasa wanashikamana kwa pamoja. Zoezi hili laweza kuwa la kuburudisha na ubunifu, na uzungushaji wa mpira unaweza kukuonesha jambo moja au mawili ya jinsi ambavyo kikundi kinaweza kusimamiwa (Kutoka Groeneweg *na wenzake*, 2006, Sehemu ya II, ukurasa wa 30).

Kuna mazoezi mbalimbali ya kuonesha hatua za maendeleo ya kikundi kwenye vitabu vingine vya miongozo - Angalia Kiambatanisho cha 3.




## Hatua ya 2: Uchambuzi wa matatizo na uwezekano wa kupata matarajio ya kweli

Wakati wa hatua za mwanzo za mradi, ni muhimu kuendeleza na kuhimiza ari na moyo wa 'Ndiyo tunaweza' kwenye kikundi. Kikundi kinapokutana kwa mara ya kwanza, wanakikundi wanaweza kutokukifahamu wanachokitegemea na kama matarajio yao yatatimizwa. Wakati wa kikao cha kijiji moyo wa 'Ndiyo tunaweza' ndipo ambapo unatakiwa kuanzia. Ni muhimu kuendeleza moyo huo hata kwenye kikundi na kuwasaidia wanakikundi kuona fursa ambazo zamani zilionekana kama ni vitu visivyowezekana. Kuamini katika mafanikio ya baadaye ni njia nzuri ya kupata maendeleo.

Ingawa wazo kuu la RIPAT, kazi na majukumu ya RIPAT yanakuwa yameshaelezewa kwenye mkutano wa kijiji kabla ya wakulima kujiunga, ni vizuri kuhakikisha kwamba matarajio hayo yanakuwa ya kweli. Hii itasaidia kutokuwavunja moyo na kupelekea wanakikundi kuacha kikundi kwenye hatua za mwanzo. Suala zima la kulipia pembejeo lazima lieleweke na kukubaliwa na wanakikundi (Angalia Sura ya 4, Jedwali 4.2). Mwanzoni baadhi ya wanakikundi wanaweza kujiondoa wanapogundua kwamba hawapewi zawadi/vitu vya bure na badala yake kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya maisha yao. Yakupasa ukubali kujitoa kwao huko bila kuwakatisha tamaa na waweza kuruhusu watu wengine kuchukua nafasi za wale walioacha kikundi. Mara nyingine unaweza kukuta kwamba wale ambao walikuwa wanaupinga sana mradi baadaye wanapata shauku ya kuufanya baada ya kuona mafanikio yake. Undani wa jinsi ambavyo katiba inaweza kusaidia kuhudumia uingiaji wa wanakikundi wakati wa mradi kuanza inaweza kupatikana kwenye Hatua ya 4 hapo chini.

## *Hatua ya 2a: Majadiliano ya ujumla ya jinsi hali ilivyo katika jamii*

Kabla ya kikundi kutengeneza 'Mti wa Matatizo' kulingana na mradi husika wa RIPAT, ni vizuri kujadili hali ya umaskini kwenye jamii kwa ujumla. Ili mabadiliko yatokee, ni muhimu kwa wakulima kuelewa kwa nini wako hapo walipo na walitakiwa wawe wapi na kwa jinsi gani. Mti wa Matatizo wa kiujumla unaopatikana kwenye Sura ya 3 unaweza kukufungua macho. Hata hivyo, mti wa matatizo ulifafanuliwa wakati wa maandalizi na uchambuzi wa mradi, ambao umeandaliwa kulingana na eneo husika na kuunda misingi ya kapu la uchaguzi, hii inatumika sana kwenye mwongozo huu. Ni vizuri zaidi kuwa na mti huu wa matatizo kwa kuonesha kwenye bango. Ni muhimu kwa kikundi kutambua hali zao – chanzo, madhara na matokeo – kwenye mti wa matatizo. Hata hivyo, hatuingii kiundani kwa sasa. Hii itaelezwa kiundani kwenye Hatua ya 2c.

- Waambie wanakikundi waelezee maana ya umaskini na wajadiliane kama umaskini au upungufu wa chakula umepungua au umeongezeka kwa miaka 10 mpaka 20 iliyopita. Tumia viashiria kama vile uzalishaji wa chakula, miezi ya njaa, uwezo wa kaya kununua mahitaji n.k. Jadilini kwa kina kwa nini hali imebaki kuwa hivyo, na waulize washiriki wanakabiliana nayo vipi.
- Waulize washiriki kama wanakumbuka miradi mingine ambayo ilishawahi kuwepo kwenye jamii yao. Waelezee miradi hiyo ilikuwaje na ilileta matokeo gani. Waache wanakikundi waukumbuke huo mradi wa kwanza, lakini unaweza kupata taarifa za miradi ya zamani wakati wa upembuzi yakinifu wa mradi ambapo orodha yote inakuwepo.
- Jadilini inapojitokeza kwamba maendeleo hayatatokea kirahisi kama walivyotegemea kwa sababu tu shirika la maendeleo limewafikia kijijini kwao. Maendeleo yanahitaji utambuzi, upangaji wa rasilimali na bidii ya wakulima inakuwa ndio ufunguo wa kufikia malengo yanayohitajika.
- Waambie wanakikundi waelezee kwa muhtasari mambo ambayo yanazuia maendeleo kijijini na maeneo yao. Kwanza wanakikundi waelezee. Sababu hizo zaweza kuwa:
  - Vizuizi vya ndani kama vile ukosefu wa fedha, mbegu zisizo na viwango, bei ya chini n.k.
  - Vizuizi vya nje kama vile udhibiti wa bei wa serikali, vikwazo vya kupeleka bidhaa nje n.k.
  - Hali mbaya ya hewa kama vile mabadiliko ya hali ya hewa, mvua chache na isiyo na uhakika n.k.
  - Hali mbaya ya ardhi kama vile ukosefu wa rutuba kwenye ardhi, umwagiliaji kutokuwa toshelevu n.k.
- Jadilini jinsi ambavyo washiriki wanaamini kuhusu RIPAT kwamba inaweza kufanya mabadiliko – nini wanategemea.

## *Hatua ya 2b: Kutambua rasilimali zilizopo kwenye mazingira yao*

Rasilimali zinazopatikana kwenye mazingira yetu mara nyingi huwa hazitiliwi maanani na wahusika. Unapaswa kuwasaidia wanakikundi kuzitambua, kuelewa na kujua thamani ya

rasilimali mbalimbali walizonazo. Zoezi hili hufanywa kwa majadiliano ya pamoja kwa kutumia chati. Yaweza kuwa ni jambo zuri kuwauliza wanakikundi kutambua rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao hasa kwenye mashamba yao na jamii yao kwa ujumla kama maandalizi. Unaweza kuuliza maswali kama vile:

- Ni rasilimali gani watu wanazo?

  ... kazi, elimu/maarifa, ujuzi – hizi zaweza kutoka kwenye kaya za wanakikundi au kutoka kwenye jamii kwa ujumla (waalimu, maafisa ugani, matabibu n.k.)

- Tuna rasilimali gani kwenye mazingira yetu ya asili?

  ... ardhi, maji, jua, mimea, wanyama – hii ni pamoja na mito, mabwawa, chemchem, mifereji, visima, mbolea ya samadi, vifaa vya kuvutwa na wanyama n.k.

- Tuna rasilimali gani kwenye jamii yetu?

  ... hii inahusisha mila na utamaduni, uongozi wa kijiji na sheria ndogondogo, kanisa, msikiti, marafiki, ndugu, na familia yenye watu wa karibu n.k.

- Tuna rasilimali gani kwenye miundombinu na huduma mbalimbali?
  ... hizi zinahusisha fursa za kufikia mabenki, huduma za mikopo, majengo, barabara, huduma za umwagiliaji, vifaa, usafiri n.k.

Mara nyingi watu vijijini ni maskini wa fedha na hali ya kimiundombinu, lakini ni matajiri kwa kiasili, kiutu, na rasilimali za kijamii. Wasaidie kuondoa umaskini wa kifikra na wasaidie wanakikundi kuona fursa na mafanikio ya siku za baadaye. Waambie wafikirie kuhusu:

- Aina ya rasilimali ambazo tayari wameshazitumia na zile ambazo bado hawajazitumia
- Aina ya rasilimali ambazo zinakosekana kwenye jamii/kikundi/kaya
- Aina ya mabadiliko ambayo yatawaletea maisha mazuri

### *Hatua ya 2c: Uchanganuzi wa kina wa matatizo na ufumbuzi wake*

Zoezi hili pia linahusishwa kwenye majadiliano ya pamoja ya vikundi kwa kutumia chati. Uchanganuzi unadhamiria kuleta uelewa na ufahamu kwa wanavikundi wa kapu la uchaguzi ambalo linapatikana kwao kwa kupitia mradi. Uelewa wa matatizo ni wa muhimu ili kutambua na kupata ufumbuzi ulio bora.

#### *Kuandaa mti maalum wa matatizo kwa urahisi*

Uchanganuzi wa matatizo unahusisha kutambua ni mambo gani ya kutatua na jinsi ya kutafuta sababu na matokeo yake na mahusiano ya matatizo hayo. Endelea kujadiliana ni kwa nini wanakikundi wameshindwa kupata uhakika wa chakula na kuondoa umaskini, na kwenda kwa kina zaidi kwenye vyanzo na matokeo yake, na kulenga zaidi kwenye misingi ya miradi ya RIPAT. Wakulima waorodheshe dhana/watoe mawazo kuhusu chanzo cha umaskini. Yakupasa kutilia msisitizo kwenye mambo waliyoyataja na kuyapa kipaumbele panapohitajika. Kama wakulima wanasema udongo hauna rutuba, mnaweza kwenda kwa kirefu zaidi na kujadiliana kinachosababisha udongo kukosa rutuba na madhara yake. Ufanye wakati huu kuwa shirikishi zaidi ili kutambua matatizo ya msingi na vikwazo vya maendeleo.

### *Kuendelea na mti wa malengo*

Mti wa malengo unaandaliwa baada ya mti wa matatizo kukamilika. Kwa kifupi ni kwamba Mti wa malengo unatumia mfumo sawa na ule wa matatizo, lakini maelezo ya matatizo (hasi) yanageuka kuwa ya matumaini (chanya). Kama sehemu ya mazoezi, wakulima watajaribu kutambua rasilimali rahisi zinazopatikana kwenye maeneo yao ambazo zinawawezesha kufikia malengo yao.

RIPAT inakusudia kutumia rasilimali rahisi zilizopo ili kuweza kufikia malengo yanayotakiwa, hii ni katika kutekeleza maendeleo ya kiuchumi kwa kutumia mashamba ya wanakikundi. Miradi ya RIPAT inahusisha muunganiko wa mazao na mifugo, na yawezekana wakulima wakahitaji kuangalia rasilimali zinazohusiana na mifugo na mazao kwenye mashamba yao. Wakulima watambue sababu zinazozuia uzalishaji, na kufanya uchambuzi wa kina kupata mbinu zitakazoleta suluhisho linalofaa kwenye mashamba/kijiji.

Mfano: Kama wakulima wamejumuisha 'ukosefu wa rutuba kwenye udongo' kwenye mti wa matatizo, hivyo, maelezo yanaweza kujadiliwa kwa njia chanya ambayo ni 'kuboresha rutuba ya udongo' kwenye Mti wa malengo. Wasaidie na uwaongoze kutambua mitazamo na rasilimali zilizopo ambazo zinatumika kufikia lengo hilo, mfano, matumizi ya mbolea ya samadi, matumizi ya mboji, mzunguko wa mazao kwa kutumia mazao jamii ya mikunde; matumizi ya mbolea zenye madini inapaswa kujadiliwa ili kupata ufumbuzi mwingine. Wakulima waanze wenyewe kuorodhesha mawazo na sababu walizonazo. Baadaye unaweza kuonesha mawazo ambayo watakuwa hawajayasema. Rasilimali zilizopo hazihusishi sio tu vitu vinavyoonekana kwenye mashamba na mazingira yanayowazunguka, lakini pia muda wanaoutumia shambani na rasilimali watu inavyotumika kwenye kilimo. Kikundi kijadili rasilimali zisizotumika na zinazotumika chini ya kiwango.

## *Hatua ya 2d: Elezea kuhusu mradi wa RIPAT kwa kifupi*

Yakupasa uelezee kwa kifupi kuhusu mradi wa RIPAT na majukumu na mchango wa kila mwanakikundi. Hii ielezee mchakato mzima wa kutekeleza RIPAT kijijini. Maelezo ya kapu la uchaguzi yatolewe/elezewe, hii ni kujumuisha kapu la uchaguzi limetokeaje, ni jinsi gani kila mwanakikundi atafaidika nalo, dhana ya kupokea pembejeo na kulipia, n.k. Ni muhimu wakulima wakaelewa maelezo ya kila chaguo. Elewa kwamba ni wale wenye taarifa sahihi ndiyo wanaoweza kuhamasika na kuthubutu kufanya kitu kwa kujitoa kwa dhati.

Muulize kila mwanakikundi aelezee matarajio yake kwa mradi wa RIPAT. Hii ni fursa nzuri kurekebisha jambo ambalo litakuwa halijaeleweka na matarajio yasiyo ya kweli.

## *Hatua ya 2e: Kuandaa kalenda ya msimu*

Ni muhimu wakulima wakaifahamu kalenda ya msimu, ili kujua kazi zilizopo na jinsi kapu la uchaguzi linaweza kufaa kwenye mfumo wa kilimo. Kuelewa kalenda ya msimu ni muhimu ili kujua jinsi ambavyo utachagua teknolojia inayofaa na muda unaofaa, na kutilia maanani sababu nyingine za kiuzalishaji. Kwenye miradi ya RIPAT kwa sasa tumefanikiwa kutambulisha kilimo cha migomba hata kwenye vijiji ambako hawakuwahi kuilima wala kufikiria kwamba kilimo cha migomba kinaweza kufaa kwenye maeneo yao (Angalia maelezo ya uenezaji kwenye kitabu cha *Chaguo la Mkulima-Tathmini ya mtazamo wa uenezaji wa teknolojia ya kilimo Tanzania*). Mambo hayo ni muhimu kupata muda wa kuwaelezea wakulima na kuwasaidia kuelewa jinsi zao jipya litakavyofaa kwenye suala zima la kalenda ya mazao kwenye eneo.



Wanakikundi wakiandaa kalenda ya msimu. Wakati mwingine ni vizuri kuwagawanya wanakikundi kwenye vikundi vidogovidogo, mfano, kikundi kimoja kiandae kalenda ya msimu ya mahindi na kunde, na kingine kiandae ya mifugo n.k.

Zifuatazo ni hatua muhimu za kufuata:

- Wanakikundi wakae pamoja kujadili kalenda ya msimu ya mwaka; wajadili muundo wa hali ya hewa ya miezi kwa mwaka mzima.
- Wachore jedwali la mvua, joto na mambo mengine yanayohusiana na uzalishaji shambani.
- Sababu zingine kama vile magonjwa na matukio ya wadudu, zibainishwe kulingana na miezi kwa mwaka wakati ambao zinatokea.
- Matukio ya kiasili kama vile kiasi kikubwa cha vipepeo pia yabainishwe.
- Sababu zote huchambuliwa ili kujua zinavyohusiana na athari zake kwenye kilimo.
- Wakulima wanashauriwa kuchukua mazuri na kuyazuia au kuyafanyia kazi yale ambayo ni mabaya.
- Wakulima wabainishe pia jinsi ambavyo kalenda ya msimu inaweza kubadilishwa baada ya kutambulishwa kwa teknolojia ya miradi ya RIPAT (mazao na mifugo) inayopatikana kwenye kapu la uchaguzi.




## Hatua ya 3: Uchaguzi wa viongozi wa kikundi

Inaweza kuchukua muda mrefu kabla ya kikundi kuwa tayari kuchagua watu wanaowahitaji kuwa viongozi wao. Pia inahitaji muda ili kikundi kiweze kupata katiba inayofaa. Hili kwa ujumla sio tatizo. Fanya diplomasia, usiharakishe kuingia kwenye mchakato huo au kutoa maamuzi mapema. Kiongozi mzuri ni kigezo kimojawapo kwa maendeleo mazuri ya kikundi, na hivyo muda mzuri unahitajika kwa ajili ya kupata wagombea wazuri wa uongozi. Hata hivyo, ili kuruhusu kikundi kuanza shughuli za kilimo mapema, ni vizuri viongozi wa muda wakachaguliwa ili kuongoza kikundi kwa miezi mitatu ya kwanza kabla ya kufanya uchaguzi halisi wa viongozi. Kumbuka wanakikundi wanakuwa wameshafahamiana, lakini kwa kipindi hiki cha miezi mitatu wanakuwa wameshafahamiana zaidi. Ni vizuri kuwaruhusu wanakikundi kuendelea kufahamiana vizuri jambo ambalo litawasaidia kutambua na kuangalia wagombea wazuri wa uongozi kabla ya kufanya chaguo la mwisho. Kwa muda wa miezi mitatu ya kwanza viongozi wa muda wataongoza kikundi kufanya shughuli zifuatazo:

- Kutafuta mashamba ya kikundi
- Kuandika katiba na sheria ndogondogo za kikundi
- Kubuni jina la kikundi na kauli mbiu
- Kuhakikisha mahudhurio yanakuwa mazuri kwenye mikutano na shughuli za kila wiki, na kuhakikisha kwamba sheria ndogo walizokubaliana zinafuatwa.

Viongozi wa vikundi wa muda watakuwa pia kama kiunganishi kati ya kikundi na shirika linalowezesha mradi.

Mchakato wa kuchagua viongozi wa muda unahusisha majadiliano juu ya ubora na kazi za kiongozi bora. Wanakikundi wenyewe watajadiliana kutokana na uzoefu walionao kwamba kiongozi bora ni yupi/anakuwaje na kwanini kuwa na viongozi. Baada ya hapo, mnaweza kujadiliana kwanini kikundi kinahitajika kuchagua viongozi watatu ambao ni Mwenyekiti, Katibu na Mtunza Hazina. Kazi za viongozi ambazo wanatakiwa kuzifanya zimeorodheshwa kwenye Jedwali la 5.1.

Ni vizuri kama viongozi wa kijiji wakiwepo ili kuangalia mchakato wa kuchagua viongozi, hii ni katika kuchagua viongozi kwa miezi mitatu ya kwanza. Mfano wa jinsi ya kutekeleza mfumo wa uchaguzi ambao hufanyika kwa kura ya siri unaelezewa kwenye Kiambatanisho Na 1.

Uchaguzi wa viongozi wa muda unahitimishwa kwa kutangazwa kwa tarehe ya kufanyika uchaguzi mkuu. Baada ya uchaguzi, viongozi wa muda yawapasa kuanza haraka majukumu yao. Cha kwanza na muhimu ni kuhakikisha kwamba maendeleo ya kikundi yanaanza siku ya kwanza na kuendelea. Kumbuka wewe kama mwezeshaji wa kikundi unasaidia na kukielekeza kikundi kuchagua viongozi na kufanya maamuzi yaliyo bora.

Mafunzo ya uongozi ni sehemu muhimu sana ya mipango ya RIPAT. Baada ya viongozi wa kudumu kuchaguliwa, mafunzo ya kina ya uongozi hufanyika kila baada ya miezi mitatu ambapo viongozi wote kutoka vikundi 16 hukutana (Inaelezewa zaidi kwenye Hatua ya 11 hapo chini).

## Hatua ya 4: Kuandaa Katiba ya kikundi

RIPAT inalenga kuanzisha vikundi ambavyo vitafanya kazi pamoja vitakavyofanya vizuri na kufikia malengo, ni muhimu kukisaidia kikundi kuandaa katiba nzuri. Kwanza, unahitajika kuwaelewesha nini maana ya katiba na kwa nini inahitajika. Baadhi ya maswali na majibu kwenye Jedwali la 5.2 yanaweza kukusaidia.

**Jedwali 5.1** Sifa na majukumu ya viongozi wa kikundi

| *Sifa za kuangalia* | *Majukumu* |
|---|---|
| *Mwenyekiti wa kikundi* | |
| • Ajue kusoma na kuandika<br>• Asiwe mbinafsi<br>• Mpenda watu; aweze kufikiwa na kila mwanakikundi; awahudumie wote kwa usawa<br>• Akubali kukosolewa / kupata changamoto kutoka kwa wenzake<br>• Awe mhamasishaji wa ushiriki wa wanakikundi<br>• Aweze kuwajengea wanakikundi uwezo kutatua matatizo yao<br>• Mbunifu, mwenye bidii na jasiri kwenye utendaji wa kazi zake<br>• Mwaminifu na anayeheshimika<br>• Mwenye uwezo wa kupanga na kubuni mipango ya mbele<br>• Awe tayari kufanya kazi muda wa ziada<br>• Awe tayari kwa mafunzo ya ziada | • Kuanzisha na kuongoza kikao<br>• Kutaja ajenda na kuongoza majadiliano<br>• Kuhakikisha kwamba mkutano unafuata hatua zote na kwamba katiba inafuatwa na kuheshimiwa<br>• Kusimamia nidhamu na kutoza faini inapohitajika<br>• Kuongoza majadiliano na kuhakikisha kwamba mawazo ya kila mtu yanasikilizwa<br>• Kutatua migogoro<br>• Kuwakilisha kikundi kwa watu wasiokuwa wanakikundi, kama vile serikali ya kijiji<br>• Kuwa msimamizi wa mali za kikundi |
| *Katibu wa kikundi* | |
| • Ajue kusoma na kuandika kwa ufasaha<br>• Afahamu mahesabu<br>• Mwaminifu na anayeheshimika<br>• Awe tayari kufanya kazi muda wa ziada<br>• Awe tayari kwenda kwenye mafunzo ya ziada | • Kupanga muda na mahali pa kikao na kuwapa taarifa wanakikundi<br>• Kuandika mihtasari ya vikao<br>• Kusoma muhtasari wa kikao kilichopita<br>• Kutunza kumbukumbu za vikao<br>• Kuandika barua na taarifa kwa za kikundi<br>• Kumsaidia Mwenyekiti kuendesha kikao<br>• Kufanya kazi kwa pamoja na Mwenyekiti kuhakikisha kwamba katiba inafuatwa |
| *Mtunza Hazina* | |
| • Afahamu mahesabu<br>• Ajue kusoma na kuandika kwa ufasaha<br>• Mwaminifu na anayeheshimika<br>• Awe tayari kufanya kazi muda wa ziada<br>• Awe tayari kwenda kwenye mafunzo | • Kutunza kumbukumbu za mahesabu ya kikundi<br>• Kutunza kumbukumbu za miamala ya wanakikundi<br>• Kutunza kumbukumbu za mali za kikundi<br>• Kutunza akaunti ya kikundi<br>• Kusoma taarifa ya fedha ya kikundi inapohitajika<br>• Kukishauri kikundi njia bora za matumizi ya fedha |

**Jedwali la 5.2** Kuielewa katiba ya kikundi

| *Maswali* | *Majibu* |
|---|---|
| Katiba ya kikundi ni nini? | Ni makubaliano ya kanuni/sheria ambazo kikundi kitazifuata/kitazitumia. |
| Je, kikundi chenu kinahitaji katiba? | Ndiyo, ni kama mwongozo wa wanakikundi. Hii inasaidia kupunguza migogoro na kufanya maamuzi sahihi. |
| Je, katiba inamaainisha kitu kwa wengine? | Hapana, ni kwa ajili ya wanakikundi tu. |
| Ni nani wa kukubaliana na katiba? | Wanakikundi wenyewe. Hata hivyo, baadhi ya vifungu vinahusiana na mradi wa RIPAT. |
| Mchakato wa kupata katiba unakuwaje? | Misingi ya kupata katiba ni kupitia majadiliano kuhusu mahitaji na matatizo ya kikundi. Majadiliano haya yanafanyika kwenye mikutano ya wanakikundi wote. Yakupasa kukitaarifu kikundi wiki moja kabla kwamba uanzishaji wa katiba utajadiliwa wiki inayofuata. Ili katiba kupitishwa au kubadilishwa makubaliano yafanywe na angalau theluthi mbili ya wanakikundi wote. |
| Ni wakati gani katiba itaanza kutumika? | Kikundi kitaanzisha na kuipitisha katiba ndani ya wiki za kwanza za mradi wa RIPAT. Katiba inaweza kuongezwa au kubadilishwa wakati wa mradi. |
| Nani na wapi katiba itatunzwa? | Katibu wa kikundi ataitunza katiba pamoja na vitabu vya kumbukumbu za kikundi, na nakala atapewa mwenyekiti wa kijiji na kwa yeyote anayeihitaji. |

Kumbuka kuwa na mfano wa katiba ya vikundi unapofanya kazi yako ya kuvisaidia vikundi kutengeneza/kuandaa katiba yao. Mfano huo wa katiba unapatikana kwenye Kiambatanisho cha 2. Baadhi ya vifungu ni kwa ajili ya miradi ya RIPAT; hizi zinaonekana kwa *maandishi mlazo*. Unahusika na kuhakikisha kwamba vipengele hivi vya lazima vinakuwa wazi na vinaeleweka kwa wanakikundi tangu mwanzoni.

Vipengele ambavyo vinapaswa kuwepo kwenye kuandaa katiba vinaelezewa Jedwali la 5.3.

**Jedwali 5.3** Kuandaa katiba ya kikundi

| *Kipengele* | *Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa* |
|---|---|
| 1. Jina la kikundi | Kikundi kinapaswa kuchagua jina la kikundi chao ambalo litakuwa ndio kitambulisho chao. Jina linaweza kuwa la kilugha au Kiswahili. Lazima lionyeshe maana, maadili au sifa ambazo kikundi kinazihitaji. |
| 2. Mawasiliano | Makazi ya kikundi-ikiwezekana anuani. |
| 3. Maana ya jina | Jina linalochaguliwa lazima lieleweke maana yake kwa wote ili kuleta hali umiliki. |
| 4. Kibwagizo cha kikundi | Kikundi kinapaswa kuwa na kibwagizo, motto na kaulimbiu ambazo zitaongoza kwenye shughuli zao za maendeleo. |
| 5. Eneo la shughuli la kikundi | Hii inelezea eneo ambalo kikundi kitafanyia shughuli zake mkoa, wilaya, kata, kijiji na ikiwezekana kitongoji. |
| 6. Mlezi wa kikundi | Katiba itaje mtu ambaye atakuwa mlezi wa kikundi. Mara nyingi mwakilishi wa serikali ya kijiji ndiyo anapaswa kuwa mlezi. |
| 7. Lengo kuu<br><br>Madhumuni maalum | *Madhumuni ya kikundi cha RIPAT ni kuboresha maisha na kujenga uwezo wa wanakikundi wake kujimudu wao wenyewe na kuhakikisha mabadiliko yanapatikana, pia kusaidia watu wengine kwenye eneo hilo ambao sio wanakikundi kupata mabadiliko/ matokeo kama ya wanakikundi.*<br><br>Kwa kuongezea lengo kuu wanakikundi wenyewe yawapasa waunde dhumuni moja au mawili kwa maneno yao wenyewe. |
| 8. Uanachama<br>8.1 Majukumu ya wanakikundi | *Kwa RIPAT, wakulima wote wahusika wanajukumu la kufundisha wakulima wengine watatu ambao sio wana RIPAT kwenye jamii kile walichojifunza na walichokifanya. Kama kwa mfano, migomba imetolewa kwa mkulima mwanakikundi, mwanakikundi huyo atatoa miche mara tatu zaidi kwa wakulima wasiokuwa wana RIPAT; na kwa mifugo kama vile mbuzi au nguruwe, mkulima atatoa mzao wa kwanza jike kwa wanakikundi wengine kama inavyoelezwa kwenye mnyororo wa pamoja wa kugawana mbuzi wa shirika.*<br><br>Kikundi kijadiliane na kuongeza majukumu mengine ya wanakikundi. Hii itahusisha ushiriki wa kazi za shamba la kikundi, kumaliza kazi kwa wakati, mchango wa muda na fedha, n.k. |

| *Kipengele* | *Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa* |
|---|---|
| 8.2 Hatua za kufuata wakati wa kumuondoa mwanachama na kupokea mwanakikundi mpya kwenye kikundi wakati wa muda wa mradi | a) Mwanachama anayejiunga<br>Kama mtu anaomba kujiunga na kikundi wakati wa muda wa mradi, kikundi kikubaliane kiasi cha kiingilio anachopaswa kulipa. Kiingilio hiki kipitishwe na theluthi mbili ya wanakikundi.<br>b) Kumfukuza mwanachama<br>Kikundi kitaamua jambo litakalosababisha mwanachama kufukuzwa na jinsi ya kumpigia kura.<br>c*) Kuacha uanachama*<br>*Mwanakikundi anaweza kuacha kikundi wakati wa muda wa mradi, mtu huyo hatapewa mali au vitu alivyovipata kwenye kikundi. Mwanakikundi aweke sawa mahesabu yake na kulipa madeni yote anayodaiwa pamoja na pembejeo alizopewa (mbegu, vifaa, wanyama n.k.) kwa SLM.* |
| 8.3 Kujiondoa kwa kikundi wakati wa mradi | *Kikundi kinaweza kuvunjwa na shirika au kwa uamuzi wake wakati wa muda wa mradi, vifaa na vitendea kazi walivyopewa bure vitarudishwa kwa shirika. Wanachama binafsi ambao ni wanakikundi walipe madeni yao kama inavyoelezwa kwenye kipengele 8.2.c.* |
| 8.4 Kugawana faida za kikundi wakati wa mradi unaendelea | *Wakati mradi unaendelea, hakuna gawio lolote kutoka mapato ya kikundi watakalolipwa wanakikundi* |
| 9. Uchaguzi wa viongozi | *Uchaguzi wa viongozi uwe wa kidemokrasia ambapo kura lazima zipigwe kwa siri (Angalia Kiambatanisho cha 1 kwenye taratibu za kupiga kura). Mwanzoni mwa mradi, viongozi wa muda watachaguliwa kwa kipindi cha miezi mitatu. Baada ya miezi mitatu, viongozi wapya watachaguliwa. Viongozi waliokuwa wa mpito wanaweza kuchaguliwa tena iwapo wanakikundi wanawaona wanafaa, lakini kwa kutumia taratibu za kidemokrasia kama inavyoelezwa kwenye kiambatanisho cha 1. Uchaguzi mwingine unaweza kufanyika kila baada ya miezi 12. Kikundi kitaamua ni vipindi vingapi kiongozi anaweza kuendelea kuongoza.* |
| 9.1 Kazi za viongozi | Majukumu ya mwenyekiti wa kikundi yatajumuisha.<br>• Kuanzisha mkutano wanapokutana<br>• Kutangaza ajenda na kuongoza majadiliano<br>• Kuhakikisha kwamba kikao kinafuata utaratibu na kwamba katiba inafuatwa na kuheshimiwa<br>• Kusimamia nidhamu na kutoza faini inapotakiwa<br>• Kuendesha majadiliano na kuhakikisha mawazo ya |

| Kipengele | Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa |
|---|---|
| 9.1 Inaendelea | kila mtu yanasikilizwa na kuheshimiwa<br>• Kutatua migogoro<br>• Kukiwakilisha kikundi nje na kwa wasiokuwa wanakikundi kama vile serikali ya kijiji<br>• Kuwa wakili wa mali za kikundi<br><br>Majukumu ya katibu yanajumuisha:<br>• Kupanga muda na mahali mkutano utafanyika<br>• Kuandika mihutasari ya vikao<br>• Kusoma mihutasari ya vikao vilivyopita<br>• Kutunza kumbukumbu za kikundi<br>• Kuandika barua na taarifa kwa niaba ya kikundi<br>• Kumsaidia mwenyekiti kwenye vikao<br>• Kufanya kazi kwa pamoja na mwenyekiti ili kuhakikisha kwamba katiba ya kikundi inafuatwa<br><br>Majukumu ya mtunza hazina zinajumuisha:<br>• Kuweka kumbukumbu za mahesabu za kikundi<br>• Kutunza kumbukumbu za miamala za wanakikundi<br>• Kutunza kumbukumbu za mali za kikundi<br>• Kuandaa taarifa ya fedha<br>• Kutunza akaunti ya kikundi<br>• Kusoma taarifa ya fedha kwa kikundi inapohitajika<br>• Kukishauri kikundi njia bora za matumizi ya fedha |
| 9.2 Kamati ndogo ndogo za kikundi | Kikundi kitaanzisha kamati ndogo ndogo kulingana na teknolojia za kilimo zinazofuatwa na wanakikundi. Kila kamati itachagua kiongozi ambaye atatoa taarifa kwa mwenyekiti wa kikundi. Kazi za wajumbe wa kamati itakuwa ni kufanya ufuatiliaji kwenye teknolojia, mauzo ya mazao, na kuhakikisha kwamba ahadi zote zilizotolewa kulipia pembejeo zinatimizwa, kama vile malipo kupitia mnyororo wa kugawana mbuzi. |
| 10. Kazi kubwa ya kikundi na ratiba ya kukutana | Kikundi kielezee aina ya shughuli kitakachokuwa kinazifanya (kutoka kwenye kapu la uchaguzi) na kikubaliane mahali, muda na siku ya wiki kwa ajili ya kukutana na kufanya shughuli za mradi. |
| 11. Adhabu za kinidhamu kwa wanakikundi | Kikundi kielezee adhabu ambazo zitakuwa kwenye mfumo wa faini na ni kiasi gani na kama sio hivyo, ni adhabu gani zitafuatwa. Adhabu za kinidhamu lazima ziwekwe, mfano, kuchelewa kufika, kutokuhudhuria, kutokufanya shughuli za kikundi kama ilivyopangwa. |

| *Kipengele* | *Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa* |
|---|---|
| 12. Marekebisho kwenye katiba | *Katiba inaweza kurekebishwa wakati wowote kama theluthi mbili ya wanakikundi watakubaliana. Ibara zilizoandikwa kwa mlazo zinaweza kubadilishwa na theluthi mbili ya kura zote baada ya muda wa mradi kuisha na baada ya malipo kufanywa kwa wanakikundi kama wakiacha kama inavyoelezwa kwenye kipengele 16.* |
| 13. Mahesabu ya kikundi: Mapato na matumizi | *Mradi unapoanza, kikundi kitafungua akaunti ya kikundi. Akaunti ya kikundi itasimamiwa na viongozi waliochaguliwa ambao ni Mwenyekiti, Katibu na Mtunza hazina. Watahusika na kujaza kitabu cha fedha na kutengeneza mizania. Mapato na matumizi ya kikundi yawekwe/yaandikwe vizuri kwenye vitabu vya fedha. Taarifa ya fedha itatolewa kwa wanakikundi kila mwezi na kwa shirika itakuwa kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya ufuatiliaji.*<br>*Mapato ya kikundi yanatokana na kuuza mazao, adhabu na ada ya uanachama pale ambapo kikundi kinakuwa kimeamua kuwatoza wanachama wake.*<br>*Wakati wa kipindi cha mradi fedha za kikundi zitawekwa benki au SACCOS iliyo jirani kwa mapendekezo ya shirika au zitatumika kwa kuendeleza kazi za kikundi. Baada ya miaka miwili, kikundi kitawekeza kwenye mali zisizohamishika kama theluthi mbili ya wanakikundi na shirika watakubaliana. Makubaliano ya shirika yatategemea kama kikundi kina:*<br>• *Mahudhurio mazuri*<br>• *Uongozi bora na kama walikuwa wanafuata katiba*<br>• *Mapato ya kila wakati na utunzaji wake mzuri* |
| 14. Mwisho/Kikomo cha kikundi au mwanakikundi kuacha kikundi baada ya mradi kuisha | *Mwishoni mwa kipindi cha mradi kuisha, taarifa ya fedha itaandaliwa. Siku ya mwisho ya kumaliza mradi, madeni yote yawe yameshalipwa. Kikundi kinaweza kufilisiwa kama inavyoelezwa kwenye kipengele cha 15 au kinaweza kuendelea kama ushirika baada ya wale wanaohitaji kulipwa kuwa wamelipwa sehemu ya fedha zao kama inavyoelezwa kwenye kipengele cha 16.* |
| 15. Ufilisi wa mali na madeni ya kikundi | *Ufilisi wa mali za kikundi utafanyika baada ya mradi kuisha (kwa kawaida kila baada ya miaka mitatu) kama theluthi mbili watalipigia kura jambo hilo.*<br>*Kama shirika limetoa vitendea kazi bure kwa kikundi wakati mradi (kama vile ripa, mabomba ya kupulizia dawa, machimbuo na vifaa vidogovidogo) vitu hivi vitarudishwa kwenye shirika. Hakuna malipo* |

| *Kipengele* | *Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa* |
|---|---|
| 15. inaendelea | *yatakayotozwa na shirika kwa kurudisha vifaa hivyo. Mali za kikundi zitauzwa na fedha itakayopatikana itagawiwa kwa wanakikundi. Mali za kikundi ni kama zifuatazo:*<br>*a) Fedha taslimu kwenye mahesabu ya kikundi*<br>*b) Shamba lolote la kikundi la kukodisha (kawaida kwa mkataba wa miaka mitano). Shamba hilo kama itawezekana litakodishwa kwa muda uliobaki. Mfano mkataba wa kipindi cha miaka miwili kwa yeyote atakayelipa kwa bei ya juu*<br>*c) Shamba lolote linalomilikiwa na kikundi. Shamba hilo litauzwa kwa bei ya juu itakayokubaliwa*<br>*d) Mali nyinginezo*<br>*Fedha itakayopatikana kutoka a–d hapo juu itagawanywa kwa usawa kwa wanakikundi, mfano kiasi cha 1/30 kwa kila mwanachama kama kuna wanakikundi 30 wakati wa kuhitimisha mradi.* |
| 16. Malipo kwa wanakikundi wanaoacha iwapo kikundi kimeamua kuendelea kama ushirika baada ya mradi kuisha | *Mwanakikundi anaweza kuacha kikundi wakati wa kuhitimisha na akaendelea kukifanyia kazi kile alichojifunza hata kwenye shamba lake au kwenye vikundi vingine. Mwanakikundi anayeacha atapata theluthi mbili ya sehemu yake ya thamani ya kikundi. Kilichozalishwa na kikundi kinakokotolewa jumla yake kama ifuatavyo:*<br>*a) Fedha taslimu kwenye mahesabu ya kikundi*<br>*b) Kadirio la thamani yote ya shamba la kikundi, kama limekodishwa au linamilikiwa na kikundi; kama limekodishwa, thamani yake ni ile ya miaka iliyobakia kwenye mkataba. Thamani yake itatathiminiwa na wanakikundi wenyewe. Kama kikundi hakitakubaliana kuhusiana na thamani na iwapo wanakikundi wanahitaji, shirika litapanga kwa ajili ya kufanya tathmini ya thamani kwa kumtumia mtaalamu mwingine huru. Gharama ya kukadiria italipwa na kikundi.*<br>*c) Thamani ya mali zingine kama ilivyokadiriwa na kikundi. Kama makubaliano hayatafikiwa, hatua kama zinavyoelezwa hapo juu zitafuatwa.*<br>d) *Madeni yote lazima yalipwe.* |

| Kipengele | Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa |
|---|---|
| 16. inaendelea | Mfano: Kwenye kikundi chenye wanachama 30, wanakikundi 5 wanataka kuondoka baada ya kuhitimisha mradi, ambapo 25 wanahitaji kuendelea kama ushirika. Malipo ya wanaoacha inakokotolewa kama ifuatavyo:<br>Fedha halisi kwenye akaunti ya kikundi(kama ilivyo kwenye akaunti): TZS 500,000<br>Mapato kutoka shamba la kikundi(mauzo/kukodisha na kilichobaki TZS 1,000,000<br>Mali zingine TZS 500,000<br>*Jumla ya mali za kikundi* *TZS 2,000,000*<br>Theluthi mbili ya mali zilizopatikana itaweka misingi ya kukokotoa kiasi atakachopata mwanakikundi.<br>Kila mwanakikundi anayeacha kikundi atapata:<br>2,000,000 x2/3 x 1/30 = TZS 44,444<br>Kwa hiyo, kikundi kitalipa<br>5 x 44,444 = TZS 222,222. Hii italipwa ndani ya siku 60 baada ya barua ya maombi kupelekwa kwa mwenyekiti na mwanachama anayeacha kikundi.<br>(Kama pungufu ya theluthi mbili ya wanachama wanahitaji kuendelea kama ushirika, mali za kikundi zinatakiwa kufilisiwa, na wanakikundi wote kwenye suala hili la kinadharia watapokea 2,000,000/30 = TZS 66,666) |
| 17. Wanachama wapya wanaojiunga na ushirika mwishoni mwa mradi wa RIPAT | Wanachama wapya wanaweza kujiunga na kikundi baada ya kuthibitishwa na theluthi mbili ya wanachama waliobakia. Kiingilio kitakubaliwa kwa mfumo huohuo. Kiasi kinaweza kuwa, kwa mfano, thamani ya gawio yote iliyopatikana ni (TZS 66,666 kwenye mfano hapo juu, kama hakuna chochote kilicholipwa na wanakikundi walioacha). |

## Hatua ya 5: Kukuza mshikamano na uwezo wa kikundi sambamba na shughuli zote katika kipindi chote cha mradi

Kama ilivyoelezwa katika Sura ya 1, kikundi ni kipengele cha msingi cha RIPAT, kushirikiana kwa pamoja katika vikundi kuna faida – lakini kwa wengine inaweza pia kuwakilisha changamoto. Vikundi huundwa na kila aina ya watu, na kila mwanachama ni wa kipekee na ana tabia tofauti na mwingine. Wanatofautiana kulingana na asili yao, tofauti ya umri, rasilimali, maarifa na uzoefu. Mtoto huzaliwa na kukua, hivyo ni pamoja na vikundi-

vinakua/kuendelea na kubadilika. Ni muhimu kuvisaidia vikundi kuelewa hatua za ukuaji, sifa na tabia za wanakikundi zinavyoweza kutofautiana.

Aina chache za haiba/mwonekano inaweza kupatikana katika vikundi vyote. Zifuatazo ni aina za tabia za watu kama ilivyoorodheshwa hapa chini, uliza kila mwanachama wa kikundi kufikiria kuhusu aina ya tabia anayofanana nayo zaidi!
Hawatakiwi kutangaza hadharani walivyojiona; ni kujua ufahamu wa watu jinsi haiba yao inaweza kuwa na mchango chanya au hasi katika maendeleo ya kikundi. Mwamko huo ni muhimu sana kwa ajili ya kuendeleza ari ya kikundi.

- Walalamikaji: watu ambao mara nyingi hawaoni chochote kizuri katika maoni na maamuzi ya watu wengine na ni wepesi wa kulalamika
- Wajuaji: watu ambao daima wanashawishi maoni yao ni sawa na mara nyingi huwalazimu wengine kufuata maoni yao, wakati mwingine hujenga mgawanyiko ndani ya kundi
- Wanachama watulivu: Watu ambao mara chache hushiriki kutoa maoni yao na mara nyingi hawachukui jukumu lolote la kufanya maamuzi
- Wanachama Chanya: Ni watu ambao hufikiria kwa makini mawazo yao kabla ya kufikia mtazamo wao wenyewe. Hujiunga katika majadiliano na kushiriki na watu katika kufanya maamuzi. Mara nyingi watu hawa ni mihimili imara katika kikundi.
- Wanajadi: Watu ambao wanachukia mabadiliko ama wanahofia kujaribu kitu chochote kipya
- Wajenga daraja: Ni watu wanaopenda wengine wajisikie amani na furaha na kila mtu na maamuzi wanayofanya. Wako tayari kuchukua muda ili kufikia muafaka mzuri ambao pande zote wanafurahia (Carter, 2003: uk 24)

Kwa asili wanyama walichukuliwa kuwa na tabia mbalimbali na pia wanaweza kutumika katika kujadili tabia za binadamu/watu. Shughuli ya muhimu katika kikundi ni kujadili haiba za wanyama wafuatao hapo chini. Na fikiria ni mnyama yupi tabia zake zinakaribia kufanana na zake.

- Punda: Ni jeuri na habadilishi msimamo wake mara akishaamua kutokufanya kitu
- Simba: Anatumia nguvu na uwezo wake kupigana mpaka apate anachotaka
- Sungura: Hukimbia mbali mara moja anapoona shida au changamoto toka kwa mtu mwingine
- Paka: Hutaka kuhurumiwa na kila mtu
- Tausi: Hutaka kusifiwa kwa uzuri na rangi zake
- Kinyonga: Hatulii; hubadilika badilika rangi/ hubadili mawazo yake muda wote
- Kobe: Hukaa kimya bila kuchangia wazo lolote katika majadiliano

*Zoezi la nguvu ya mabadiliko katika kikundi*

Lengo la zoezi la nguvu ya mabadiliko katika kikundi ni kufanya kila mtu kwenye kikundi ajisikie kuwa ni wa muhimu katika kufanya vizuri kwa kikundi na mafanikio ya mradi kama lengo kuu na hamu ya kikundi kupata kitu kizuri. Kuna mazoezi au michezo mingi inayoweza kutumika kuelezea faida nyingi za kufanya kazi kama kikundi na mahitaji ya uongozi. Mfano uliotolewa hapo chini ni zoezi linaloonesha faida ya kuwa kwenye kikundi.

**Zoezi Faida ya kuwa kwenye kikundi**

| *Zoezi* | *Matokeo* |
|---|---|
| Njoo na mzingo mkubwa wa fimbo usiopungua sentimita moja za kipeuo. Mpe mwanakikundi mmoja fimbo moja na mwambie aivunje (hakuna shida).<br>Toa vijiti viwili kwa mtu mwingine na mwambie avishike pamoja na avivunje. Endelea kwa njia hiyo, kila wakati ongeza kijiti cha ziada.<br>Hatimaye mzingo utakuwa mnene na hakuna awezaye kuvunja. | Faida ya kuwa kwenye kikundi wakati wa masuala magumu ni lazima yapatiwe ufumbuzi:<br>Kama ukisimama peke yako au kama mko wachache tu, unaweza kushindwa au kuvunja<br>Pindi unapokuwa katika umoja na kushirikiana kwa pamoja hakika uko imara. |

Kuna mazoezi mengi katika mienendo ya kikundi ambayo inaweza kutumika wakati wa hatua za mwanzo za mradi. Wakati wowote ukijisikia kuna haja ya kufafanua suala linalohusiana na mshikamano wa vikundi, au ungependa kusisitiza juu ya jambo fulani kupitia zoezi sawa, basi usisite kufanya hivyo. Mazoezi kama haya hayahitaji kuchukua zaidi ya nusu saa. Angalia Kiambatanisho cha 3 kwa ajili ya maelekezo hayo.

## Hatua ya 6: Kuimarisha stadi za utetezi kwa vikundi

RIPAT inawezesha vikundi kwa kuwapa mafunzo ya utetezi. Kwa kutumia huu utetezi/ujuzi, wanachama wa kikundi wanatakiwa kuwasilisha mbele ya umoja, na vikundi hivi viwili katika kijiji hicho lazima walau kusimama pamoja iii kuwa na sauti ya pamoja katika kushughulikia masuala husika kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa jamii yao. Vikundi vya RIPAT hutumia utetezi katika maeneo kadhaa kama iliyoorodheshwa hapa chini:

### *Utekelezaji wa sheria ndogondog*

Inaweza kuwa hasara kubwa kwa vikundi vya RIPAT na wakulima wengine kama sheria ndogondogo hazitatekelezwa, hasa kwa sheria ndogo ya kudhibiti ufugaji huria kijijini. Katika vijiji vingi imezoeleka kwamba baada ya kuvuna mahindi shambani wanawaacha mifugo huria kula mabaki ya mazao mashambani. Mahindi ni moja ya zao muhimu la chakula na inachukua sehemu kubwa ya mashamba yaliyolimwa katika maeneo mengi ya Kusini mwa Afrika. Hata hivyo, tabia ya kuachia mifugo huria inaweza kuathiri sana uanzishwaji wa teknolojia mpya, kama vile muda mrefu au mazao ya kudumu, au mazoezi ya kilimo hifadhi na kufunika udongo kwa muda wote (mafunika ardhi na matandazo). Kwa mfano matatizo yaliyojitokeza wakati mradi wa RIPAT ulivyoanzisha mazao mseto pamoja na mbaazi ya muda mrefu. Hii aina ya mbaazi inachukua msimu mrefu kukomaa kuliko mahindi, lakini wanakijiji bado wataachia mifugo yao huria mara tu wanapovuna mahindi, na matokeo yake mbaazi zinaharibika. Wakulima wengine waliiga migomba-zao la kudumu ambalo linakuwa na majani ya kijani kibichi kwa mwaka mzima. Wakulima wa RIPAT walikua na shida ya kuchunga migomba yao iii isiharibiwe na ng'ombe au mbuzi wanaoachiliwa huria. Kama isiposhughulikiwa na umakini wao, matatizo kama haya yangeweza kufanya mradi kushindwa kabisa!




Hii pia ni moja ya sababu kubwa inayoonesha ni kwa nini ni muhimu kushirikiana kwa karibu sana na mamlaka ya kijiji.

Katika vijiji vingi nchini Tanzania sheria ndogondogo juu ya mifugo huria ni kweli zimewekwa - lakini hazitekelezwi na mamlaka hizo. Wakati mkulima binafsi anapeleka malalamiko ya sheria ndogondogo kuvunjwa, mtu huyo hasikilizwi. Lakini wakati vikundi viwili vya RIPAT ambavyo jumla ni watu 70 kwa pamoja wanaenda ofisi ya serikali ya kijiji na kuwaomba watekeleze sheria ndogondogo zinazohusiana na mifugo huria, wanakua na nafasi kubwa zaidi ya kusikilizwa!

Hatua unazopaswa kuchukua iii kusaidia kikundi ni:

- Kuhamasisha viongozi wa kikundi kupata nakala ya sheria ndogondogo za kijiji chao kwa ajili ya kikundi
- Saidia kikundi kujifunza na kuelewa sheria ndogondogo. Viongozi wa kikundi wanatakiwa kwenda kwenye baraza la kijijini kuomba utekelezaji wa sheria ndogondogo ambapo hii itasaidia kutatua matatizo, na kuomba sheria ndogondogo za vijiji zibadilishwe kama zilizopo hazitoshelezi
- Kuhimiza kikundi kwa kurejea sheria ndogondogo katika Mkutano Mkuu wa Kijiji na kusisitiza haja ya utekelezaji
- Wakumbushe viongozi wa kikundi kusisitiza matumizi ya sheria ndogondogo wakati wa mikutano ya uratibu na kuhakikisha kuwa viongozi wa vijiji wanaahidi kufuatilia utekelezaji

*Kukuza mipango ya maendeleo vijiji*

Vijiji vina ajenda/dondoo za maendeleo ambazo zimejadiliwa na Baraza Kuu na kamati ndogondogo za vijiji. Vikundi vya RIPAT vinaweza kuleta chachu katika mpango huu na kukuza utekelezaji.

Hatua unazopaswa kuchukua iii kusaidia vikundi ni:

- Kusaidia vikundi/kikundi kuelewa mipango ya maendeleo ya kijiji pamoja na vyanzo vya mapato vilivyoelekezwa katika utekelezaji wa mipango hiyo
- Saidia vikundi kupata na kuelewa mipango ya maendeleo katika kata na wilaya zao na kutoa msukumo wa utekelezaji wa mipango hiyo
- Kupitia matokeo yaliyojitokeza katika shughuli za RIPAT, viongozi wa vikundi wanatakiwa kuiga baadhi ya shughuli za maendeleo kutoka RIPAT na kuitekeleza katika mipango ya maendeleo ya kijiji!vijiji

**Mfano:** Kama kuna mradi wa maji uliopangwa, kikundi wanaweza kushawishi utekelezaji mara moja iii waweze kujipatia maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kwa ajili ya mifugo yao.

*Kusambaa*

Mradi wa RIPAT una mkakati wa kusambaza teknolojia za RIPAT kwa watu wengine katika kijiji hicho na vijiji jirani.

Kupitia mafunzo yako na uwezeshaji, vikundi wanapaswa kutetea kwa ajili ya kupata jukwaa kwa ajili ya kuhamisha maarifa watakayokuwa wamefaidi kupitia RIPAT. Moja kama jukwaa inaweza kutenga maeneo na muda wakati wa mikutano ya vijiji kwa viongozi wa kikundi na wakulima vichocheo kuongea. Jukwaa lingine lingeweza kutolewa kupitia mikutano maalum kama vile sikukuu ya wakulima. Unapaswa kuhakikisha kuwa maafisa ugani wanashiriki kikamilifu katika mchakato wa usambazaji.

*Mengineyo*

Mipango ya maendeleo ya vijiji, kata na wilaya inapaswa kurekebishwa mara kwa mara, kuanzia ngazi ya kijiji.

Hatua unazoweza kuzichukua kusaidia kikundi/vikundi ni:

- Hamasisha vikundi katika kushiriki katika vikao mbali mbali vinavyoandaliwa katika vijiji ambapo mipango ya maendeleo inajadiliwa
- Viongozi wa vikundi, kwa pamoja na viongzi wa vijiji na mamlaka za vijiji kuhakikisha mipango yao inajumuishwa katika mipango ya maendeleo ya kata na vivyo hivyo katika mipango ya maendeleo ya wilaya

**Mfano:** Vikundi vinaweza kushawishi kwa ajili ya kuboresha miundo mbinu kama vile barabara, mifereji ya umwagiliaji na masoko ya vijiji.

## Hatua ya 7: Kuchagua shamba la kikundi

Shamba la kikundi ni moja ya kipengele kikubwa cha RIPAT. Kusaidia kikundi kutafuta shamba zuri kwa ajili ya shughuli za kikundi ni hatua ya muhimu ambayo inatakiwa

kuchukuliwa baada ya kikundi kukutana mara chache, na wameelewa na kulipitisha kapu la uchaguzi ambalo limebeba teknolojia zote za kilimo zilizoletwa na mradi, na wamechagua viongozi wa kikundi wa muda/mpito. Kumbuka kwamba baadhi ya teknolojia mpya zilizopo hazijulikani kabisa miongoni mwa wakulima, kwa hiyo wanahitaji sana msaada wako katika kuchagua shamba linalofaa kwa mafunzo.

Teknolojia zilizoletwa na 'kapu' lazima zifae katika udongo husika, maji na hali ya hewa ya eneo hilo; hali ya hewa ya Afrika inatofautiana sana hata kwa umbali kidogo tu. Njia moja ya kilimo inayofaa na teknolojia zinaweza kutofautiana kutoka kijiji kimoja na kingine na hata kutoka shamba moja na shamba lingine. Uangalizi maalum, lazima kuhakikisha shamba la kikundi lililochaguliwa linafaa kwa zao hilo/zao husika.

- Miradi ya RIPAT iliyotekelezwa hadi sasa inahusisha mazao na teknolojia nyingi kama inavyoonekana katika kisanduku 3.2. Yaliyoorodheshwa hapa chini ni baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kama mradi unajumuisha teknolojia hizi mbili ambazo zimetekelezwa katika miradi yote ya RIPAT, yaani kilimo cha kisasa cha migomba na kilimo hifadhi.Hali ya mazingira: Kitu cha muhimu sana ni kuhakikisha udongo, maji na hali ya hewa vinafaa kwa zao/teknolojia iliyolengwa. Kimawazo mazao yote lazima yalimwe (jaribio, kuonesha na kuzalisha mbegu) na kikundi katika shamba moja la kikundi. Lakini kivitendo mara nyingi haiwezekani. Mazao huhitaji udongo wake maalum na mahitaji ya maji na ni muhimu kuhakikisha ulinganifu wa zao husika na shamba. Kikundi kinaanzisha shamba la migomba upande mmoja wenye uwezekano wa umwagiliaji au kuvuna maji ya mvua yanayotiririka na kuna vizuizi vya upepo, wakati shamba la kilimo hifadhi mara kwa mara linafanyika majaribio kwenye sehemu nyingine ndani ya kijiji hicho.



- Ufikikaji: ni lazima shamba la kikundi ikiwezekana liwe sehemu ambayo ni rahisi kufikika kwa wanakikundi na mwonekano mzuri kwa mradi. Wanajamii wanaalikwa kutembelea shamba la kikundi na kuona maendeleo ya mradi mara moja kwa mwaka katika sikukuu ya wakulima (angalia Hatua ya 12 hapo chini).
- Usalama: Mashamba ya kikundi lazima kuwa salama na wanyama waharibifu wanaozunguka ovyo na wezi ili kuzuia uharibifu wa shamba la kikundi. Ni vizuri sana kama mashamba la kikundi yatakuwa karibu na nyumbani kwa mwanakikundi.
- Ukubwa wa eneo: Ukubwa wa eneo la shamba la kikundi unaweza kuwa angalau kuanzia ekari moja ili kuhakikisha kikundi kinakuwa na eneo la kutosha kwa mafunzo ya teknolojia mbalimbali na kwa ajili ya kuzalisha mbegu. Shamba kubwa linaweza pia kuruhusu upanuzi wa shughuli za kikundi na kusaidia kikundi kupata kipato kwa kuuza mavuno kutoka shamba la kikundi.
- Kufanana kwa rutuba ya udongo: Tangu sehemu ya shamba itakapopimwa kwa ajili ya majaribio, ni muhimu kuwa na sehemu thabiti ya hali ya udongo kuwezesha mlinganyo mzuri kati ya teknolojia inayojaribishwa (angalia Hatua ya 8 hapo chini).

Migomba ni zao la kudumu linalohitaji upatikanaji mzuri wa maji. Linahitaji nguvu kazi kubwa wakati wa kuanzisha, lakini kama likitunzwa vizuri, mimea inaweza kuendelea kuzaa matunda kwa miaka mingi. Kwa hiyo kikundi kinatakiwa kuwa na shamba la migomba kwa ajili ya matumizi yao kwa angalau kipindi cha miaka mitano, na ikiwezekana muda mrefu zaidi (angalia Sanduku 5.2, shuhuda zilizotolewa). Ukweli kwamba vikundi vya RIPAT kwa kawaida huendelea kufanya kazi kwa pamoja hata baada ya kukamilisha mradi (baada ya miaka mitatu) linaonesha zaidi haja ya kukodisha mashamba la kikundi la migomba kwa muda mrefu.

Katika RIPAT, mashamba yanayotumika kwa majaribio ya kilimo hifadhi, uvunaji wa maji ya mvua na upanuzi wa wigo wa mazao pia zimekuwa zinaoneshwa katika mashamba kwa 'wastani' au 'kawaida' katika eneo hilo. Kilimo cha mahindi, mikunde na mazao ya mizizi yana gharama ndogo ukihusisha hali ya udongo na maji kuliko kilimo cha migomba, na mashamba ya kikundi mengi katika kijiji yanakuwa ni sahihi kwa malengo hayo. Mikataba ya mashamba haya hayahitaji kuwa ya muda mrefu kuliko muda wa mradi (miaka mitatu).

Wakati ukichagua kipande cha ardhi kwa ajili ya shamba la kikundi la kikundi, kikundi kinapaswa kuamua kama watalitumia:

- ardhi ya serikali jumuiya, pamoja na ardhi ya taasisi ambayo haitumiki (kama shule), au
- ardhi ya mtu binafsi (ambayo ni mali ya mwanakikundi).

Njia bora lazima kuangalia kwa makini katika kila jambo, kwa vile hakuna mapendekezo ambayo yamewekwa ili kufuata viwango fulani. Kitu cha muhimu sana ni kuhakikisha kwamba shamba lililotolewa lina mazingira yanayofaa kwa zao husika, hasa migomba na mazao mengine pamoja na udongo na maji yanaotakiwa, na kwamba wajumbe wa kikundi kuelewa zaidi thamani ya shamba la migomba wakati wa kurudisha kwa mmiliki wa ardhi. Katika vijiji ambavyo serikali ina ardhi nzuri ya kutumia, SLM linaweza kushawishi serikali ya kijiji kutoa sehemu ya ardhi nzuri kwa kikundi kwa kufanya kama sharti la kusaidia mradi. Lakini kumbuka mwisho wa siku ni kikundi chenyewe kuamua njia bora ya kutumia kupata shamba la kikundi. Baadhi ya wanavikundi wana mitazamo yao kuhusu kutumia shamba la

kijiji;-na hawapaswi kulazimishwa kutumia mashamba ya serikali ya kijiji. Kazi ya mwezeshaji wa kikundi ni kusaidia maamuzi mazuri kutokana na hali halisi.

Uzoefu wa miradi ya RIPAT imeonesha kwamba chaguzi zote mbili zinaweza kufanya kazi vizuri (angalia mifano katika Sanduku 5.2), lakini mara nyingi vikundi wanapendelea kukodi mashamba ya kikundi yanayomilikiwa na watu binafsi. Sababu kubwa ni kwamba serikali ya kijiji mara nyingi haina ardhi nzuri inayofaa, na hata kama ardhi nzuri inayofaa ikiwepo, urasimu wa serikali za vijiji mara nyingine unaweza kuzuia au kuwa tatizo.

Ni muhimu sheria na masharti kwa ajili ya kukodisha mashamba ya kikundi iwe wazi kama ilivyoainishwa katika mkataba, kwa yeyote anayemiliki ardhi. Mwongozo wa mkataba umetolewa katika kiambatanisho cha 4A. Ni lazima SLM kuangalia-usahihi wa uchaguzi wa vikundi na kuhakikisha kwamba mkataba unaokubalika umesainiwa na viongozi wa kikundi na mmiliki wa ardhi. Pia mkataba lazima usainiwe na mamlaka ya serikali ya kijiji na SLM, na nakala inawekwa katika ofisi ya serikali ya kijiji.

## Sanduku 5.2 Simulizi zilizochaguliwa

Baadhi ya simulizi kuhusu mashamba ya kikundi kama ilivyoainishwa hapa chini, na kuelezea baadhi ya faida na hasara za chaguzi zote mbili

**Vikundi kutumia ardhi ya Jumuiya**

a) Natang'amwaki ni mojawapo ya kikundi katika kijiji cha Losikito (wilaya ya Arumeru). Kikundi kiliweza kupata ekali moja ya shamba zuri katika ofisi ya serikali ya kijiji kwa lengo la kujifunzia kwa sababu shamba lilikuwa halihitajiki kwa matumizi ya kijiji. Kikundi hakikuwahi kukutana na tatizo lolote na mimea ya migomba inaendelea vizuri. Shamba liko karibu na shule, na linafikika na linaweza kuonekana na mtu yeyote. Hata hivyo kikundi kinakabiliwa na hatari kama serikali ya kijiji inaweza kuhitaji shamba kwa malengo mengine na kutoa taarifa ya muda mfupi sana. Kama hili litatokea, kikundi kitalazimika kuachia/kutoa shamba.

b) Katika kijiji kimoja cha RIPAT kikundi kilipewa shamba la jumuia na serikali ya kijiji na wakasaini mkataba na mamlaka ya serikali ya kijiji. Mwanamke mmoja alidai kwamba shamba hilo alikuwa amepewa na serikali ya kijiji, na alifyeka migomba yote ya kikundi. Swala hilo lilikuwa nje ya uwezo wa serikali ya kijiji na wakaamua kulipeleka mahakamani; lakini kikundi na shirika lililokuwa linatekeleza (RECODA) waliamua kuacha wazo la kutumia mashamba ya serikali ya kijiji kwa sababu mahakama iliendelea kuahirisha siku ya kusikiliza kesi. SLM halikuweza kuendelea kupoteza muda wake, na kikundi kilipaswa kuanza kutafuta shamba la kikundi lingine jipya kwa ajili ya majaribio.

**Vikundi vinavyotumia mashamba yanayomilikiwa na watu binafsi**

a) Ayenda ni moja ya vikundi ya RIPAT katika kijiji cha Endamararieki (wilaya ya Karatu) Kikundi kilikuwa na shamba la migomba ambalo lilikuwa limekodishwa kutoka kwa mwanakikundi mmoja. Baada ya kuchunguza na kuthibitisha uwepo wa ardhi kwa ajili ya migomba, kikundi kilisaini mkataba na mwenye shamba kwa muda wa miaka mitano, ambaye ni mwanakikundi. Kikundi kilitumia shamba kujifunza namna ya kulima migomba na pia kujipatia vipandikizi vya kuotesha kwenye mashamba yao na watu wengine wanaohitaji miche ya migomba. Kwa vile kuanzisha shamba la migomba ni uwekezaji kamili, kikundi kilifanya majadiliano na mwenye shamba ili

kuongeza muda wa miaka miwili tena kwenye mkataba wa shamba la migomba (iii kufanya jumla miaka 7) kabla hawajamrudishia shamba lake. Kikundi kitakuwa kimetengeneza faida nzuri sana kwa muda huo kutokana na shamba la kikundi.

b) Jikomboe ni moja ya vikundi vya RIPAT katika kijiji cha Kwaugoro (wilaya ya Arumeru). Kikundi kilianzisha shamba la kikundi la migomba katika shamba la mwanakikundi mmoja na walisaini mkataba wa kutumia shamba kwa miaka mitano. Wakati wa muda wa mradi kikundi kilikuwa na uwezo wa kuuza ndizi na machipukizi na kutengeneza faida nzuri. Kutokana na faida kikundi kiliweza kununua shamba eka moja kutoka katika kijiji chao ambapo walianzisha shamba la kikundi lingine, shamba hili si kwa madhumuni ya kujifunza tena ila ni kwa ajili ya biashara.

**Hatua katika kutambua na kuchagua shamba la kikundi**

- Hakikisha kikundi kinaelewa mambo muhimu ya kuzingatia (kama ilivyotajwa hapo juu), hasa mahitaji ya mazingira ya kilimo ya mazao yaliyochaguliwa.
- Jadili pamoja na kikundi faida na hasara za njia hizi mbili: i) Kukodisha shamba kutoka kwa mkulima binafsi katika kijiji (ikiwezekana mwanachama wa kikundi), au ii) kupata shamba kutoka kwa ardhi ya jumuiya uwezekano mkubwa ardhi ambayo ni mali ya taasisi na haitumiki (mfano shule).
- Kama njia zote zimekubalika unaweza kugawanya kikundi katika makundi madogo matatu kila kundi liwe na watu angalau 10. Kila kundi dogo linapewa kazi ya kutafuta shamba la kikundi zuri ndani ya kijiji kabla ya kikao kijacho:
    * Kama shamba la jumuiya/taasisi ndiyo njia nzuri, na serikali ya kijiji tayari imeahidi SLM kutoa shamba kwa mradi, mbinu hii ni lazima viongozi wa kijiji kwa pamoja na viongozi wa kikundi waliochaguliwa kujadili njia sahihi inayoweza kufanyika. Kundi la kwanza lazima litafute ardhi ya jumuiya wakisaidiana na viongozi wa kijiji.
    * Kikundi cha pili wanaweza kutafuta shamba linalomilikiwa na wanachama wa kikundi.
    * Na kikundi cha tatu wanaweza kutafuta shamba linalomilikiwa na wakulima binafsi katika kijiji.
- Mkutano ujao wa kikundi, mashamba yaliyopatikana yakaguliwe na kikundi kizima pamoja na msaada wa mwezeshaji, na kufaa kwa ardhi ni kujadiliwa kwa kila hatua.
- Mara tu kikundi kitakapofanya uchaguzi, viongozi wa kikundi huandaa mkataba wa kukodisha shamba (chini ya uongozi wako). Mkataba lazima ukubalike na kikundi. Mwezeshaji na msimamizi wa mradi lazima kuangalia usahihi wa uchaguzi huo na kuhakikisha mkataba umekubalika na kusainiwa na viongozi wa kikundi na mwenye shamba. Fomu za mikataba zimetolewa katika kiambatanisho 4A. Pia mkataba unasainiwa na uongozi wa kijiji na SLM, na nakala inaachwa katika ofisi ya serikali ya kijiji. Kikundi kitalipa gharama za kukodisha shamba sawasawa na bei ya soko la nje kutokana na fedha za kikundi.

Mara kikundi kitakapoanza kutekeleza teknolojia zilizoko kwenye kapu la uchaguzi katika shamba la kikundi ni muda wa kuweka vibao vinavyoonesha mradi wa RIPAT katikati ya kijiji. Vibao havitakiwi kuwekwa hadi kikundi kimekuwa imara na kimeanza shughuli za kilimo. Maneno yaliyoko kwenye kibao ni kama yafuatayo:







## Hatua ya 8: Kufanya tafiti linganishi - sambamba na shughuli zingine kwa muda wote wa mradi

*Uzoefu*

Baada ya kupata mashamba ya kikundi mazuri shughuli za kilimo zinaweza kuanza. Kumbuka shamba la kikundi lenye ukubwa wa eka moja linatumika kwa madhumuni tofauti (Angalia kielelezo). Kama ilivyotangulia kutajwa hapo, vikundi vya RIPAT mara kwa mara vinakuwa na mashamba la kikundi mawili: Moja linatumika kwa migomba, na lingine kwa kilimo hifadhi na mazao ya msimu/muda mfupi. Mashamba ya mazao ya muda mfupi yanaweza kutumika kwa maonyesho rahisi na kwa ajili ya kuzalishia mbegu au vipando (mazao jamii ya mikunde vipande vya mihogo na viazi vitamu), bila mfumo unaoeleweka wa majaribio ya kulinganisha. Sehemu nyingine inaweza kutengwa kwa ajili ya mazoezi ya kufanya kilimo kipya cha jembe jembamba la Zambia liitwalo “chaka” au au jembe la kukokotwa na wanyama la ripa. Lakini sehemu ya shamba inatengwa kwa majaribio zaidi ya kulinganisha teknolojia zilizochaguliwa au mazao kwa mfumo unaoeleweka.

Eneo lote la shamba la kikundi, ukijumuisha na sehemu za majaribio ni kwa ajili ya kujifunza kwa kujaribu teknolojia mpya kwa vitendo (vifaa na mazao); kulinganisha njia zilizochaguliwa na teknolojia; na kuona matokeo ya utafiti wa majaribio.

Matumizi ya mashamba ya majaribio yenye mpangilio mzuri yanaweza kuwa elekezi sana na mazuri kwa kujifunzia kama yatafanywa kwa uangalifu mkubwa! Kama shamba la majaribio halikupangwa vizuri na kutunzwa/ hamtajifunza chochote - au kuishia pabaya/ linaweza kuwapoteza. Kuna baadhi ya vitu utataka kuwa halisia kuhusu shamba kama unataka shamba liwe /mwalimu' mzuri. Kumbuka kuwa kazi zote zinazotakiwa kufanywa kwenye shamba la majaribio zinafanywa na wakulima wenyewe na sio na mwezeshaji. Lakini ni lazima kuwaongoza kwa karibu sana katika mchakato mzima.

Kama wakulima wataona faida kutokana na teknolojia/ wataiga teknolojia/njia hiyo/ na wengine kwenye jamii watawafuata. Kama teknolojia mpya imetekelezwa vibaya na kutoa majibu mabaya/ ujumbe utakaopelekwa ni kuwa teknolojia mpya haifai kutumika; hata kama igefanikiwa vizuri kama ingetekelezwa vizuri. Hii itatokea kama/ kwa mfano/ kikundi kimepata shamba zuri la kikundi, yamkini wakaanzisha shamba kubwa la migomba katika eneo lote na pana upepo mkali na hakuna uwezekano wa umwagiliaji au kuvuna maji ya mvua. Inaweza kutokea pia kama hamkuwa makini na muda/ kwa mfano kuotesha au kuweka mbolea kwa kuchelewa sana. Ni lazima kuhakikisha kwamba pembejeo (mbegu/ michelvifaa/ mbolea na madawa mengine yanayofanana na hayo) vinapatikana kwa muda muafaka. Unawajibika kuhakikisha kwamba shamba la maonyesho linakuwa sehemu nzuri ya kujifunzia.

Kama ilivyokwisha tajwa/ udongo/ maji na hali ya hewa vinaweza kutofautiana sana kwa umbali kidogo. Hivyo/ huwezi kuwaza kwamba 'teknolojia moja inafaa kwa maeneo yote' na teknolojia iliyofanya kazi sehemu moja itafanya kazi sehemu zote. Njia na teknolojia zilizoonyeshwa lazima kuruhusu wakulima kutambua/ kukumbuka na kusogeza karibu na mazingira yao. Mbinu na teknolojia zilizotumika mahali pale ziwasaidie wakulima kugundua/ kutafakari na kubadili mbinu na teknolojia hizo zilingane na hali halisi ya mazingira yao kwa lengo la kupunguza uwezekano wa kutofanikiwa.



Sharnba la kikundi lina rnaturnizi rnbalirnbali . Kwa rnfano, sehernu rnoja inaweza kuturnika kujaribu kilirno bora cha rnigornba,na sehernu nyingine rnazoezi ya kilirno hifadhi na sehernu nyingine kwa ajili ya rnajaribio ya kulinganisha na sehernu nyingi kwa ajili ya kuzalishia rnbegu bora za kuotesha (rnfano rnbaazi, rnihogo, ngwara, viazi vitarnu).

Kimsingi mafunzo ya kikundi yawawezeshe wakulima kupata taaluma muhimu ya kuendelea kufanya majaribio madogo katika mashamba yao.

*Kuanzisha no kutunza shamba Ia majaribio*

Upimaji halisi wa eneo la majaribio inategemea moja kwa moja teknolojia maalum inayojaribiwa na kuonyeshwa. Wakulima lazima wajifunze kutambua mambo yanayoathiri uzalishaji. Lakini idadi muhimu inayovutia mazoezi ya shughuli zote za kilimo ambazo zimekusudiwa katika mradi wa RIPAT kwa kawaida ni kubwa zaidi ya idadi ambayo inasimamiwa na majaribio ya kikundi (angalia Sanduku 5.3). Kwa hiyo unatakiwa kuelezea vitu ambavyo vinafaa na kupatikana kwenye kapu la uchaguzi, na kujadili na kukubaliana na wakulima ni vitu gani vya kujifunza na kulinganisha katika majaribio. Kwa mfano, katika vikundi vingi vya RIPAT mahindi yanachanganywa na mazao jamii ya mikunde (mfano: mbaazi, ngwara na kunde) kwa makusudi ya kulinganisha maandalizi ya shamba na kutunza maji (mfano: ripa na jembe la Mzambia), kwa kutumia mbinu za kawaida ya mkulima kama kigezo (angalia Kielelezo 5.1).

*Hali yo udongo unaofanana*

Matumizi ya majaribio yaliyorudufishwa yanaboresha kiwango cha kuaminika cha matokeo. Huwezi kupata matokeo yanayofanana kutoka kwenye sehemu zote mbili zilizokuwa zinapata matunzo sawa. Sehemu hizo kamwe haziwezi kufanana kwa 100%, na ambazo zinaongozwa na tofauti za kihistoria. Usuli wa sababu ya msingi ya tofauti kati ya sehemu na sehemu ni rutuba ya udogo au kutunza unyevu na maudhui ya juu ya eneo la majaribio. Kwa hiyo eneo la kikundi la majaribio ambalo limetengwa kwa lengo la mashamba ya majaribio ya kulinganisha lazima lifanane kwa viwango vinavyokaribiana kadiri iwezekanavyo.

Tofauti za rutuba ya udongo au kuhifadhi unyevu kwa kweli ni rahisi kugundua wakati wa msimu wa kupanda mazao/nafaka, mfano: mahindi. Tofauti katika rutuba ya udongo inaonekana waziwazi wakati wa ukuaji (mfano: urefu, rangi) wa hila zao. Lakini tangu mradi wa RIPAT ulianza rasmi wakati wa msimu wa ukame (wakati wa kuvuna mazao na kuacha shamba tupu), kutakuwa na kutegemea kwa kiasi kikubwa taarifa kutoka kwa mwenye shamba. Muulize kuhusiana na hali ya shamba na kuonesha maeneo yenye rutuba na yasiyo na rutuba, na maeneo ambayo mazao mara zote ni mazuri. Pia jaribu kupata taarifa za kihistoria za mazao katika shamba ikiwa ni pamoja na matumizi ya mbolea na mbolea za madini. Eneo litakalokuwa na hali nzuri zaidi lazima litengwe kwa ajili ya shamba la kikundi la majaribio.

*Ukubwawa eneo*

Kwa uzoefu inajumuisha mimea mikubwa kama vile mahindi na mihogo, eneo la mavuno lazima sio chini ya mita za mraba 40. Lakini kwa mazao kama vile mpunga, ngano, kunde na kadhalika eneo la mavuno linaweza kuwa dogo.

*Vitu vingine vyote kuwa sawa*

Bila kujali teknolojia zilizojaribiwa katika mashamba ya vikundi, ni muhimu kufanya kazi ya uhakika. Ili kuwezesha ulinganifu kufanywa na uelewa sahihi wa madhara ya matunzo sawa kupatikana, kila kitu kinachotegemewa kwa ajili ya matunzo lazima iwe kwa pamoja. Hivyo, kama njia ya maandalizi ya ardhini sababu ya kulinganishwa katika majaribio.




Kielelezo 5.1 Mfano wa shamba la majaribio lililopimwa-kulinganisha njia mbali mbali za maandalizi ya shamba kwa mfumo unaoeleweka

(kama kwenye mfano hapo juu), mambo mengine yote lazima kubakia sawa. Sehemu zote lazima zipandwe siku moja, kwa kina sawa cha mmea, kwa aina moja ya mbegu, na kwa msongamano sawa. Sehemu zote lazima kupata kiasi cha mbolea au madini ya mbolea kwa kiasi kinachofanana na lazima kupalilia kwa siku moja na kadhalika. Kama hutahakikisha kwamba hali na shughuli zote zinafanana- isipokuwa tu kwa utendaji uliokusudiwa - hautaweza kulinganisha matokeo ya majaribio ya sehemu mbalimbali. Kisha jaribio halitakufundisha chochote - au kibaya linaweza kukufundisha kitu ambacho ni makosa kabisa!

Unaweza pia kuanzisha mashamba ya majaribio ambapo unaweza kuchanganya njia bora mbalimbali katika eneo moja, na kulinganisha sehemu hizi na kawaida ya mkulima katika eneo lingine. Hata hivyo, hasara ni kwamba wakulima hawawezi kutofautisha sababu zilizochangia kwa ujumla kuboresha matokeo. Wakulima wanaweza kushangaa na kukataa sababu za kilimo bora cha mahindi kufanya vizuri kuliko kilimo cha kienyeji cha mahindi. Ni kwa sababu ya mbegu bora ya mahindi? Njia ya kulima kwa kuchimbua au samadi au kuweka mbolea? Lakini kwa ajili ya kuonesha uwezo na nyongeza ya manufaa ya kutumia mbinu bora za kilimo, ni vema kuwepo na shamba ambalo litatumika kama kilinganisho cha majaribio (Angalia Mchoro 5.2).




Kielelezo 5.2 Kulinganisha teknolojia bora na kilimo cha kawaida

**Sanduku 5.3 Vitu halisi vya kulinganisha katika agronomia ya kilimo**

Viko vitu vingi vya kiagronomia vinavyovutia kulinganisha majaribio rahisi ya kilimo. Si rahisi kuyafumbua yote katika mradi halisi wa RIPAT. Yafuatayo yametolewa kama kutia msukumo kwa kilimo cha mahindi:

- Maandalizi ya shamba (mfano, ripa, jembe la mzambia)
- Vipando bora vya kuotesha (aina mbali mbali), kiasi cha mbegu kinachostahili, nafasi
- Magugu na kuthibiti wadudu (mfano: matandazo, zao linalofunika ardhi, dawa ya kuua wadudu)
- Teknolojia ya kutunza maji na udongo (mfano, kutengeneza makinga maji mazao yanayofunika ardhi, matandazo, matuta ya kufunga na kukusanya maji ya mvua yanayotiririka)
- Kurejesha rutuba ya udongo
  * mbolea zinazotokana na viumbe hai (mfano, ng'ombe, mbuzi, au mbolea ya kuku, mboji, mabaki ya mazao, mbolea ya kijani)
  * Kuzungusha mazao (nafaka/mikunde, nafaka /mazao ya miZIZI, kuchanganya mazao)
  * Mazao jamii ya mikunde kama mafunika ardhi

Kwa ajili ya kilimo bora cha migomba

- Mashimo ya kuotesha- nafasi na ukubwa
- Kiasi cha mbolea inayopaswa kuwekwa
- Aina ya migomba
- Kufunika udongo muda wote (matandazo, mazao yanayofunika ardhi).
- Umwagiliaji
- Njia za kuvuna maji ya mvua (ukusanyaji wa maji ya mvua yanayotiririka kwenye mikondo ya maji; uchujaji wa maji, utengenezaji wa makinga maji shambani)

*Kujifunzo kutokono no mojoribio no kulingonisho motokeo yo mojoribio hoyo*

Kwa kipindi chote cha ukuaji, mashamba ya majaribio yanafuatiliwa kwa karibu na wakulima wanachambua chini ya mwongozo wa mwezeshaji. Wakulima hupenda kulaumu uzalishaji mdogo kutokana na vitu ambavyo viko nje ya uwezo wao kuzuia, kama vile ukame na mafuriko. Lakini kwa kupitia mashamba ya majaribio wanaona, wakulima huelewa na kujifunza kuhusu vitu ambavyo viko ndani ya uwezo wao kuvizuia-vitu vinavyoweza kuboresha uzalishaji.

Mifano ya vitu unavyoweza kujifunza kwenye mashamba la kikundi/majaribio:

- Kiwango cha uotaji na maendeleo ya mmea kwa ujumla
- Rangi, urefu wa mmea, upungufu wa virutubisho
- Kushambuliwa na wadudu na kuathiriwa na majani
- Upungufu wa maji
- Maji kutiririka wakati wa mvua/kupenya

- Uzalishaji-mavuno ya mazao. lakini pia wingina kiwango cha mabaki ya mazao na bidhaa zitokanazo na mazao hayo
- Mahitaji ya nguvu kazi

Matokeo hayo yananakiliwa na wakulima wenyewe wakati wa mikutano ya kikundi mara nyingi kadri inavyohitajika. Wakati mwingine ni vizuri kugawanya kikundi katika makundi madogo kwa ajili ya kukusanya taarifa. Lazima kuwasaidia wakulima iii kuweza kujifunza kutafsiri uchunguzi iii kufanya maamuzi sahihi. Uangalifu unahitajika iii kuhakikisha kwamba matokeo ya majaribio hayaharibiwi na msongamano ndani ya visehemu. Wakati wa mwisho wa majaribio, lazima kuwezesha mjadala wa jumla juu ya faida na hasara ya teknolojia mbalimbali zilizojaribiwa. Njia mojawapo ni kuoanisha na kikundi kitaamua juu ya njia nzuri.

### *Kuzalisha mbegu kwa wingi kwa ajili ya kuotesha*

Pamoja na kutumia mashamba ya vikundi kama kituo cha kujifunzia. mashamba hayo pia yanatumika kuzalisha mbegu za wanakikundi na wakulima wengine kijijini waliovutiwa. Mbegu kama hizo zinaweza kujumuisha mbegu za migomba, mbegu jamii ya mikunge, vipando vya viazi vitamu na mihogo n.k. Baadhi ya teknolojia ambazo zimetambulishwa vijijini ni mpya. na kwa hiyo mbegu na vipando haviwezi kupatikana kwenye maeneo yao. Kwa kuzalisha mbegu kwenye mashamba ya vikundi inarahisisha upatikanaji wa vipando na mbegu kwenye maeneo yao. Pia wakulima wanajifunza jinsi ya kuchagua mbegu/vipando vizuri na jinsi ya kuvitunza. Kuuza vipando au machipukizi kwa wanakijiji wengine ni chanzo cha kujipatia kipato katika kikundi. Lakini hili linaweza kufanyika tu baada ya wanakikundi wote kuchukua kiasi wanachotaka.



## Hatua ya 9: Kuunda kamati ndogo na kuchagua wakulima vichocheo

### *Uundaji wa kamati ndogo*

Uundaji wa kamati ndogo ni sehemu muhimu ya mafunzo ya RIPAT. Kwa sababu vikundi vya RIPAT ni vikubwa kwa uhalisia (wanachama 30-35) na miradi inahusisha teknolojia kadhaa, ni vizuri kutenga baadhi ya majukumu kwa kamati ndogo kama inavyoelezewa hapa chini.

Mara kikundi kinapopata shamba la kutosha la kikundi, wanakikundi wanakuwa tayari kwa kufundishwa teknolojia maalum. Katika Sanduku 5.4 tumetoa orodha ya mada ambazo lazima zifundishwe kwa kila zao linalotambulishwa, na Kiambatanisho 3 tumetoa orodha ya baadhi ya miongozo ya kitaalamu kwa ajili ya kufanya kwa vitendo utekelezaji wa teknolojia mbali mbali za mazao/mifugo. Mafunzo mengi ni kwa vitendo, yaani kujifunza kwa kufanya. Lakini kabla ya uanzishaji halisi, kwa mfano, shamba la kikundi la migomba, ni lazima uwafundishe wanakikundi nadharia ya historia muhimu ili waweze kuelewa kanuni zilizopo za zao au teknolojia.

Baada ya vipindi vya mafunzo ya mwanzo, kamati ndogo zinaundwa, kila moja ikiwa na wakulima wanne au watano wenye kupenda/kuvutiwa na teknolojia fulani (tazama Sanduku 5.6). Wanafanya kazi kama watu wa kusaidia kikundi, huku wakiwa na majukumu maalum kuzingatia kazi ya vitendo kwa zao au aina ya mifugo. Pia wana kazi maalum ya kufuatilia uchukuaji na ufanyaji wa teknolojia miongoni mwa kikundi. Baadhi ya kamati ndogo zimeelezwa hapa chini. Kuunda kamati ndogo kunaokoa muda na ni njia ya kugawa majukumu, kwa sababu siyo wanakikundi wote wanahitajiwa kushirikishwa katika shughuli zote.

Kamati moja ndogo inaundwa kwa ajili ya kila teknolojia kuu inayochukuliwa katika kikundi, kwa mfano migomba, kilimo hifadhi na mifugo. Kwa vile kwa kawaida wanakikundi wanakikundi wanafahamiana, wanaweza kuchaguana wao wenyewe kwa ajili ya watu wa teknolojia. Hata hivyo, ni vizuri kufuata uchaguzi wao wa wajumbe wa kamati ndogo. Kila kamati ndogo inachagua kiongozi atakayetoa taarifa kwa mwenyekiti wa kikundi.

Wajumbe wa kamati ndogo wana wajibu wa kufuatilia teknolojia kwenye shamba la kikundi (ambapo inafaa), na wanatembelea wanakikundi mara kwa mara na kuweka kumbukumbu za uigaji/uchukuaji – kwa mfano, ni miche mingapi ya migomba imepandwa, au ni watoto wangapi wamezaliwa kutokana na aina mpya ya mifugo.Wanatoa taarifa kwa kikundi kwenye kikao kinachofuata. Taarifa hizi ni muhimu, kwa sababu zinaweka msingi kwa ajili ya kuangalia na ufuatiliaji wa maendeleo ya mradi kwa jumla (angalia sehemu ya 3).

Majukumu maalum kwa kamati ndogo ndogo binafsi yameelezwa hapa chini. Kumbuka daima kwamba wako chini ya usimamizi wako wakati wanafanya kazi hizo.

Sanduku 5.4 Mazao

Vipengele hivi hapo chini vinatakiwa kufundishwa kwa kila zao linalotambulishwa katika mfululizo wa vipindi vya mafunzo. Mwezeshaji wa kikundi ana wajibu wa kuhakikisha kwamba mada zote husika zinafundishwa kwa wakati unaotakiwa.

- Kwa nini aina hili ya zao lililoboreshwa/jipya limechaguliwa katika kapu la uchaguzi
  * Faida/hasara, ikiwamo uchambuzi wa hatari, gharama za uzalishaji, uchambuzi wa faida, mahitaji ya nguvu kazi. Utumiaji wa rasilimali zilizopo
- Mnyororo wa mgawanyo (angalia chini)
- Kanuni za uzalishaji wa mazao
- Mazingira (joto, maji, udongo)
- Aina ya mazao
- Maandalizi ya shamba
- Uchaguzi wa mbegu/vipando
- Upandaji/uoteshaji
- Palizi
- Mbolea
- Mzunguko/uchanganyaji wa mazao
- Wadudu na magonjwa
- Uvunaji
- Utunzaji baada ya mavuno (uhifadhi, usindikaji, utumiaji) na kuhifadhi vipando/mbegu
- Masoko na mlolongo wa thamani

Masomo haya yanafundishwa katika mpangilio wa vipindi vya mafunzo kwa kikundi katika kipindi cha upandaji na ukuaji wa mazao. Kabla ya uanzishaji halisi wa shamba la kikundi, mada saba za kwanza (hadi 'uchaguzi wa mbegu') zifundishwe kwa nadharia.

**Mnyororo wa mgawanyo**

Katika RIPAT, kwa ujumla kuna kanuni katika 'mnyororo wa mgawanyo' – wakulima wote washiriki wanawajibika kwa ajili ya kufundisha wakulima wengine watatu katika jamii kwa vile walivyojifunza na kufanya wenyewe. 'Mnyororo wa mgawanyo' wa kupeana miche ya mimea mwanzoni imekuwa ikitumika kwa migomba (angalia Sanduku 4.2). Kila mkulima katika kikundi aliyechukua teknolojia ya kilimo cha migomba bora anatazamiwa kugawa mara tatu ya idadi ya miche ya migomba aliyopokea kupitia mradi. Agawe kwa wakulima wengine wanaopenda kulima migomba katika jamii na kuwafundisha teknolojia bora za kilimo cha migomba.

## Sanduku 5.5 Mifugo

Vipengele hivi hapa chini vinatakiwa kufundishwa katika kila teknolojia ya mifugo inayotambulishwa (kwa mfano aina bora za mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku) katika mfululizo wa vipindi vya mafunzo. Mwezashaji wa kikundi ana jukumu la kuhakikisha kwamba mada zote husika zinafundishwa kwa wakati.

- Kwa nini aina hii bora ya mfugo imechaguliwa kuwa katika kapu la uchaguzi
  * faida/hasara, ikijumuisha uchambuzi wa hasara, gharama za uzalishaji, uchambuzi wa faida, mahitaji ya kazi. Utumiaji wa rasilimali zilizopo
- Mnyororo wa mgawanyo (isipokuwa kuku), angalia chini
- Kanuni za uzalishaji
- Ulishaji
- Nyumba
- Aina na uzalishaji
- Udhibiti wa wadudu na magonjwa (ikijumuisha chanjo)
- Uzalishaji (kwa mfano nyama ikilinganishwa na maziwa, mayai yakilinganishwa na nyama na kadhalika)
- Uhifadhi, usindikaji, utumiaji
- Masoko na mlolongo wa thamani

Masomo haya yanafundishwa kwenye kikundi katika vipindi vya mafunzo kwa muda wa miaka mitatu. Kabla ya kutoa wazazi bora wa mifugo kwa kikundi, vipengele vitano vya msingi (hadi 'nyumba' hapo juu) vifundishwe kwa nadharia.

**Mnyororo wa mgawanyo (mfano mbuzi bora wa maziwa, kondoo, nguruwe)**

Kila kikundi kinapewa majike watano na madume wawili halisi wa kisasa kama kianzio cha uzazi. Kikundi kinaamua miongoni mwao akina nani watapokea hao mifugo wazazi wa kuanzia. Kikundi kinaandaa orodha ya mfululizo ya wanakikundi watakaopokea watoto – mnyororo wa mgawanyo. Kwa upande wa mbuzi na kondoo, watoto wawili wa kwanza wa kike watakaozaliwa wagawanywe kwa wanakikundi wengine kwa kuzingatia orodha iliyotengenezwa. Baada ya yule mwenye mnyama mzazi kutoa watoto majike wawili kwa wanakikundi wengine ni kwamba lile jike mzazi linabaki kuwa mali yake.

Ili kuwa na vigezo vya kupokea mnyama mzazi wa mwanzo au mtoto atakayezaliwa, mwanakikundi lazima kwanza athibitishe nia na utayari wake, yaani lazima amalize kujenga banda la kutosha, ameweka mfumo mzuri wa ulishaji, ameotesha majani, na kadhalika. Kamati ndogo itasimamia jambo hili kwa umakini (angalia Sanduku 5.6 chini).

Kwa upande wa nguruwe, majike halisi watano na madume wawili halisi watatolewa kwa kila kikundi kama kizazi anzilishi. Lakini kwa sababu ya nguruwe kuzaa watoto wengi kwa uzao mmoja ukilinganisha na mbuzi na kondoo, kila mkulima anahitajika kutoa watoto majike watano wa kwanza kwa mkulima anayefuata aliyepo kwenye orodha.

Mkataba maalum wa 'mnyororo wa mgawanyo' kuhusu makubaliano haya unasainiwa kati ya kikundi na SLM. Kuna kielezo katika kiambatanisho cha 4B.

### Sanduku 5.6 Mfano wa kamati ndogo ndogo na majukumu yake

Kamati ya migomba inachukua nafasi katika kuongoza:

- ukulima wa zao la migomba la kikundi na shamba lolote la majaribio la migomba lililoanzishwa
- kuhakikisha vifaa vya kikundi kwa ajili ya migomba viko sehemu sahihi na katika hali nzuri
- kuvuna na kuuza mikungu ya ndizi na miche ya migomba kutoka kwenye shamba la kikundi
- kuwasaidia wakulima wengine katika kijiji kuanzisha shamba la migomba (ingawa mwanakikundi mwingine yeyote anayeweza kuelimisha katika hilo)
- kufuatilia kwa kutembelea wanakikundi:
  * kukusanya taarifa ya wakulima binafsi (idadi ya mashimo, mashina yaliyopandwa na changamoto)
  * kuwakumbusha wanakikundi kuhusu makubaliano ya 'ulipaji' kwa ajili ya pembejeo – yaani ugawaji wa miche kwa wakulima wengine katika kijiji (angalia Sanduku 4.2)

Kamati ya kilimo hifadhi inachukua nafasi katika kuongoza:

- kutunza shamba la kilimo hifadhi na shamba lolote la majaribio la kilimo hifadhi
- kuhakikisha vifaa vyote vya kikundi viko mahali sahihi na katika hali nzuri (yaani ripa, majembe ya Kizambia liitwalo chaka, bomba la kupulizia na kadhalika)
- usambazaji wa vipando (mbegu/vijiti) kwa wanakikundi wengine,
- kuuza ziada iliyozalishwa kutoka shamba la kikundi la kilimo hifadhi
- kufuatilia kwa kutembelea wanakikundi wengine:
  * kukusanya taarifa kwa wakulima binafsi walioiga (idadi ya wakulima wanaofanya kilimo hifadhi, mafanikio na changamoto)
  * kuwakumbusha wanakikundi kuhusu makubaliano ya ‘ulipaji’ wa pembejeo (angalia Sanduku 4.2)

Kamati ya mifugo inachukua nafasi kuongoza katika:

- kuandaa mnyororo wa mgawanyo (kuweka orodha ya ugawaji wa mbuzi jike wanaozaliwa)
- kuangalia kwa makini kuwa mtu anayefuata katika orodha kwamba anakidhi vigezo kabla ya kupokea mbuzi jike wanaozaliwa (amejenga banda la kutosha, ameanzisha mfumo wa ulishaji, malisho yamepandwa na kadhalika)
- kufuatilia kwa kutembelea wanakikundi wengine:
  * kukusanya taarifa juu ya idadi na jinsi ya watoto wa mifugo wanaozaliwa: idadi ya watoto wa mifugo waliogawanywa kupitia mnyororo wa mgawanyo: uigaji wa teknolojia (nyumba, ulishaji, na changamoto)
- kufuatilia mlipuko wa magonjwa na wadudu (pia kutoa taarifa kwa afisa ugani kuhusu huo mlipuko)
- kuratibu mpango wa uzalishaji (kubadilishana madume ili kuepuka ukoo mmoja kuzaliana)

- kukumbusha wanakikundi kuhusu makubaliano ya ‘ulipaji’, kwa mfano majogoo (angalia Sanduku 4.2)

Kamati ndogo ya mifugo mara zote inakuwa na wanakamati watano wanaopewa majike wazazi wa kwanza na madume wazazi).

### *Kuchagua wakulima vichocheo*

Wakulima vichocheo watu ambao, wakati wa kipindi cha utekelezaji, wametambuliwa kama watu walioendelea kama wajasiriamali jamii na wakala wa mabadiliko. Ni wakulima waliofanikiwa kutoka katika vikundi ambao wameshika ujuzi uliotolewa kupitia mafunzo ya RIPAT na wametekeleza kwa mafanikio angalau teknolojia moja iliyowezeshwa na RIPAT.

Wakulima vichocheo wanatakiwa kuwa na uwezo wa kupeleka ujuzi wa teknolojia maalum kwa wakulima wengine. Kazi kubwa ya wakulima vichocheo ni kusaidia kueneza ujuzi uliopatikana kutoka kwenye mradi kwenda kwa wakulima wengine na baadaye kwa vikundi vingine ndani ya kijiji alichopo au kwa vikundi na/au wakulima katika vijiji vingine.

Aina mbili ya wakulima wataalamu:

- Wakulima vichocheo wa teknolojia – mkulima mmoja kwa teknolojia kwa kikundi (mfano migomba, kilimo hifadhi, mifugo)
- Wakulima vichocheo enezi (WV)– watu wawili kwa kikundi

### *Wakulima vichocheo wa teknolojia*

Hawa wanachaguliwa miongoni mwa wanakikundi mara wanapothibitishwa kuwa wakulima wanaofanya vizuri ambao wanachukua hatua kuleta mabadiliko katika teknolojia fulani. Wanatakiwa pia kuwa na uwezo wa kuwafundisha wakulima wengine, na wawe wanaheshimika. Kila kikundi kinachagua mtu mmoja kwa kila teknolojia. Mara zote huchaguliwa kutoka kwenye wanakamati wa kamati ndogo – lakini kikundi kinaweza kuchagua yeyote wanayejisikia atakuwa bora zaidi kwa kazi. Baada ya uchaguzi, wakulima vichocheo wa teknolojia kutoka vikundi 16 kwenye mradi wa RIPAT wanapelekwa kwenye mafunzo ya siku 3 hadi 5 ambapo wanapata elimu kwa undani ya nadharia na vitendo katika teknolojia husika, pia mafunzo ya uwezeshaji wa jinsi ya kuwafundisha wengine. Kila mkulima kichocheo atashughulika kama mtu wa kufundisha wataalamu wengine na kuwa na kazi ya kutoa msaada wa kitaalamu kwa wanakikundi wengine na kijiji/jamii nzima. Kawaida maafisa ugani wanashiriki katika mafunzo haya kwa kina.

### *Wakulima vichocheo enezi (WV)*

Wakulima vichocheo enezi wanachaguliwa wakati mradi umefika nusu ya utekelezaji wake. Kazi ni kueneza ujuzi walioupata kwa wakulima wengine ndani na nje ya vijiji vyao. Wanatakiwa kuwa wametekeleza angalau teknolojia moja katika zilizotekelezwa na awe na uwezo wa kuwezesha, kushawishi/kuhamasisha, na kufundisha wakulima wengine. Mara nyingi huchaguliwa kutoka miongoni mwa wakulima vichocheo wa teknolojia, lakini kikundi kiko huru kuchagua mwanakikundi yeyote. Baada ya kuchaguliwa, hawa wakulima vichocheo enezi wanaenda kwenye mafunzo kwa undani kwa mfano kwenye “akademia”

ya RECODA pamoja na maafisa ugani. Kisha wanatarajiwa kuanzisha vikundi vipya katika vijiji vya jirani kwa kusaidiwa na mamlaka ya wilaya.

Vigezo katika kuchagua wakulima vichocheo enezi

- Ni mwanakikundi anayehudhuria mikutano yote ya kikundi na shughuli kulingana na sheria ndogo ndogo za kikundi
- Ana uelewa mzuri wa dhana yote ya RIPAT na amefanya kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo
- Ana ujuzi wa teknolojia alizozichukua na amezitekeleza vizuri
- Ana uwezo wa kufundisha na kuwafundisha wengine (kupeleka ujuzi/maarifa kwa wengine kwa njia inayoeleweka)
- Anaweza kusoma na kuandika
- Anaheshimika kwa wanakikundi na kijiji kwa ujumla, na ana msimamo mzuri katika jamii

Wanakikundi wanatakiwa kufanya uchaguzi huu wao wenyewe – lakini wakiwa chini ya usimamizi wa mwezeshaji wa kikundi. Kwa sababu wakulima vichocheo enezi ni muhimu sana kwa ajili ya mradi kuwa endelevu, na kwa kuwa mradi unawekeza rasilimali nyingi kwao katika kuwafundisha zaidi, ni muhimu kuthibitisha mara ya pili kuhusu sifa zao. Ni vizuri zaidi kikundi kutambua watu wanne bora katika kikundi. Uchaguzi wa mwisho kwa ajili ya kuwapata wawili bora miongoni mwa wale wanne unafanyika kama ifuatavyo:

- Kagua ufanisi wao kwa kuwatembelea katika mashamba yao na kukagua utekelezaji wa teknolojia walizochukua
- Endesha jaribio la nadharia la kuandika
- Fanya mahojiano binafsi (na mhusika)

Kutokana na matokeo, wewe na mwenyekiti wa kikundi mfanye uchaguzi wa mwisho.

## Hatua ya 10: Utunzaji wa kumbukumbu na usimamizi wa fedha – kazi inayoenda sambamba kwa kipindi chote cha mradi mzima

Wakati wote wa kipindi kizima cha mradi kikundi kinafundishwa katika maeneo mbali mbali ili kujenga nguvu kama kikundi. Tayari utakuwa ulishawafundisha misingi ya uongozi bora, na umewasaidia katika kuandaa katiba ya kikundi. Shughuli nyingine za mafunzo katika kujenga nguvu ya kikundi inajumuisha utunzaji wa kumbukumbu na usimamizi wa fedha. Kuna mada kadhaa zitakazofundishwa wakati wa mradi, ikijumuisha kufanya kilimo kama biashara, utunzaji wa kumbukumbu na mfumo wa kuweka na kukopa. Kwa undani unatakiwa kuangalia mwongozo mwingine.

### *Kilimo kama biashara*

Kwa ujumla makusudi ya mafunzo haya ni kuboresha uelewa wa wanakikundi jinsi ya kuongeza kupata faida, kuwasaidia kutoka kwenye kilimo cha kujikimu kwenda kilimo uchumi. Mafunzo yanalenga katika mada zifuatazo:

- Uchaguzi wa mazao au mradi
- Kufanya maamuzi katika kilimo

- Kupunguza gharama za uzalishaji
- Kuongeza utumiaji wa rasilimali zilizopo

Sehemu ya mafunzo yanahusiana na kapu la uchaguzi kwa kuwasaidia wakulima kulingana na teknolojia zilizopo na zile zilizoboreshwa kwa kuangalia ufanisi, mahitaji ya nguvu kazi na faida taslimu. Uchaguzi wa zao usiangalie utamaduni peke yake, bali uangalie zaidi kuongeza faida kifedha.

RIPAT pia inajaribu kupunguza hatari kwa wakulima kwa kuanzisha upanuzi wa wigo wa mazao, kwa mfano kuwatia moyo wanakikundi kupanda mazao yanayovumilia ukame kama mihogo, ngwara na mbaazi, na kwa kutumia mbinu za kuhifadhi maji. Kwa mkulima wa kujikimu anayezoea kupata njaa angalau kwa kipindi, teknolojia bora zaidi haiwezi kuwa inayoleta faida ya juu katika mwaka bora wa mvua nzuri, lakini ile inayozalisha mavuno yanayokubalika katika mwaka mbaya. Kuwasaidia wakulima wazingatie kupata faida ya juu iwezekanavyo na kupunguza hatari ni muhimu. Mkulima hahitaji tu kupata mapato ya kutosha kutoka kwenye mazao na mifugo kulipia gharama za chakula, mavazi, ada za shule, matibabu, na kadhalika, lakini pia kuwa makini kuminya athari.

Jedwali 5.4 linaonesha mfano wa kulinganisha uzalishaji wa mahindi na migomba (pamoja na mazao mengine) kwenye eka moja ya ardhi. Kwa mfano, mkulima anapata TZS 628,000 ikiwa ni faida zaidi kwa mwaka wa kwanza kama migomba ingepandwa kwenye eka moja badala ya mahindi, hata ingawa fedha nyingi zingewekezwa.

Katika miaka inayofuata, hakutakuwa na gharama ya kuchimba mashimo, kuchanganya mbolea, au kununua na kupanda miche, ingawa gharama nyingine kama kupunguza machipukizi, kupalilia na kupanda tena ngwara inaweza kujitokeza. Hii inamaanisha kwamba faida itakuwa kubwa zaidi katika miaka ya itakayofuata. Tena faida ya mkulima inakuwa kubwa zaidi kama kazi alifanya yeye mwenyewe kwa mikono yake. Kwa mfano huu, shamba la migomba linatoa fursa kwa mtu kujiajiri mwenyewe, kumruhusu mkulima kupata mshahara kwa kuwekeza kazi yake katika kuanzisha shamba la migomba. Mzigo mkubwa wa kazi ya uanzishaji inatokea wakati wa kipindi cha kiangazi, wakati kuna shughuli nyingine kidogo za kufanya shambani. Kama mkulima hatatumia vibarua kuchimba mashimo lakini akachimba mashimo wenyewe na kuchanganya mbolea kwa ajili ya migomba wakati wa majira ya kiangazi, wakati ambapo kazi za kilimo zimepungua.

**Jedwali 5.4** Ulinganisho kati ya mahindi na migomba kwenye eneo la eka moja kwa kuangalia gharama na mapato (TZS)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | *GHARAMA* | | | |
| *Mahindi* | | | *Migomba* | | |
| Kulima | | 30,000 | Kupima shamba | | 20,000 |
| Kupiga haro | | 30,000 | Kupiga mashimo | | 675,000 |
| Kupanda | | 30,000 | Kuchanganya mbolea | | 450,000 |
| Mbolea ya kwanza | | | Kupanda | | 100,000 |
| Mbolea ya pili | | | Miche | | 540,000 |
| Mbegu | | 120,000 | Ngwara | | 12,000 |
| Mbaazi | | 30,000 | Palizi ya kwanza | | 50,000 |
| Palizi ya kwanza | | 60,000 | Palizi ya pili | | 20,000 |
| Palizi ya pili | | 60,000 | Kutoa machipukizi | | 900,000 |
| Kuvuna | | 80,000 | | | |
| Usafiri na vitu vya kupakia | | 15,000 | | | |
| Jumla ya gharama kwa mwaka | | 455,000 | Jumla ya gharama mwaka wa kwanza | | 2,767,000 |
| | | *MAPATO* | | | |
| *Mahindi* | | | *Migomba* | | |
| Magunia ya mahindi yaliyovunwa | 20 | | Mikungu ya ndizi iliyovunwa | 450 | |
| Bei kwa gunia | 50,000 | | Bei kwa mkungu | 8,000 | |
| Jumla mapato -mahindi | | 1,000,000 | Jumla ya mapato ya ndizi | | 3,600,000 |
| Mbaazi - mavuno gunia | 4 | | Machipukizi yaliyovunwa | 900 | |
| Mbaazi bei kwa gunia | 80,000 | | Bei kwa chipukizi | 600 | |
| Jumla mapato ya mbaazi | | 320,000 | Mapato toka machipukizi | | 540,000 |
| | | | Ngwara zilivunwa gunia | 1 | |
| | | | Bei ya gunia la ngwara | 120,000 | |
| | | | Jumla ya mapato ya ngwara | | 120,000 |
| Jumla ya mauzo | | 1,320,000 | Jumla ya mauzo | | 4,260,000 |
| Toa gharama | | 455,000 | Toa gharama | | 2,767,000 |
| *Faida kwa jumla* | | *865,000* | *Faida kwa jumla* | | *1,493,000* |

Kama mkulima hatatumia vibarua kuchimba mashimo lakini akachimba mashimo mwenyewe na kuchanganya mbolea kwa ajili ya migomba wakati wa majira ya kiangazi, tofauti ya mapato kati ya mahindi na migomba itakuwa kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Jumla ya gharama za migomba kama ilivyo kwenye jedwali namba 5.4 ni | TZS 2,767,000 |
| Toa gharama ya kuchimba mashimo na kuchanganya mbolea | TZS 1,125,000 |
| *Jumla ya gharama mpya ni* | *TZS 1,642,000* |

Jumla ya faida kwa mkulima itakuwa (TZS 4,260,000 – 1,642,000) = TZS 2,618,000,
Ambayo ni 1,753,000 zaidi ya ile ya mahindi.

Mifano kama hiyo inaweza kuwafungua macho wakulima. Hata hivyo, haipendekezwi kwamba wakulima kuanzisha eka moja ya migomba kwa mara moja. Wanatakiwa kuonja na kujaribu kwanza, na kupanua kama wanaona mafanikio. Kazi yako ni kuwataarifu siyo tu juu ya uwezekano, lakini pia kuhusu uwezakano na matatizo yanayoweza kujitokeza.

Jedwali namba 5.5 linaonesha jinsi wakulima wanavyoweza kupanga uzalishaji wa mazao na gharama zinazohitajika wakati wa majira husika. Gharama zimeorodheshwa kulingana na mwezi ambao tukio linategemewa kutokea.

**Jedwali 5.5** Gharama za uzalishaji mahindi kwa eka moja

| *Gharama* | *Mwezi* | | | | | *Jumla TZS* |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | *1* | *2* | *3* | *4* | *5* | |
| Kulima | 30,000 | | | | | 30,000 |
| Kupiga haro | 30,000 | | | | | 30,000 |
| Kuotesha | | 30,000 | | | | 30,000 |
| Mbegu | | 120,000 | | | | 120,000 |
| Mbolea ya kwanza | | | | | | |
| Mbolea ya pili | | | | | | |
| Mbolea ya tatu | | | | | | |
| Palizi ya kwanza | | 60,000 | | | | 60,000 |
| Kupanda mbaazi | | 30,000 | | | | 30,000 |
| Palizi ya pili | | | 60,000 | | | 60,000 |
| Kiua magugu (1) | | | | | | |
| Kiua magugu (2) | | | | | | |
| Kuvuna | | | | 80,000 | | 80,000 |
| Mifuko ya kuwekea | | | | 5,000 | | 5,000 |
| Gharama za usafiri | | | | | 10,000 | 10,000 |
| *Jumla ya gharama* | *60,000* | *240,000* | *60,000* | *85,000* | *10,000* | *455,000* |

**Mpango wa uzalishaji**

Mapato yanayotarajiwa: = mazao yanayotarajiwa **mara** bei inayotarajiwa **toa** jumla ya gharama

**Uchambuzi wa uzalishaji**

Mapato halisi: = mavuno halisi **mara** bei halisi **toa** jumla ya gharama halisi

### *Utunzaji wa kumbukumbu na vitabu*

Utunzaji wa kumbukumbu utawasaidia wakulima kuwa na uelewa bora, kuchambua, na kulinganisha uzalishaji, kipato, gharama, na faida kutokana na shughuli zao za kilimo. Katika biashara yoyote, ikiwemo kilimo, ni muhimu kuweka mfumo wa ufuatiliaji wa shughuli zote, ikijumuisha uzalishaji, mapato kutokana na mauzo, na gharama zinazohusiana na uzalishaji. Bila hizo taarifa haiwezekani kutambua ni shughuli ipi inaleta kipato kizuri au chakula kingi, na kuchagua shughuli ambazo ni nzuri kwa ajili ya kuendeleza kaya. Taarifa rahisi zinaweza kuwasaidia wakulima kufanya maamuzi mazuri kuhusiana na shughuli wanazowekeza kwazo. Hata hivyo taarifa zinazokusanywa zinatakiwa ziwe rahisi iwezekanavyo ili wakulima wenye elimu ndogo waweze kuzielewa.

Wakati kikundi kinapoanza shughuli zake, ni muhimu kuanza kutunza kumbukumbu. Kumbukumbu ambazo kikundi kinatakiwa kutunza, na mafunzo yanayotakiwa kutolewa kwa kikundi ni kama ifuatavyo:

- Shughuli za kikundi kama maandalizi ya shamba (kupanda, kupalilia, kuvuna), masoko na mauzo ya mazao, na upatikanaji wa pembejeo

- Makubaliano na maamuzi, kama mikataba ya ardhi, mikataba na shirika linalotekeleza mradi juu ya kulipia pembejeo, mnyororo wa mgawanyo, na kadhalika.
- Mali kama vifaa, kama vimetolewa na mradi au vimepatikana kupitia uwekezaji ambao kikundi kimefanya
- Akaunti za vikundi, ikujumuisha mapato kutokana na ada/michango ya wanakikundi na mauzo, na gharama

Ni muhimu sana kwa kikundi kwamba wanakikundi wote kujua ni faida kiasi gani inayopatikana kutokana na shughuli zao, na hasara yoyote. Hii itaweka msingi katika kufanya maamuzi. Kwa vikundi vyovyote visivyofanya vizuri, kumbukumbu zitatoa taarifa ni wapi tatizo lilipo, inasaidia vikundi kuamua ni hatua zipi zinahitajika kuchukua.

Vikundi vitumie vitabu vifuatavyo kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za fedha:

- Hati ya malipo
- Stakabadhi ya pesa
- Kitabu cha mauzo na manunuzi ya kila siku

Kutokana na hivi vitabu, vikundi vitaweza kufahamu lini na jinsi ambavyo wametumia pesa zao. Vitabu pia vinawezesha vikundi kuandaa yafuatayo:

- Kitabu cha fedha taslimu, kinachotumika kuweka kumbukumbu ya fedha zote taslimu zilizolipwa na kutolewa na biashara
- Kitabu cha siku cha mauzo na manunuzi, kinachotumika kuweka kumbukumbu zote za mauzo kwa mkopo na manunuzi kwa mkopo
- Karatasi ya mizania, inayoandaliwa kutokana na kitabu cha taslimu na kitabu cha siku cha mauzo na manunuzi baada ya muda uliochaguliwa, ikiwezekana miezi sita

*Hatua za kufuata*

- Kuanza kwa mafunzo na shughuli kwa vitendo, miamala ya fedha inaanza.
- Mwanzo kabisa wa mradi, vikundi vinafundishwa kanuni za usimamizi wa fedha, ikijumuisha uelewa wa tarakimu kwenye hati ya malipo na stakabadhi ya pesa.
- Kutokana na hizi kumbukumbu, viongozi wa kikundi wanajaza kitabu cha taslimu kila mwisho wa mwezi, na kutengeneza karatasi ya mizania kila miezi mitatu.
- Taarifa rahisi ya mapato na matumizi iandaliwe na na kuwasilishwa kwa wanakikundi kila mwezi.

Viongozi wa kikundi (yaani wenyeviti, makatibu na hasa watunza hazina) wanatakiwa kupokea mafunzo ya ziada kutoka kwa SLM ili kwamba wawe na uwezo wa kuweka kumbukumbu kwa kuzingatia kanuni za utunzaji wa kumbukumbu. Wajibu wako utakuwa ni kusaidia waweka hazina wa vikundi na kutoa kozi fupi ya marudio kwa ajili ya vikundi inapoonekana ni muhimu.

Kwa nyongeza, makatibu wa vikundi wanapokea mafunzo maalum kutoka kwenye SLM. Mafunzo yatahusu wajibu wao, kuchukua kumbukumbu za vikao, kuweka kumbukumbu ya mahudhurio, kujaza fomu za mikataba, na kadhalika. Kama mwezeshaji utasaidia na kumshauri katibu wa kikundi wakati unapohitajika kufanya hivyo.

### *Mfumo wa kuweka na kukopa*

Ukosefu wa mtaji mara nyingi umewazuia wakulima kupanua na kuboresha biashara zao. Wakulima wanaweza kuwa na vitu vyote muhimu, kama vile ardhi na nguvu kazi, hata elimu/maarifa na mawazo mazuri. Hatahivyo, ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununua vitendea kazi na pembejeo unawazuia kutekeleza mipango yao. Wengi wa wakulima wa vijijini hawana uwezekano wa kuweka akiba benki. Mara zote benki ziko mbali nao, na masharti yanayotolewa hayako rafiki sana na wakulima wenye fedha kidogo za kuweka.

Hata hivyo kuna njia nyingine ambazo vikundi vinaweza kutumia kuweka na kukopa fedha kutoka kwenye ushirika wa kuweka na kukopa vijijini (UKKV/VSLA) imekuwa ikijumuishwa kwenye 'kapu la uchaguzi' katika miradi ya RIPAT, na imeonekana kuwa maarufu miongoni mwa wakulima. Hii njia imewawezesha hata wakulima maskini kuweka fedha na kuweza kununua vitu vinavyotumika katika kaya na kuwekeza kwenye biashara.

### *Dhana ya ushirika wa kuweka na kukopa (UKKV/VSLA) kwa ufupi*

Kikundi cha UKKV/VSLA (mara zote huwa na wanachama 15-30) ambao hukutana mara moja kwa wiki kuweka akiba fedha za wanachama ambazo wanachama wanaweza kukopa pia. Vikundi vinapokea mafunzo jinsi ya kusimamia na kutunza fedha zao, kutengeneza katiba na kuchagua Bodi. UKKV/VSLA inaendeshwa kwa mzunguko wa mwaka mmoja. Kwa hiyo akiba iliyokusanywa na faida zinagawanywa kwa wanachama kulingana na jinsi walivyoweka akiba, na mzunguko mpya unaanza. *Fedha zote zinatokana na wanachama wenyewe* – hivyo hakuna mtaji wa kutoka nje unaohusika. Wanachama wanaweka akiba kwa kununua 'hisa' katika UKKV/VSLA. Wanachama wanaamua thamani ya hisa. Kila wiki mwanachama ananunua hisa kwa thamani iliyokubaliwa. Mwanachama yeyote anaruhusiwa kukopa kutoka kwenye kikundi cha UKKV/VSLA. Kawaida, mwanachama anaruhusiwa kukopa mara tatu ya kiasi cha fedha alizoweka akiba.

Riba ya kutozwa kwenye mikopo, muda wa kukaa na mikopo, na muda wa kila mzunguko unaamuliwa na wanachama. Mzunguko ukiisha, wanachama wanapokea hisa zao pamoja na faida iliyotengezwa kutokana na mikopo.

Kikundi kinapewa sanduku la kuhifadhi fedha na makufuli matatu, ambapo hakuna mwanachama mmoja anayeweza kufungua sanduku na kuchukua fedha. Miamala inaweza tu kufanyika pale ambapo wanachama wote wa kikundi wapo, ambayo inahakiksha uwazi na kuaminiana. Kumbukumbu zinawekwa kwenye kitabu cha mwanachama kwa kutumia mihuri ambayo hata mtu asiyejua kusoma anaweza kuhesabu kirahisi. Madeni anayodaiwa yanathibitishwa na wanachama waliokaa karibu na mkopaji kwenye kikao.

### *Wakati gani wa kuhusisha UKKV/VSLA kwenye mradi wa RIPAT*

UKKV/VSLA inaweza kuwa moja ya vipengele kwenye 'kapu la uchaguzi' katika mradi wa RIPAT. Inaweza kutambulishwa wakati wowote wa mzunguko wa mradi. Inaweza kuchaguliwa kama moja ya 'teknolojia ya kwanza katika uchaguzi' inayopatikana kwenye kikundi; vinginevyo, inaweza kutambulishwa baadaye wakati wakulima wameshaanza kupata pesa kutokana na teknolojia mpya za kilimo zilizotambulishwa.

Hata hivyo inapendekezwa, kama muda unaruhusu, kuanza UKKV/VSLA mapema iwezekanavyo. Mfumo wa kuweka na kukopa utawasaidia wakulima kupanua biashara ya shughuli za kilimo.

Ni muhimu kutambua kwamba wakulima ni watu wenye shughuli nyingi – hasa wakati wa majira ya kupanda – na SLM lazima liwe makini lisiwalemee wakulima kwa shughuli nyingi kwa wakati mmoja. Ratiba ya shughuli kwa kipindi cha miaka mitatu lazima ifikiriwe vizuri kabisa kupitia wakati wa kupanga mradi kwa kina.

*Tunza fedha pembeni*

Kujiunga na ushirika wa kuweka na kukopa ni uchaguzi wa wanakikundi, siyo shughuli ya lazima ambayo wanakikundi wote wanatakiwa kuifanya. Wale wanaotaka kujiunga (angalau watu 10-15) wataunda kikundi kidogo. Watapokea mafunzo maalum kuhusu dhana ya UKKV/VSLA na waunde katiba tofauti, kuchagua uongozi tofauti kwa ajili ya shughuli za UKKV/VSLA.

Uzoefu unaonesha kwamba wengi wa wakulima wa RIPAT wameonesha kutaka kujiunga na mfumo wa UKKV/VSLA. Baadhi ya vikundi vinachagua watu wale wale kama viongozi wa UKKV/VSLA kama ilivyo kwenye kikundi cha RIPAT; wengine wanachagua viongozi wapya kwa ajili ya shughuli hii. Hata hivyo, ni muhimu sana kutofautisha bayana mtaji kati ya UKKV/VSLA (kwa kuzingatia akiba za wanachama) na wa akaunti ya RIPAT (kuhusisha kipato kinachotokana na shughuli za pamoja za kikundi, kwa mfano kutokana na mauzo ya ndizi na mazao mengine kwenye mashamba la kikundi).

Ni muhimu kwamba mwezeshaji wa kikundi afundishwe kabisa kwa undani kuhusu dhana ya UKKV/VSLA kabla ya kwenda kutoa mafunzo kwa vikundi vya RIPAT. Undani kuhusu dhana ya UKKV/VSLA na mwongozo wa mafunzo hatua-kwa-hatua kwa ajili ya utekelezaji unaweza kupatikana kutoka kwenye mtandao www.vsla.net

## Hatua ya 11: Kikundi kujifunza kutoka kikundi kingine na mafunzo ya uongozi

Kikundi kujifunza kutoka kikundi kingine hufanywa kupitia mikutano ya robo mwaka (baada ya miezi mitatu), lakini siku za wakulima (ona Hatua ya 12) inatoa fursa ya kujifunza.

### *Uratibu wa mikutano ya robo mwaka*

Viongozi watatu wa kikundi, yaani mwenyekiti, katibu, na mweka hazina, wanatakiwa kushiriki katika mikutano ya robo mwaka. Vikundi 16 vyamradi wa RIPAT halisi vina viongozi 48 wa vikundi. Viongozi wa vijiji, na maafisa ugani wanaoshiriki kwenye mradi, na mratibu wa mradi aliyeteuliwa na wilaya pia anatakiwa kushiriki, hivyo kupelekea idadi ya watu katika mkutano kuwa kama 60 hivi.

Katika mikutano hii, masuala na mawazo yanayohitaji hatua kuchukuliwa kutoka kwenye viongozi wa kijiji au mamlaka ya serikali ya mtaa hujadiliwa. Maombi yanaandikwa na kupelekwa kwenye mamlaka zinazofaa. Maafisa ugani wanachangia mawazo yao na uchunguzi kwa ajili ya mafanikio ya vikundi vyote vya mradi wa RIPAT. Viongozi wa vikundi kawaida huchagua mwenyekiti na katibu wa viongozi wa vikundi kwa ajili ya mkutano huu na majukumu yao yameelezewa hapa chini.

Mwenyekiti wa mkutano wa viongozi wa vikundi:

- Kusimamia mikutano
- Kutembelea vikundi vyote kuona maendeleo

- Kuleta usuluhishi wa migogoro ndani ya vikundi na kati ya vikundi na vikundi
- Kutangaza mradi miongoni mwa viongozi wa vijiji kwa ujumla
- Kushauri meneja wa mradi na SLM mambo yanayohusiana na mradi/jamii

Katibu wa mkutano wa viongozi wa vikundi
- Kuchukua kumbukumbu za vikao na kuandika taarifa
- Kupeleka taarifa zozote muhimu kwa vikundi
- Kupokea taarifa za miradi kutoka kwenye vikundi

Mikutano ya robo mwaka ina makusudi yaliyofafanuliwa hapa chini.

*Kushirikishana uzoefu na masomo waliyojifunza, na kumtaarifu kila mmoja juu ya maendeleo ya mradi, mafanikio, na changamoto walizokutana nazo*

Viongozi wa kila kikundi wanatoa taarifa fupi ya mafanikio ya kikundi, ikujumuisha taarifa ya uigaji/uchukuaji wa teknojia na taarifa ya changamoto walizokutana nazo. Wanaeleza jinsi walivyokabiliana na hizo changamoto na nini walichojifunza kutokana na shughuli walizotekeleza kwa hiyo robo na taarifa ya uvumbuzi, uigaji wowote, na kadhalika. Washiriki wanajifunza kupitia kushirikishana, na kisha wanaweza kushirikisha wanakikundi wao ni nini wamejifunza kutoka kwa wanakikundi wenzao. Vikundi vinaweza kushirikishana taarifa juu ya masoko na bei za bidhaa, na wanaweza kuamua kuuza bidhaa zao kwa pamoja. Kuelekea mwisho wa mradi, mkutano unaweza kuangalia kuunda ushirika wa vikundi.

*Kuhakikisha kwamba unakuwepo ukaribu/mawasiliano mazuri na uelewa wa mradi kati ya viongozi wa kijiji na taasisi za kiserikali*

Vikundi vinahitaji msaada wa uongozi wa vijiji, na shughuli zao zinahitaji kulindwa. Kwa kuendelea kufuatilia maendeleo ya mradi kwa kila robo mwaka, viongozi wa vijiji wako kwenye nafasi kuchukua hatua yoyote muhimu, ikijumuisha kukuza uenezaji zaidi wa mradi kwenye kijiji, utekelezaji wa sheria ndogondogo na kadhalika. Kuhusisha viongozi wa vijiji kwenye mikutano ya robo mwaka inawezesha nguvu ya ushawishi kwa viongozi wa vikundi.

*Kusimamia maazimio ya migogoro yoyote kati na miongoni mwa wanakikundi*

Wakati mwingine kutokuelewana inatokea miongoni mwa wanakikundi, au wanakikundi na wanakijiji; wakati mwingine kesi za uharibifu wa mali za kikundi huripotiwa. Migogoro hiyo kama haitashughulikiwa na wanakikundi, mkutano wa robo mwaka unaweza kupitisha azimio na kuchagua wawakilishi wa kufuatilia kesi. Inaweza kutokea kwamba wanakikundi wanatumia vibaya mali ya kikundi na kukataa kulipa uharibifu, kwa mfano, kwa kesi kama hiyo mpatanishi wa nje anaweza kuhitajika.

*Kuratibu shughuli na maafisa ugani wa serikali*

Maafisa ugani wanajua kuhusu mipango na sera za serikali, ikijumuisha vitu kama msaada wa serikali kwa wakulima. Kwa hiyo wanaweza kuwashauri wakulima. Vinginevyo, maafisa ugani wanaweza pia kusaidia kueneza teknolojia kwa wakulima wengine ndani na nje ya vijiji vya mradi.

*Kujiandaa kwa ajili kuunda ushirika wa vikundi*

Mbinu za RIPAT zinatoa uwezekano wa kuunda ushirika wa vikundi ambao utaendelea na shughuli za mradi baada ya mradi kufungwa. Kiongozi wa jukwaa la viongozi wa vikundi anatoa msingi unaofaa kwa ajili ya kuanza huu mchakato (angalia Hatua ya 13 chini).

*Kufanya mafunzo ya uongozi kwa vikundi, na wakati mwingine kwa viongozi wa vijiji*

Ili kukuza mshikamano wa kikundi, ni muhimu kwamba viongozi wakawezeshwa kupitia mafunzo ya ujuzi wa uongozi. Mafunzo ya uongozi yanayohusiana na mada mbali mbali yanatolewa wakati wa mikutano ya robo mwaka.

Gharama za moja kwa moja kwa ajili ya chakula na usafiri kwa ajili ya mikutano ya robo mwaka zinatakiwa kulipwa kutoka kwenye bajeti ya mradi, lakini hakuna gharama nyingine zinazolipwa kwa watu wanaohudhuria hii mikutano. Hakuna 'posho za kuhudhuria vikao' zinazolipwa. Mikutano inatakiwa 'kumilikiwa' na washiriki, na wanakuja kwa sababu ni viongozi na wavumilivu katika kuwezesha maendeleo, siyo kwa sababu wanapokea pesa kwa kuhudhuria.

### *Maandalizi na ajenda*

Wakati wa kipindi cha mradi, meneja wa mradi na kiongozi wa jukwaa la viongozi wa vikundi wanaitisha mikutano ya robo mwaka. Taarifa ya mkutano inatumwa kwa kuwaandikia barua washiriki wote wanaotarajiwa kuhudhuria angalau mwezi mmoja kabla.

Kwa sababu vikundi vinatazamiwa kuwasilisha taarifa wakati wa mkutano, meneja wa mradi anatakiwa kuandaa mwongozo wa taarifa kwa kuzingatia taarifa zitakazohitajika kushirikisha na kujadiliwa katika mkutano huo *wa robo mwaka* (Sanduku 5.7).

Sanduku 5.7 Mwongozo wa taarifa ya kikundi kwa ajili ya mkutano wa robo mwaka

1. Hali ya kikundi
   - Kubadilika kwa wanachama
   - Mahudhurio
2. Hali ya maendeleo tangu mkutano wa mwisho
   - mafanikio kwa kila kilichotekelezwa
   - mgeni yeyote kwenye kikundi au tukio maalum
3. Changamoto na suluhisho
4. Mipango kwa robo mwaka ijayo

Ajenda za msingi kwa mkutano zinatakiwa kuwa kama ifuatavyo:

1. Kuandikisha mahudhurio
2. Maombi ya kufungua mkutano
3. Maneno ya kufungua yanatolewa na kiongozi wa mkutano
4. Malengo na matarajio ya mkutano (Meneja wa Mradi - MM)
5. Taarifa za vikundi na majadiliano
   (Makatibu kutoka kila kikundi wanatoa taarifa zao, na majadiliano mafupi yanafanyika kila baada ya taarifa kuwasilishwa juu ya maendeleo na magumu yoyote yanayozuia maendeleo. Mwenyekiti wa kijiji na afisa ugani wa kijiji husika wanatarajiwa kutoa maoni kila baada ya taarifa ya kikundi kuwasilishwa. Washiriki wachangie mawazo kuhusu suluhisho kwa changamoto ambazo zimeonekana na kuweka mkakati wa wakati ujao)
6. Majumuisho ya mijadala (Meneja wa Mradi- MM)
7. Maoni kutoka kwa Mratibu wa Mradi wa Wilaya (MMW)
8. Mwongozo wa matazamio (Meneja wa Mradi- MM)
9. Kufunga

Uwe makini mikutano isiendelee kwa muda mrefu hadi wakulima wakachoka na kupoteza usikivu. Kama ikitokea mara nyingi kuna hatari washiriki kukata tamaa na kukosa uvumilivu, matokeo yake kupoteza shauku. Wengine wanaweza kuanza kuacha mikutano ijayo, au kufika kwa kuchelewa au kuondoka mapema. Ni muhimu kwamba mikutano ikapangwa vizuri na mada zinazohusika zijadiliwe, kwa hiyo kila mmoja ajisikie kushiriki kwake ni muhimu. Hapa ni vitu vichache ambavyo mwenyekiti wa kikao anatakiwa kuzingatia kwenye akili:

- Weka mkutano kuzingatia na kuhakikisha kwamba kila mmoja anajikita kwenye ajenda. Usiogope kumkatisha mtu anayezungumza wakati wote au anayetoka nje ya mada inayojadiliwa – lakini ukimkatisha, jaribu kuweka hali iwe nzuri.
- Panga kabla ya muda kwamba mkutano uishe saa ngapi, na fanya bidii kuhakikisha iwe hivyo
- Kuwe na kikomo cha ajenda
- Weka akilini kwamba makusudi yote yamejadiliwa hapo juu. Chochote kisichoendana kulingana na makusudi kijadiliwe mahali pengine

*Mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa vijiji na vikundi*

Mikutano ya robo mwaka inatumika kutoa mafunzo ya uongozi. Mada zinazofundisha katika haya mafunzo ni ujuzi wa uongozi, utatuzi wa migogoro na matatizo. Kiongozi wa programu au meneja wa mradi anatakiwa kuendesha mafunzo.

Malengo ya mafunzo:

- Kuongeza umoja na ulinganifu miongoni mwa viongozi wa vijiji na vikundi katika kutekeleza mradi, na kuhakikisha kwamba wanaelewa jinsi ya kuchangia kwa mafanikio ya mradi
- Kuongeza maarifa ya utawala bora na hivyo kukuza maendeleo
- Kuhakikisha uelewa wa sheria ndogo ndogo zilizopo na utekelezaji wake katika kijiji husika. Mfano wa kawaida wa hizi sheria na utekelezaji wake unaweza kuwa sheria kuhusiana na ufugaji huria, kama ilivyoelezewa katika hatua ya 6 kwenye sura hii.

## Hatua ya 12: Siku ya wakulima na mahafali

Siku ya wakulima ni siku za maonesho ya mwaka ambapo teknolojia mbali mbali katika kapu la uchaguzi zinaoneshwa kwa kijiji na wageni kutoka maeneo yanayozunguka mradi. Katika mwaka wa tatu ambao ni wa mwisho wa mradi, siku ya wakulima inaunganishwa na sherehe za mahafali ambapo watu kutoka vijiji vilivyolengwa wanakuja pamoja katika kijiji kusherehekea matokeo ya mradi na kufanya mahafali kwa wanakikundi.

### *Malengo*

- Kuelekeza jamii, serikali za mitaa, na taasisi nyingine juu ya teknolojia mbali mbali zilizotekelezwa na maarifa ambayo vikundi vya RIPAT vimepata wanayaonesha na kushirikisha uzoefu wao.
- Kubadilishana uzoefu kati ya wanakikundi wa vikundi vya RIPAT na wakulima wengine, ofisi za serikali, maafisa ugani na wageni wengine.

### *Hatua*

Siku za wakulima inahusisha vikundi viwili vya RIPAT kila kijiji. Kwa kawaida hufanyika katika siku ambazo vikundi hukutana. Ni rahisi kupanga siku hizo na hakuna gharama ambazo mradi unaingia. Hatua kuu zimeorodheshwa hapa chini.

1. Kila vikundi viwili vinaunda kamati ya siku ya wakulima kupanga hilo tukio. Inatakiwa kufanyika kipindi cha mwaka wakati matokeo ya teknolojia bora yanaonekana.
2. Jamii za kijiji kizima na vijiji jirani wanaalikwa kwenye tukio, hasa viongozi wa kijiji na kata.
3. Mabanda ya maonesho yanatengenezwa (kwa kutumia rasilimali zilizopo) na hutumika kuonesha bidhaa zilizotokana na kufanyika kwa mradi. Wanakikundi wanaelezea jinsi walivyofikia matokeo yao.
4. Wakati wa siku ya wakulima, wageni wanatembelea mashamba ya vikundi vya RIPAT na kukagua mashamba mbali mbali ya maonyesho. Kama inawezekana, pia inapangwa watembelee mashamba ya wakulima binafsi.
5. Burudani kama nyimbo, maigizo/futuhi na mashairi huwepo. Hivi huwa na ujumbe unaotia hamasa wengine kuiga teknolojia bora. Katika Afrika, kuna msemo unasema kama unataka kuficha kweli, uandike katika kitabu; lakini kama unataka kuwasilisha kweli kwa watu, ziweke kwenye nyimbo, maigizo au ngoma.
6. Viongozi wa kikundi na kijiji wanaelezea kusudi la siku ya wakulima, na wanakikundi wanapewa nafasi ya kusema nini wamejifunza, na kueleza jinsi wengine wanavyoweza kufaidika kutokana na mradi.
7. Pia afisa ugani anaeleza shughuli za mradi.
8. Mwisho, viongozi wa kijiji wanahitimisha mkutano, kuwatia moyo jamii kuiga teknolojia za RIPAT.

## *Siku ya mahafali*

Katika mwaka wa tatu, siku ya wakulima inachukua muundo wa siku ya mahafali, ambayo inaleta pamoja vijiji vyote nane vya mradi wa RIPAT. Siku ya mahafali hufanyika kusherehekea mafanikio yaliyopatika wakati wa kipindi cha utekelezaji wa mradi wa RIPAT. Inatakiwa kuratibiwa na SLM kwa kuungana na viongozi wote wa vikundi.

Wadau wengi hualikwa, ikijumuisha viongozi wa serikali (katika ngazi za mkoa, wilaya na kata), na wadau wa maendeleo kwenye maeneo ulipotekelezwa mradi kama mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kiraia, mashirika ya dini, na wanajamii kutoka vijiji vilivyopitiwa na mradi na vya jirani. Ni tukio kubwa ambalo mara nyingi huhudhuriwa na watu karibu 1,000. Inajumlisha yote yaliyofikiwa katika kipindi cha miaka mitatu ya mradi na kueleza shauku ya kusambaza zaidi teknolojia za mradi chini ya uongozi wa jamii na serikali za mitaa. Wakulima wanatunukiwa vyeti vya ushiriki; kwa kawaida hivi vyeti husainiwa kwa kushirikiana na mamlaka za wilaya.

### *Uchaguzi wa wakulima bora wa kupewa zawadi*

Wakulima bora katika kila teknolojia bora huchaguliwa, kwa kushirikisha wanakikundi katika mchakato, kwa ajili ya zawadi ya siku ya mahafali. Mchakato wa uchaguzi huunza muda ambao tarehe ya siku ya mahafali hutangazwa miezi sita kabla. Vigezo kwa kila teknolojia bora vinaorodheshwa na meneja wa mradi na mwezeshaji wa kikundi na kupelekwa kwa wanakikundi (angalia mfano katika Sanduku 5.8)

Wanakikundi wanaweza kushauri mabadiliko kwa vigezo kwa misingi ya uchambuzi wao. Ikifuatiwa na majadiliano, kila kikundi kinapendekeza watu binafsi katika kikundi chao wanaofikia vigezo. Ubora wa kila mkulima aliyependekezwa hujadiliwa hadi apatikane mmoja au wawili bora zaidi.

Baada ya kila kikundi kumaliza kupendekeza watu wao bora, mwezeshaji wa kikundi na/au Meneja wa Mradi hutembelea shamba la kila aliyependekezwa kutathmini ubora wa utekelezaji kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho.

### *Hatua muhimu*

Hatua muhimu za kuzingatia siku ya mahafali ni hizi hapa chini

1. Mipango ya mahafali inaanza wakati wa mkutano wa mwisho wa robo mwaka, lakini tarehe hutangazwa na meneja wa mradi kwa vikundi miezi sita kabla. Viongozi wa vikundi vyote 16 katika mradi wa RIPAT huchagua kamati ya mahafali chini ya mwenyekiti wa mikutano ya viongozi wa vikundi.
2. Meneja wa mradi na kamati ya mahafali huamua eneo la siku ya sherehe za mahafali na kulitangaza hili kwa vikundi.
3. Taratibu za vikundi kufunga akaunti zao na kulipa madeni yoyote yaliyopo kwa SLM kulingana na katiba yao inatakiwa kutangazwa kwa vikundi kupitia wawezeshaji wa kikundi.
4. Wakulima bora (kupewa zawadi) katika kila teknolojia wanachaguliwa (angalia chini).
5. Mgeni rasmi (kawaida Mkuu wa Wilaya) hualikwa angalau mwezi mmoja kabla ya tukio, wakati wageni wengine muhimu hualikwa si zaidi ya wiki mbili kabla ya siku ya mahafali. Kwa kawaida mgeni rasmi anafahamishwa vizuri kuhusu mradi – lakini kama

### Sanduku 5.8 Mifano ya kuwapa zawadi wakulima bora na vigezo vyake

Mkulima bora wa migomba

- Idadi ya mashina ya migomba iliyopandwa, matandazo
- Kupanda kwa nafasi sahihi, usafi wa shamba, kuweka matandazo
- Kuacha migomba mitatu kwenye shina
- Kutumia mbinu nzuri za uvunaji maji ya mvua
- Mkulima amefundisha angalau wakulima wengine watatu wasio wa RIPAT na kuwapa miche ya kupanda

Mfugaji bora wa mbuzi/kondoo/nguruwe

- Nyumba inayofaa ya mnyama (rahisi kusafisha, nafasi ya kutosha, hewa nzuri, usalama)
- Idadi ya mifugo iliyoboreshwa, kisasa halisi/chotara
- Ulishaji sahihi (mimea, pumba)
- Udhibiti wa magonjwa na wadudu – kuwapa dawa za minyoo
- Utunzaji wa kumbukumbu

Mfugaji bora wa kuku

- Banda linalofaa la kuku (rahisi kusafisha, lina nafasi, hewa nzuri, usalama)
- Idadi ya kuku walioboreshwa, kisasa halisi/chotara
- Udhibiti wa wadudu na magonjwa – kuchanja kwa kuzingatia
- Kumbukumbu nzuri za uzalishaji na mauzo
- Ulishaji – kufuga nusu ndani na nusu nje, chakula cha ziada, siyo huria kabisa

Mkulima bora wa kilimo hifadhi

- Anafanya kilimo hifadhi na anaendelea (miaka miwili mfululizo au zaidi)
- Eneo lililopandwa kwa kutumia kilimo hifadhi
- Kuchanganya na mikunde/mazao funika
- Shamba halichungiwi mifugo (mabaki yanatunzwa)
- Ubora wa zao la mahindi

Mkulima bora wa mradi kwa ujumla

- Ametekeleza teknolojia mbali mbali, zote zimetekelezwa kulingana na mafunzo yaliyotolewa, ametumia rasilimali zilizopo/zinazopatikana kwake
- Anatengeneza kaya bora

Kikundi bora cha RIPAT

- Kina mahudhurio mazuri
- Kinafuata katiba
- Wanatenda sawa na maelekezo na ushauri wa
- Kimeiga teknolojia zilizochaguliwa
- Wametunza vizuri shamba/mashamba ya kikundi

Ni mgeni ameteuliwa siku si nyingi katika eneo la mradi, anaweza kutaka kutembelea mradi siku chache kabla ya mahafali ili kupata uelewa mzuri wa vitu vilivyotekelezwa kwenye mradi na mafanikio yake. Wakati wa kumwalika mgeni rasmi, inashauriwa siyo kumjulishakwa kifupi tu juu ya malengo na matokeo ya RIPAT, bali pia kumwonesha baadhi ya mada zinazotakiwa kujumuishwa kwenye hotuba ya siku ya mahafali. Hizi mada zinaweza kuwa:

- Kuimarisha sheria ndogo ndogo za kijiji
- Utunzaji wa mazingira
- Maafisa ugani kushirikiana na washiriki wa RIPAT na wakulima vichocheo
- Kueneza teknolojia kwa wakulima wa vijiji visivyo vya RIPAT
- Kuwatia moyo wanakikundi kuendelea kutumia teknolojia walizojifunza kupita mradi wa RIPAT

6. Kamati ya uratibu inapanga mipango ya shughuli za kufanya na kila kikundi kinaamua ni shughuli ipi itafanyika. Vikundi vinaandaa burudani (kwa masomo yanayohusiana na miradi) kwa siku, ikijumuisha mashairi, ngoma za asili, nyimbo, hotuba, mabango na maonesho. Pia wanapanga zawadi kwa wakulima bora.
7. Kamati ya uratibu inaandaa hotuba kwa niaba ya wanakikundi. Hotuba inaelezea mafanikio na changamoto walizokutana nazo wakulima, na kuiomba serikali kuendelea kusaidia shughuli za mradi.
8. Meneja wa mradi na kamati ya mahafali wanaandaa njia kwa ajili ya kutembelea teknolojia zilizotekelezwa katika vijiji mbali mbali (mashamba ya vikundi na watu binafsi). Hii itaonesha serikali na wageni waalikwa zile teknolojia zilizotekelezwa na mradi.
9. Siku ya mahafali, mgeni rasmi na wageni wanatembelea sehemu zilizochaguliwana kasha wanaelekea eneo latukio ambako mahafali yanafanyika.

## Hatua ya 13: Baada ya mahafali

### *Baada ya mahafali na uenezaji zaidi wa teknolojia*

Kama fedha zinapatikana, SLM lisiache kuwasiliana na wakulima baada ya siku ya wakulima. Ufuatiliaji kwa kutembelea vikundi kwa mwaka wan ne unashauriwa kuhakikisha mwendelezo mzuri.

Kwa sababu ya kipindi cha utekelezaji wa mradi kimefikia mwisho, ni ama kuondoa vibao vyote vinavyoonesha utekelezaji wa mradi wa RIPAT kwa pamoja, au angalau kubadilisha maneno kuwa kama ifuatavyo:




Vikundi vinakuwa rasilimali endelevu kwa ajili ya kuendeleza na kueneza teknolojia zaidi kwa kuzingatia ujuzi/maarifa, vipando, na mifugo. Wakulima vichocheo wa teknolojia na uenezaji huchaguliwa na kupata mafunzo kupitia mradi kwa ajili ya mwendelezo wa mradi na uenezaji (angalia Hatua ya 9 katika sura hii). Maafisa ugani wa eneo husika kushiriki kwa karibu kwa kipindi chote cha mradi kunahakikisha kwamba ujuzi wao unaenda na teknolojia bora mpya. Kufanya kazi kwa karibu kwa kushirikiana na maafisa ugani na wakulima vichocheo enezi unaanzishwa kuhakikisha kuendeleza na kueneza teknolojia baada ya mradi kuisha. ”Akademia” ya RECODA inatoa kozi za mafunzo kwa maafisa ugani na wakulima vichocheo jinsi wanavyoweza kufanya kazi zao katika kufundisha wakulima wapya na kwenye shughuli za uenezaji katika eneo baada ya kipindi cha mradi (tazama www.recodatz.org).

*Kuunda shirika la muungano wa vikundi*

Kuunda shirika la muungano wa vikundi, vikundi vinatakiwa kuwa na mapatano ya pamoja na kusudi na kushirikishana mambo, matatizo, na mahitaji yanayofanana. Hawatakiwi kutofautiana/kuwa mbali na mwingine. Kazi za shirika la muungano wa vikundi zinaweza kuwa:kununua kwa ujumla pembejeo na bidhaa

- soko kubwa la mazao yanayotoka kwa wanakikundi
- uratibu na mafunzo ndani ya vikundi
- huduma ya fedha za kuchangia za akiba na mikopo

Kabla ya kufunga mradi, viongozi wa kikundi wanatakiwa kujadili uwezekano wa kuunda shirika la muungano wa vikundi kwenye mikutano ya robo mwaka. Kama baadhi ya vikundi au vyote 16 vinataka kuunda shirika kama hilo, SLM linaweza kukubali kuwezesha huu mchakato. Hata hivyo, kabla ya kuanza kusaidia mchakato huu ni vema kutathmini kama vikundi husika viko tayari kuunda muungano na kama mazingira ya nje yanaruhusu. Mpaka sasa haijawa rasmi kama sehemu ya mbinu za mradi wa RIPAT kuunda shirika la muungano wa vikundi kwa hiyo ni nje ya huu mwongozo kuelezea kwa kina huu mchakato. Hivyo tuangalie kwenye miongozo kutoka sehemu nyingine (angalia mfano FAO 2001).

## Sehemu ya 3

# Ufuatiliaji na udhibiti wa ubora – mwongozo kwa mashirika mengine na SLM

**SURA YA 6**

# Ufuatiliaji na Udhibiti wa Ubora

Ufuatiliaji ni sehemu ya juhudi zozote za maendeleo ili kuweka kumbukumbu za mchakato wa utekelezaji na kuhakikisha kuna utaratibu sahihi wa kutafakari na kuchukua hatua ili kuboresha mchakato. Ufuatiliaji ni upimaji wa mara kwa mara wa kuangalia maendeleo ili kuona kama viwango na malengo yaliyowekwa kwenye mpango wa utekelezaji unafikiwa. Taarifa zinazokusanywa zinatumika kwa ajili ya usimamizi na kufanya maamuzi na kuwezesha kuendelea kujifunza wakati wa utekelezaji. Kuwa na taarifa kwa wakati mwafaka za maendeleo ya mradi (ziwe chanya au hasi) husaidia watu katika ngazi zote za mradi yaani vikundi, meneja mradi na wawezeshaji na uongozi wa SLM kuweza kufanya maamuzi yanayoweza kusaidia kukabiliana na matatizo au changamoto katika utekelezaji (Sanduku 6.1)

Sanduku 6.1 Nguvu na umuhimu wa kupima matokeo[1]

- Usipopima matokeo huwezi kutofautisha mafanikio na kushindwa
- Usipotambua mafanikio hautayazawadia
- Usipo zawadia mafanikio labda una zawadia kushindwa
- Usipotambua mafanikio huwezi kujifunza kutoka kwayo
- Usipotambua makosa huwezi ukayasahihisha
- Usipodhibitisha matokeo huwezi kupata kuungwa mkono na umma

1 Osborne na Gaebler (1992)

Ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa huhitaji muda na rasilimali nyingi na kwa hivyo lazima kuwa makini ili kutokukusanya taarifa sizizo za muhimu. Tumelenga kubuni mfumo ambao ni rahisi na unaotekelezeka.

Ufuatiliaji wa siku hadi siku wa wanakikundi wenyewe na viongozi wao na ule wa wawezeshaji kutoka SLM ni vya muhimu. Lakini wafanyakazi wanaotekeleza mradi wakikusanya taarifa za ubora wa kazi yao wenyewe hayawezi kuwa bila upendeleo – wanaweza kutaka mradi uonekane una mafanikio kuliko hali halisi ya mafanikio. Ni vigumu mtu yeyote kuwa na uhakika hasa wa kuhusu kiwango cha utendaji wake. Kujua ya kwamba utendaji au kazi ya mtu itaangaliwa na mtu wa tatu utapunguza upendeleo wa makusudi au usio wa makusudi katika ukusanyaji, uchambuzi na tafsiri ya taarifa/takwimu.

### *Ulinganifu wa Ufuatiliaji na kudhibiti ubora*

Katika mradi wa RIPAT, tunatofautisha kati ya ufuatiliaji na kudhibiti ubora. Taarifa za ufuatiliaji hukusanywa wakati wa utekelezaji wa mradi na kamati ndogo, viongozi wa vikundi, MM/WV lakini taarifa za kudhibiti ubora hukusanywa na wadhibiti ubora. Ili kuondoa upendeleo wadhibiti ubora wasihusike katika utekelezaji wa mradi. Kinadharia kudhibiti ubora kunastahili kufanywe na shirika lingine tofauti ambalo limetekeleza miradi

ya RIPAT kwa mafanikio au inayofanana na RIPAT (kama RECODA ambayo iko Arusha, www.recodatz.org) au vizuri kiasi kama utafanywa na idara tofauti kwenye SLM ambayo haitekelezi mradi na haiko karibu na wafanyakazi wanaotekeleza mradi.

Ni lazima ufuatiliaji na kudhibiti ubora kupangwe vizuri na lazima kuwe kwa muundo maalum ili kukusanya taarifa zote zinazohitajika kwa wakati mwafaka. Hapa chini tumeainisha zana za kukusanya taarifa kwa ajili ya ufuatiliaji na kudhibiti ubora. Kwanza tunaanza na shughuli za ufuatiliaji.

### *Ufuatiliaji wenye mpangilio*

Katika sehemu hii tunaainisha mifano ya jinsi kikundi na WV/MM wanaweza kufuatilia shughuli za mradi kwa miaka mitatu na kufuatilia kwa karibu hali na hadhi ya maendeleo ya kikundi.

Ni muhimu kuhakikisha wanakikundi wanamiliki au wanakuwa sehemu ya shughuli za ufuatiliaji. Wakati wa kuwezesha shughuli hizi, WV wasisitize ya kwamba ufuatiliaji sio shughuli inayofanyika ili kuwapendezesha wanaotekeleza mradi au mfadhili, mbali taarifa zinazokusanywa ni kwa manufaa yao – ili kikundi kijadili na kuzitumia katika kupanga shughuli zao. Wanakikundi lazima wahusike katika kutathmini maendeleo ya kikundi chao na wajadili hatua zozote za ziada zinazo hitajika kuchukuliwa kutokana na taarifa zinakazokusanywa.

Wakati wa mikutano ya kuratibu ya kila robo mwaka, viongozi wale watatu wanategemewa kutoa taarifa ya maendeleo ya kikundi chao kwa viongozi wengine wote wa vikundi na uongozi wa vijiji zikiwemo taarifa za mahudhurio, utekelezaji wa teknolojia tofauti na wanakikundi, maendeleo ya shamba la kikundi n.k. Taarifa hii inaandikwa kutokana na ufuatiliaji wa wanakikundi wenyewe chini ya usimamizi wa WV.

### *Taarifa katika ngazi ya kikundi*

Kikundi kina daftari ambalo katibu wa kikundi hutunza kumbukumbu zote za kikundi. Katibu afuatilie mahudhurio ya kikundi, wanakikundi – wanaoacha na wanaojiunga na kikundi. (Wanaoacha inaweza kuwa kwa sababu ya kifo, kuhama, sababu binafsi, kufukuzwa kwa sababu yoyote kwa mujibu wa katiba ya kikundi). Katika kila mkutano, mahudhurio ya wanakikundi yanawekwa kumbukumbu na asilimia ya mahudhurio yanakokotolewa.

X: wanakikundi waliohudhuria mkutano wa kikundi leo

Y: Idadi ya wanakikundi (wale ambao kikundi kinahesabu ni wanachama leo). Inajumuisha na wale ambao hawakuhudhuria leo kwa sababu fulani lakini ni wanakikundi.

Mahudhurio (X/Y *100) =_ _ _ _ %

Wastani wa mahudhurio kwa mwezi au kwa robo mwaka yanakokotolewa kama ilivyoonyeshwa.

Maendeleo ya shamba la kikundi kwa mfano idadi ya mashina ya migomba, idadi ya mikungu iliyovunwa, na vinastahili kuwekwa kama taarifa za shamba binafsi (mifano iko kwenye karatasi za kukusanyia takwimu).

*Ubora wa uwezeshaji wa kikundi*

Ufuatiliaji na kuainisha ubora wa uwezeshaji wa kikundi ni kazi muhimu na pia nyeti. Inastahili ifanywe na wanakikundi wenyewe. Kwa kawaida, WV hawawezi kuhusika kutathmini kazi yao wenyewe; WV wawaelekeze viongozi wa vikundi jinsi ya kujaza fomu hizi lakini WV hawastahili kuona hizi taarifa. Ni kiongozi wa programu tu kutoka shirika linalowezesha mradi na mtu wa tatu yaani mdhibiti ubora wanaostahili kuliona daftari lenye taarifa za utendaji kazi wa WV.

Kama ilivyoelezewa kwenye sehemu zilizotangulia vikundi vya RIPAT kwa kawaida hukutana mara moja kila wiki lakini wakati wa kilimo wanaweza kukutana mara mbili au zaidi kwa wiki. Wakati mradi unaanza, WV anatakiwa kukutana na vikundi mara moja kila wiki lakini baadaye, kadri kikundi kinavyoendelea kukua WV sio lazima waje kila wiki. Baada ya kila mkutano viongozi wa kikundi wanastahili wajaze taarifa zifuatazo kwenye vitabu vyao au karatasi walizopewa na SLM:

1. Je Mwezeshaji wa Kikundi(MK) alipangiwa kuja leo
   - ☐ Ndiyo
   - ☐ Hapana (nenda swali namba 8)

2. Je MK amekuja?
   - ☐ Ndiyo – kwa muda unaostahili
   - ☐ Ndiyo – alichelewa (kama alifika zaidi ya nusu saa)
   - ☐ Hapana, hakuja

3. Kama MK alikuwepo:
   Jina la MK aliyekuja_____________________

4. Ametumia muda gani kwenye kikundi? Saa ________

5. Je alirejea somo lililopita?
   - ☐ Ndiyo
   - ☐ Hapana

6. Somo la leo lilikuwaje?
   - ☐ Limeeleweka vizuri
   - ☐ Limeeleweka kiasi
   - ☐ Halikueleweka

7. Je MK ameacha zoezi la kufanywa na kikundi na/au ametaja somo linalofuata au hatua za kuchukua?
   - ☐ Ndiyo
   - ☐ Hapana

8. Afisa ugani alikuwepo leo?
   - ☐ Ndiyo
   - ☐ Hapana

Viongozi wa kikundi wawe tayari kumuonyesha Mdhibiti Ubora, Kiongozi wa Programu lakini sio MK au MM (angalia sehemu B hapo chini)

*Taarifa za kutekeleza/kuchukua teknolojia kwa wanakikundi*

Takwimu za ufuatiliaji wa jinsi wanakikundi wanachukua mbinu za kilimo bora kwa kila mwanakikundi huchukuliwa baada ya muda fulani kipindi chote cha utekelezaji mradi. Takwimu hizi hukusanywa na wajumbe wa kamati ndogo ndogo wakifanya kazi chini ya MK (angalia Sura ya 5 Saduku 5.6). Takwimu za kila teknolojia zijazwe kwenye karatasi tofauti na zikusanywe taarifa/takwimu muhimu tu (Jedwali 6.1). Mifano iliyoainishwa hapa chini sio miongozo tu inayoweza kutumika katika miradi yote ya RIPAT, ni mifano tu ambayo inastahili irekebishwe kulingana na mradi husika.

## **Jedwali 6.1** Mfano wa wakati wa kukusanya taarifa za uigaji wa teknolojia kutoka kwenye vikundi na wanakikundi mmoja mmoja kwa mradi wa miaka mitatu

Taarifa hizi zinastahili zikusanywe kwenye fomu maalum ya kila teknolojia kama inavyoonekana kwenye mpango, kwa mfano MK, M, KH, MM, M1, M2

| *Mpango wa Ufuatiliaji* | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *Mwaka 1* | | | | *Mwaka 2* | | | | *Mwaka 3* | | | |
| *Shughuli* | *R1* | *R2* | *R3* | *R4* | *R1* | *R2* | *R3* | *R4* | *R1* | *R2* | *R3* | *R4* |
| Mashamba ya kikundi k.m. migomba, kilimo hifadhi, uzalishaji mbegu | | MK | | MK | | MK | | MK | | MK | | MK |
| *Wakulima binafsi*<br>Migomba | M | M | | M | | M | | M | | M | | M |
| Kilimo Hifadhi | KH | | KH | | KH | | KH | | KH | | KH | |
| Mazao kama mihogo, viazi vitamu, ngwara, mbaazi | MM | MM | | MM | | MM | | MM | | MM | | MM |
| Mifugo k.m. mbuzi bora M1 | M1 | | M1 | | M1 | | M1 | | M1 | | M1 | |
| Kuku | M2 | | M2 | | M2 | | M2 | | M2 | | M2 | |

Mifano ya **[M]** na **[M1]** imeonyeshwa kwenye jedwali 6.2 na 6.3. Fomu nyingine ([KH], [M2], [MM]) zimewekwa kwenye kiambatanisho 4E. Taarifa zilizoko kwenye fomu hizi zinakusanywa na wanakamati husika wakati wa mkutano wa kikundi wakifanya kazi na wawezeshaji wa vikundi. Wanakamati husika na wawezeshaji wa vikundi pia hutembelea wanakikundi kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji na hukagua papo kwa hapo taarifa ambazo wanakikundi wamezitoa kwenye mkutano.

**Jedwali 6.2** Fomu ya ufuatiliaji wa Migomba [M] (jinsi wanakikundi walivyoiga/tekeleza teknolojia ya migomba)

| Jina la kijiji ........................ Jina la kikundi ....................... Robo ............................ | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jina la mwanakikundi | Idadi ya miche ya kisasa aliyopokea kutoka kwenye mradi | Idadi ya miche ya kisasa aliyopanda kwenye shamba lake | Idadi ya mashimbo yaliyoko shambani kwako ambayo hayajapandwa | Idadi ya miche uliowapatia wengine wasio wanakikundi | Idadi ya wakulima uliowapatia miche | Idadi ya mikungu uliovuna kutoka shamba lako |
| 1 | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | |
| 3 | | | | | | | |
| .... | | | | | | | |
| 35 | | | | | | | |
| Jumla | | | | | | | |

**Jedwali 6.3** Fomu ya ufuatiliaji wa taarifa za Mbuzi [M1] (jinsi wanakikundi walivyoiga/tekeleza teknolojia ya uzalishaji wa mbuzi bora)

| Jina la kijiji ........................ Jina la kikundi ........................ Robo ............................ | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Jina la mwanakikundi | Mkulima amejenga banda bora la mbuzi? (Ndiyo/hapana) | Mkulima amepokea mbuzi jike kutoka kwa mnyororo wa ugawaji wa mbuzi? (Ndiyo/hapana) | Mkulima anafuga kwa kufungia mbuzi ndani? (Ndiyo/hapana) |
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| ..... | | | | |
| 35 | | | | |
| Jumla | | | | |

## Kudhibiti Ubora

Hapa chini tumeeleza muundo wa kumhusisha mtu wa tatu katika kudhibiti ubora wa miradi ya RIPAT. Udhibiti ubora na mtu wa tatu (nje) unafanywa na Mdhibiti Ubora (MU) mwenye ujuzi na huru. Jukumu lake ni kama la mkaguzi wa hesabu – wakifanya ukaguzi wa papo kwa hapo ili kuhakikisha kumbukumbu zilizopo ni za kweli. MU hakagui kila kitu kwenye mradi bali hukagua mambo muhimu tu yatakayothibitisha kwamba utekelezaji unaenda kama ilivyopangwa. Fomu zilizopo hapa chini zimegawanyika mara mbili:

1. Taarifa zinazokusanywa kutoka kwenye vikundi 16 vya mradi
2. Taarifa zinazokusanywa katika ngazi ya mradi

MU hutembelea vikundi kwa wakati uliopangwa kukusanya taarifa za mradi kwa kutumia orodha zilizopo hapa chini.

*Taarifa katika ngazi ya kikundi*

Sehemu kubwa ya taarifa zitatolewa na viongozi wa vikundi ambao ndio wana taarifa za mahudhurio, maendeleo ya shughuli za kikundi na utekelezaji wa teknolojia na wanakikundi binafsi kwenye fomu rahisi kama ilivyoelezewa hapo juu kwenye sehemu ya ufuatiliaji. MU huchukua fomu zilizojazwa kutoka kwa kikundi k.m. mahudhurio na utekelezaji wa teknolojia tofauti tofauti kutoka kwenye kapu la uchaguzi. Lakini pia MU afanye ukaguzi wa papo kwa papo kwenye mashamba machache yaliyochaguliwa kibahati nasibu ili kuhakiki taarifa zilizojazwa kwenye fomu. MU pia awahoji viongozi wa vikundi na MM/WV na pia akusanye taarifa zingine kutoka kwenye SLM.

MU hukagua pia vitabu vya vikundi na kudondoa taarifa stahiki juu ya uwezeshaji wa kikundi na hutoa uamuzi kama uwezeshwaji ulikuwa wa kutosha au la. Kama ulikuwa hautoshi, ufuatiliaji unahitajika.

Ili uwezeshaji kikundi uwe wa kutosha WV wanatakiwa wawe:

- Wanatembelea kikundi kila wakati kama ilivyopangwa
- Wasiwe wamechelewa zaidi ya mara moja katika mara nne waliotembelea kikundi
- Kila wakati warejee somo lililopita na kusema nini kitafanyika somo linalofuata
- Wasiwe wamejaziwa “halikueleweka” kwenye somo lolote

*Taarifa katika ngazi ya mradi*

MU hupata taarifa hizi kutoka kwa MM ambaye hutunza taarifa za mahudhurio ya viongozi wa vikundi, vijiji, AU na MMW wanapohudhuria kwenye vikao vya robo mwaka vya kuratibu mradi. Taarifa zingine zote za mradi zinapatikana kwa MM.

*Jinsi ya kutumia taarifa hizi*

Inategemewa kuwa majibu yawe ‘ndiyo’ kwa maswali yote yenye majibu ya ‘ndiyo/hapana’ kwenye madodoso yaliyoko hapa chini ambayo yameainisha mazoezi saba ya ukaguzi wa udhibiti ubora kwa ajili ya mradi wa miaka mitatu. Kama jibu ni hapana MU akusanye taarifa juu ya shughuli hiyo au hali ya mradi ili kuchunguza kwa nini haikufikia kiwango kinachohitajika. Maelezo haya ayanakili kwenye daftari lake.

Kila baada ya zoezi la kudhibiti ubora, MU atatoa taarifa kwa SLM. Maswali ambayo majibu yake ni ‘hapana’ yawe yamewekwa alama na ijadiliwe jinsi ya kurekebisha makosa

hayo na SLM. Katika zoezi linalofuata la kudhibiti ubora, MU afuatilie kuona kama marekebisho yaliyohitajika yameshafanyika na SLM.

Kwa mfano kama mahudhurio ya wanavikundi yalikuwa chini ya 70% na uwezeshaji wa WV ulikuwa chini ya kiwango, MU awaulize viongozi wa kikundi kwa nini na aandike sababu hizo. Lakini MU asitoe ushauri wowote au kuamrisha jambo lolote kwa viongozi wa kikundi au WV/MM. Kazi ya MU ni kutoa taarifa nzima yenye lengo na iliyoainisha yote yaliyobainika/onekana kwa kiongozi wa program au SLM kwa ajili ya kufuatilia tatizo na kujifunza kutokana na hayo.

Mradi wa utekelezaji wa miaka mitatu unapendekezwa uwe na ziara saba za kudhibiti ubora. MU achukue taarifa kwa kutumia madodoso saba tofauti kwa ajili ya kila ziara. Muda wa ziara hizi kwa mradi wa miaka mitatu ni kama ifuatavyo:

Kabla ya mradi kuzinduliwa, MU lazima aangalie na kuhakikisha maandalizi ya mradi ni ya ubora unaostahiki na mchakato wote umehusisha wakulima, wataalamu na ofisi za serikali husika (mamlaka za serikali za mitaa). Mradi unastahili uwe umeelezewa vizuri kwenye maandiko stahiki na ushirikiano na mamlaka za wilaya pamoja na maafisa ugani watakaohusika - iwe imeelezewa kwenye mkataba wa maelewano.

| | Kabla | | | Mwaka wa 1 | | | | | | | | | | | | Mwaka wa 2 | | | | | | | | | | | | | Mwaka wa 3 | | | | | | | | | | | Baada | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwezi | | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | 32 | 33 | 34 | 35 | 36 | | | |
| | | 1 | | | 2 | | | | | | | 3 | | | | | | 4 | | | | | 5 | | | | | | | | 6 | | | | | | | | | | 7 | |

Mtiririko wa ziara saba za udhibiti ubora zitakavyofanyika na taarifa za kukusanywa katika kila ziara, kama inavyoelezwa kwa ufupi kwenye fomu hapo chini.

**Zoezi la 1 la Kudhibiti Ubora: Lifanyike kabla mradi haujazinduliwa. (Linafanyika katika ngazi ya mradi tu. Fomu ijazwe kwa ajili ya vikundi vyote 16 vilivyoko kwenye mradi)**

Lini: Kabla ya miradi kuzinduliwa

Namna gani: MU atamhoji kiongozi wa program/MM, achuje/aangalie maandiko ya mradi kama vile mihtasari ya vikao, taarifa ya uchunguzi wa hali ilivyokuwa awali, Andiko la mradi, ubao-mantiki, mpango wa kina wa utekelezaji (MKU), Mikataba ya maelewano (MwM) nk.

Jina la mradi ......................................................

Jina la MU ...........................................................

1. Mwakilishi wa wilaya alishiriki kwenye kufanya tathmini ya awali (alitembelea angalau 50% ya vijiji husika) ☐ Ndiyo ☐ Hapana
2. Afisa ugani alishiriki katika kufanya tathmini ya awali (alitembelea angalau 50% ya vijiji husika) ☐ Ndiyo ☐ Hapana
3. Mkutano wa kutengeneza mpango wa shughuli za mradi ulifanyika (Kukubaliana Ku) ☐ Ndiyo ☐ Hapana
4. Mkutano wa kutengeneza mpango wa shughuli za mradi ulihusisha wataalamu, mamlaka za serikali za mitaa, maafisa ugani (2 au 3) ☐ Ndiyo ☐ Hapana
5. Mratibu Mradi wa Wilaya (MMW) alichaguliwa ☐ Ndiyo ☐ Hapana
6. Mkataba wa makubaliano baina ya wilaya na SLM juu ya ushirikiano na ushiriki wa maafisa ugani umetiwa saini ☐ Ndiyo ☐ Hapana
7. Andiko la mradi, ubao-mantiki, mpango wa utekelezaji zipo (zinastahili ziwepo) ☐ Ndiyo ☐ Hapana
8. Wawezeshaji wanaotekeleza mradi wamefundishwa juu ya mfumo wa RIPAT na wamefaulu jaribio ☐ Ndiyo ☐ Hapana

**Zoezi la 2 la Kudhibiti Ubora**
**Taarifa zilizokusanywa kutoka kwenye kila kikundi**

Lini: Miezi 2 – 3 baada ya mradi kuanza

| Jina la MU ........................................... | Jina la Mradi ........................................................<br>Jina la kikundi.....................................................<br>Tarehe ...................................................................... |
|---|---|

1. Takwimu za wanakikundi:
   Idadi ya wanakikundi waliojiandikisha wakati wa kuunda kikundi
   Wanaume _______ Wanawake _______
   Jumla _______
2. Idadi ya walio hai sasa
   Wanaume _______ Wanawake _______
   Jumla _______
3. Idadi yawanakikundi walioacha tangu mradi uanze _______
4. Idadi ya wanakikundi wapya tangu mradi uanze _______
5. Wastani wa mahudhurio (asilimia) _______

Masuala maalumu

6. Mkutano wa kijiji ulihusisha mamlaka ya serikali za mitaa(wilaya, kata, kijiji) ☐ Ndiyo ☐ Hapana
7. Vigezo vya kutosha vilitumika kama ilivyoainishwa kwenye mwongozo wa RIPAT ☐ Ndiyo ☐ Hapana
8. Mkataba kati ya kikundi na shirika linalotekelza mradi kuhusu mahudhurio, kulipia pembejeo na mnyororo wa mifugo umesainiwa ☐ Ndiyo ☐ Hapana
9. Viongozi wa kikundi (watatu) wa muda wamechaguliwa ☐ Ndiyo ☐ Hapana
10. Viongozi hawa walichaguliwa kwa kura ya siri kama mwongozo wa RIPAT unavyoeleza ☐ Ndiyo ☐ Hapana
11. Mchakato wa kuandika Katiba ya kikundi unaendelea ☐ Ndiyo ☐ Hapana
12. Masharti ya lazima juu ya utekelezaji kama ilivyoainishwa kwenye kitabu cha mwongozo wa RIPAT yamewekwa kwenye katiba ya kikundi ☐ Ndiyo ☐ Hapana
13. Kikundi kimepata mashamba la kikundi ☐ Ndiyo ☐ Hapana
14. Mashamba yanafaa kwa ajili ya chaguo kutoka kwenye "kapu la uchaguzi" ☐ Ndiyo ☐ Hapana
15. Mkataba wa kukodi shamba kati ya kikundi na mwenye shamba umetiwa saini na nakala iko katika file la kijiji ☐ Ndiyo ☐ Hapana
16. Kikundi kimepata nakala ya sheria ndogo ndogo za kijiji ☐ Ndiyo ☐ Hapana
17. Uwezeshaji katika kipindi cha taarifa hii umekua
    ☐ unaridhisha ☐ hauridhishi (ufuatiliajo unahitajika)
18. Afisa ugani ametembelea kikundi mara _____ katika kipindi cha taarifa hii

Kutoka kwenye fomu za ufuatiliaji za kikundi ambazo zinahifadhiwa na katibu wa kikundi (k.m. [M], [M1] MU akusanye taarifa zifuatazo kulingana na kapu la uchaguzi na teknolojia iliyotekelezwa na wanakikundi binafsi

19. Teknolojia namba 1: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ___
20. Teknolojia namba 2: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ___
21. Teknolojia namba 3: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ___
22. Teknolojia namba 4: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ___
23. ..........

**Zoezi la 3 la Kudhibiti Ubora**
**Taarifa zilizokusanywa kutoka kwenye kila kikundi**

Lini: Miezi 9 – 10 baada ya mradi kuanza

| | |
|---|---|
| Jina la MU ……………………………………… | Jina la Mradi ………………………………………<br>Jina la kikundi ………………………………………<br>Tarehe ……………………………………………… |

1. Idadi ya wanakikundi waliohai sasa
   Wanaume ____________
   Wanawake ____________
   Jumla ____________
2. Idadi yawanakikundi walioacha tangu ziara ya mwisho ya KU ____________
3. Idadi ya wanakikundi wapya tangu ziara ya mwisho ya KU ____________
4. Wastani wa mahudhurio (%) ____________

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Katiba ya kikundi imekamilika | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 6. | Kikundi kina nakala ya sheria ndogo ndogo za kijiji | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 7. | Sheria ndogo ndogo za kijiji zimejadiliwa na kikundi wakati wa mikutano yao | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 8. | Viongozi wa kikundi watat u wa 'kudumu' wamechaguliwa | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 9. | Viongozi hawa walichaguliwa kwa kura ya siri kama mwongozo unavyoelezea | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 10. | Viongozi wa kijiji wakikuwepo wakati wa uchaguzi wa viongozi hawa | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |

11. Mwenyekiti: amechaguliwa yuleyule ☐ mwingine ☐
12. Katibu: amechaguliwa yuleyule ☐ mwingine ☐
13. Mtunza hazina: amechaguliwa yuleyule ☐ mwingine ☐

Shughuli za vikundi (kama ilivyo kwenye KU)

| | | |
|---|---|---|
| 14. | Mnyororo wa mga wanyo wa mifugo umeanza (kikundi kimeainisha wakulima watakaopokea mifugo, wameshapokea mifugo) | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 15. | Kikundi kimeunda kamati ndogo kulingana na KU | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 16. | Idadi ya kamati ndogo zilizoundwa ni | ____________ |
| 17. | Pembejeo zimesambazwa k wa wanakikundi kama kila mmoja alivyotaka (mfano mbegu, vipando, pembejeo za kilimo, majogoo) | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 18. | Pembejeo zilifika kwa wakati (kulikuwa na muda wa kuzitumia) | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 19. | Wakulima wamelipa nusu ya gharama ya pembejeo kama ilivyo kwenye makubaliano | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| 20. | Vijishamba vya majaribio vimeanzisha kwenye shamba la kikundi la kikundi | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |

21. Uwezeshaji katika kipindi cha taarifa hii umekuwa
    ☐ unaridhisha
    ☐ hauridhishi (ufuatiliajo unahitajika)
22. Afisa ugani ametembelea kikundi mara ___ katika kipindi cha taarifa hii

Kutoka kwenye fomu za ufuatiliaji wa kikundi ambazo zinahifadhiwa na katibu wa kikundi (k.m. [M], [M1] MU anakusanya taarifa zifuatazo (kulingana na kapu la uchaguzi na muda wa mradi)

23. Teknolojia namba 1: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
24. Teknolojia namba 2: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
25. Teknolojia namba 3: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
26. Teknolojia namba 4: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
27. ........

Shamba la kikundi

28. Kwa ajili ya teknolojia kuu ambazo kikundi kimetekeleza k.m. migomba
    Idadi ya mashina ya migomba ____________
    Idadi ya mikungu iliyovunwa ____________
29. .........

**II) Taarifa zinazokusanywa katika ngazi ya vikundi (kwa ajili ya vikundi vyote 16)**

Mikutano ya kuratibu mradi ya kila robo mwaka:

1. Mikutano ya robo mwaka ya kuratibu mradi imefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana
2. Wastani Mahudhurio ya viongozi wa vikundi ni (%) ____________
3. Wastani Mahudhurio ya viongozi wa vijiji ni (%) ____________
4. Wastani Mahudhurio ya AU (%) ____________
5. Wastani Mahudhurio ya MMW (%) ____________
6. Mafunzo kwa viongozi wa vikundi juu ya usimamizi wa fedha yamefanyika angalau mara moja ☐ Ndiyo ☐ Hapana

**Zoezi la 4 la Kudhibiti Ubora (KU)**
**Taarifa zikusanywe kutoka kwenye kila kikundi**

Lini: Miezi 15 – 16 baada ya mradi kuanza

| Jina la MU ............................ | Jina la Mradi ......................................<br>Jina la kikundi ...................................<br>Tarehe ................................................ |
|---|---|

1. Idadi ya wanakikundi wanaoendelea na kikundi hadi kufikia leo:
   Wanaume __________
   Wanawake __________
   Jumla __________
2. Idadi ya wanakikundi walioacha tangu ziara ya mwisho ya MU __________
3. Idadi ya wanakikundi wapya tangu ziara ya mwisho ya MU __________
4. Wastani wa mahudhurio (%) __________

5. Wakulima vichocheo katika fani tofauti wameainishwa na wanakikundi
   ☐ Ndiyo ☐ Hapana
6. Idadi ya wakulima vichocheo walioainishwa katika kikundi __________

7. Uwezeshaji katika kipindi cha taarifa hii umekuwa
   ☐ Unaridhisha ☐ Hauridhishi(unahitaji ufuatiliaji)
8. Afisa ugani ametembelea kikundi mara ngapi katika kipindi cha taarifa hii __________

Kutoka kwenye fomu za ufuatiliaji za kikundi ambazo zinahifadhiwa na katibu wa kikundi k.m. [M], [M1] MU akusanye taarifa zifuatazo kulingana na kapu la uchaguzi na teknolojia na muda wa mradi

9. Teknolojia namba 1: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia __________
10. Teknolojia namba 2: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia __________
11. Teknolojia namba 3: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia __________
12. Teknolojia namba 4: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia __________
13. ........

Shamba la kikundi

14. (Kwa ajili ya teknolojia kuu kwenye shamba la kikundi, k.m. migomba)
    Idadi ya mashina ya migomba __________
    Idadi ya mikungu iliyovunwa __________
15. ........

**II) Taarifa zinazokusanywa katika ngazi ya mradi (kwa ajili ya vikundi vyote 16)**

Mikutano ya kuratibu mradi ya kila robo mwaka:

1. Mikutano ya robo mwaka ya kuratibu mradi imefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana
2. Wastani Mahudhurio ya viongozi wa vikundi (%) ____________
3. Wastani Mahudhurio ya viongozi wa vijiji (%) ____________
4. Wastani Mahudhurio ya AU (%) ____________
5. Wastani Mahudhurio ya MMW (%) ____________
6. Mafunzo kwa viongozi wa vikundi juu ya usimamizi wa fedha yamefanyika mara moja ☐ Ndiyo ☐ Hapana

Masuala mengine katika ngazi ya mradi

7. Wakulima vichocheo wa fani mbali mbali wamepata mafunzo ya ziada ☐ Ndiyo ☐ Hapana
   (kwa kawaida inachukua siku 3 – 4 kwa mafunzo maalum ya wakulima vichocheo)
8. Afisa ugani wamefundishwa (pamoja na wakulima vichocheo) ☐ Ndiyo ☐ Hapana
9. Siku ya wakulima (maonyesho) imefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana

**Zoezi la 5 la Kudhibiti Ubora**
**Taarifa zitakusanywa kutoka kila kikundi**

Lini: Miezi 21 – 22 baada ya mradi kuanza

| Jina la MU....................................................... | Jina la mradi ..................................................<br>Jina la kikundi ..............................................<br>Tarehe ............................................................ |
|---|---|

1. Idadi ya wanakikundi hai mpaka sasa:
   Idadi ya wanaume ____________
   Idadi ya wanawake ____________
   Jumla ____________
2. Idadi ya walioacha kikundi tangu ziara ya mwisho la MU ____________
3. Idadi ya waliojiunga tangu ziara ya mwisho la MU ____________
4. Wastani wa mahudhurio kwa kipindi hiki (%) ____________

---

5. Kikundi kimebadilisha katiba yake? ☐ Ndiyo ☐ Hapana
6. Uchaguzi wa viongozi wa vikundi umefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana
7. Uchaguzi ulikuwa wa siri kama ilivyo kwenye kitini ☐ Ndiyo ☐ Hapana
8. Viongozi wa kijiji walikuwepo wakati wa uchaguzi ☐ Ndiyo ☐ Hapana
9. Mwenyekiti: ☐ Amechaguliwa yule yule ☐ Amechaguliwa mwingine
10. Katibu: ☐ Amechaguliwa yule yule ☐ Amechaguliwa mwingine
11. Mweka hazina: ☐ Amechaguliwa yule yule ☐ Amechaguliwa mwingine

---

12. Uwezeshaji wa kikundi katika kipindi cha taarifa hii umekuwa ☐ Unaridhisha ☐ Hauridhishi (unahitaji ufuatiliaji)

13. Mara ngapi afisa ugani ametembelea kikundi kwa kipindi cha taarifa husika

---

Kutoka kwenye fomu za vikundi ambazo zinawekwa na katibu k.m. [M] au [M1], MU akusanye taarifa zifuatazo (kulingana na kapu la uchaguzi na umri wa mradi).

14. Teknolojia namba 2: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
15. Teknolojia namba 3: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
16. Teknolojia namba 4: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
17. Teknolojia namba 4: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
18. ................

Shamba la kikundi

19. Kwa ajili ya teknolojia kuu ambazo kikundi kimetekeleza k.m. migomba
    Idadi ya mashina ya migomba ____________
    Idadi ya mikungu iliyovunwa ____________
20. ...................

**II) Taarifa zinazokusanywa katika ngazi ya vikundi (kwa ajili ya vikundi vyote 16)**

Mikutano ya kuratibu mradi ya kila robo mwaka:

1. Mikutano ya robo mwaka ya kuratibu mradi imefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana
2. Wastani Mahudhurio ya viongozi wa vikundi ni (%) __________________
3. Wastani Mahudhurio ya viongozi wa vijiji ni (%) __________________
4. Wastani Mahudhurio ya AU (%) __________________
5. Wastani Mahudhurio ya MMW (%) __________________
6. Mafunzo kwa viongozi wa vikundi juu ya usimamizi wa fedha yamefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana

**Zoezi la 6 la Kudhibiti Ubora**
**Taarifa zinazokusanywa kutoka kila kikundi**

Lini: Miezi 30 – 31 baada ya mradi kuanza

Jina la MU ............................................................ Jina la mradi ..............................................
Jina la kikundi ...........................................
Tarehe ..................................................................

1. Idadi ya wanakikundi hai mpaka sasa:
   Idadi ya wanaume _______________
   Idadi ya wanawake _______________
   Jumla _______________
2. Idadi ya walioacha kikundi tangu ziara ya mwisho ya MU _______________
3. Idadi ya waliojiunga tangu ziara ya mwisho ya MU _______________
4. Wastani wa mahudhurio kwa kipindi hiki (%) _______________

5. Wakulima vichocheo wa kueneza mradi wameainishwa na kikundi ☐ Ndiyo ☐ Hapana
6. Idadi ya wakulima vichocheo wa kueneza mradi waliochaguliwa _______________
7. Uchaguzi wa viongozi umefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana
8. Uchaguzi ulikuwa wa siri kama mwongozo wa RIPAT unavyoelekeza ☐ Ndiyo ☐ Hapana
9. Viongozi wa kijiji walikuwepo wakati wa uchaguzi ☐ Ndiyo ☐ Hapana
10. Mwenyekiti: ☐ Amechaguliwa yule yule ☐ Amechaguliwa mwingine
11. Katibu: ☐ Amechaguliwa yule yule ☐ Amechaguliwa mwingine
12. Mweka hazina: ☐ Amechaguliwa yule yule ☐ Amechaguliwa mwingine

13. Uwezeshaji katika kipindi cha taarifa hii umekuwa
    ☐ Unaridhisha
    ☐ Hauridhishi (unahitaji ufuatiliaji)
14. Mara ngapi afisa ugani ametembelea kikundi kwa kipindi cha taarifa husika

Kutoka kwenye fomu za vikundi ambazo zinawekwa na katibu, k.m. [M] au [M1], MU akusanye taarifa zifuatazo (kulingana na kapu la uchaguzi na umri wa mradi).

15. Teknolojia namba 1: wakulima wangapi wanatumia hii teknolojia _______________
16. Teknolojia namba 2: wakulima wangapi wanatumia hii teknolojia _______________
17. Teknolojia namba 3: wakulima wangapi wanatumia hii teknolojia _______________
18. Teknolojia namba 4 : wakulima wangapi wanatumia hii teknolojia _______________
19. ........

Shamba la kikundi

20. Kwa ajili ya teknolojia kuu ambazo kikundi kimetekeleza k.m. migomba
    Idadi ya mashina ya migomba
    Idadi ya mikungu iliyovunwa
21. ...........

**II) Taarifa zinazokusanywa katika ngazi ya mradi (kwa ajili ya vikundi vyote 16)**

Mikutano ya kuratibu mradi kila robo mwaka

1. Mikutano ya robo mwaka ya kuratibu mradi imefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana
2. Wastani Mahudhurio ya viongozi wa vikundi ni asilimia ________
3. Wastani Mahudhurio ya viongozi wa vijiji ni asilimia ________
4. Wastani Mahudhurio ya afisa ugani ________
5. Wastani Mahudhurio ya mratibu wa serikali wa mradi ________
6. Mafunzo kwa viongozi wa kikundi juu ya usimamizi wa fedha yamefanyika ☐ Ndiyo ☐ Hapana

Mambo mengine kwenye ngazi ya mradi

7. Tarehe ya mahafali imetangazwa kwa wanakikundi ☐ Ndiyo ☐ Hapana
8. Wakulima vichocheo wa kueneza mradi wamepata mafunzo ya ziada ☐ Ndiyo ☐ Hapana
9. Maafisa Ugani walifundishwa pamoja na wakulima vichocheo ☐ Ndiyo ☐ Hapana
10. Vijiji ambapo mradi utaenezwa vimeainishwa na wakulima vichocheo na maafisa ugani ☐ Ndiyo ☐ Hapana

**Zoezi la 7 la Kudhibiti Ubora (mwisho)**
**Taarifa zinakusanywa kutoka kwenye kila kikundi**

Lini: Mwezi 1 – 2 baada ya mradi kumaliza muda wake

| Jina la MU.............................................. | Jina la Mradi ..................................................<br>Jina la kikundi ................................................<br>Tarehe ......................................................... |
|---|---|

1. Kikundi kiliamua kuendelea kufanya kazi pamoja kama kikundi ☐ Ndiyo ☐ Hapana
   Kama ndiyo endelea na namba 2
   Kama hapana nenda namba 6

2. Kikundi kinaendelea
   Idadi ya wanakikundi walio hai sasa
   Wanaume ____________
   Wanawake ____________
   Jumla ____________

3. Wastani wa mahudhurio (%) ____________
4. Idadi ya wanakikundi walioacha kikundi baada ya mahafali ____________
5. Wanakikundi walioacha kikundi walipata mgao wao kutoka kwenye mali ya kikundi kulingana na kitini cha RIPAT (Katiba ya kikundi) ☐ Ndiyo ☐ Hapana

Kikundi ambacho hakiendelei

6. Kuvunjika kwa kikundi kuliamuliwa na theluthi mbili ya wanakikundi au zaidi ☐ Ndiyo ☐ Hapana
7. Taarifa ya akaunti za vikundi zimechukuliwa ☐ Ndiyo ☐ Hapana
8. Hela iliyopatikana iligawanywa kwa wanakikundi kulingana na mwongozo wa RIPAT (katiba ya kikundi) ? ☐ Ndiyo ☐ Hapana

Kutoka kwenye fomu za ufuatiliaji za kikundi ambazo zinahifadhiwa na katibu wa kikundi (k.m. [M], [M1] MU akusanye taarifa zifuatazo (kulingana na kapu la uchaguzi na muda wa mradi)

9. Teknolojia namba 1: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
10. Teknolojia namba 2: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
11. Teknolojia namba 3: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
12. Teknolojia namba 4: wakulima wangapi wanafanya hii teknolojia ____________
13. ........

Shamba la kikundi

14. Kwa ajili ya teknolojia kuu ambazo kikundi kimetekeleza k.m. migomba
    Idadi ya mashina ya migomba ____________
    Idadi ya mikungu iliyovunwa ____________
15. ..........

Taarifa zinazokusanywa katika ngazi ya mrandi (kwa ajili ya vikundi vyote 16)
Mikutano ya kuratibu mradi ya kila robo mwaka:
Kikundi kimefanya jitihada za kuunda umoja wa vikundi ☐ Ndiyo ☐ Hapana

# Viambatanisho

**KIAMBATANISHO CHA 1**

# Taratibu za uchaguzi

Mwezeshaji wa Kikundi (MK) awaandae wanakikundi kwa ajili ya uchaguzi na kuelezea utaratibu wa uchaguzi. Kwa uchaguzi wenye wagombea wawili MK alete sanduku, vikadi vidogo, makopo mawili kwenye mkutano wa kikundi. (Kwa ajili ya uchaguzi wenye wagombea zaidi ya wawili angalia maelezo hapo chini). Kopo moja liwe la langi nyeupe na jingine nyeusi. Makopo haya lazima yawe na mifuniko wenye mwanya ambao vikadi vinaweza kuingia (kama kisanduku la pesa). MK alete kadi mbili moja nyeupe na nyeusi. Katika kikundi, kila mwanakikundi apewe kikadi.

Wagombea wale wawili kila mmoja apewe kadi moja (nyeupe au nyeusi). Makopo yale yenye rangi yawekwe kwenye lile sanduku nyuma ya uzuio (au kwenye chumba) mbali kidogo na walipokaa wanakikundi na wapiti njia nyingine ili wengine wasione kinachoendelea. Kila mwanakikundi ataenda nyuma ya uzuio (au kwenye chumba) na wanakikundi wengine wasiwe wanaona lakini MK aweze kuona na kuweka kikadi chake kwenye kopo ambalo lina rangi ambayo mgombea anayetaka kumchagua (hata MK asiweze kuona kikadi kinawekwa kwenye kopo lipi).

Baada ya watu wote kupiga kura, MK ahesabu kura zote mbele ya wanakikundi wote kwa kutoa vikadi kutoka kwenye makopo na kuzihesabu. Ahakikishe kwamba hakuna vikadi vya ziada ambavyo vimewekwa kwenye makopo – idadi ya kura iwe sawa na ya wanakikundi waliopiga kura. Aliyepata kura nyingi zaidi ndiye mshindi. Utaratibu huu urudiwe kwa uchaguzi wa vyeo vyote vitatu.

Baada ya uchaguzi, MK atangaze majina ya viongozi watatu waliochaguliwa kuongoza kwa mwaka mmoja. Baada ya mwaka mmoja



uchaguzi huu utarudiwa kwa utaratibu zile zile. Viongozi hawa wanaweza kuchaguliwa tena au wakabadilishwa kwa kutumia utaratibu huo huo wa kidemokrasia.

Mfano huu wa uchaguzi umewahusisha wagombea wawili kwa ajili ya kila nafasi. Endapo kuna wagombea watatu, MK aongeze kopo lingine na kadi nyingine ya rangi tofauti.

Angalizo: Uchaguzi huu umetolewa kwenye mwongozo wa UKKV/VSLA.

VSLA (bila tarehe) *Village savings and loan associations (VSLAs). Field officer training guide*, Version 1.03, Solingen: VSL Associates. Available from Hugh Allen: hugh@vsla.net

**KIAMBATANISHO CHA 2**

# Mwongozo wa jinsi ya kuandaa katiba ya kikundi

Baadhi ya vifungu ni vya lazima katika mradi wa RIPAT; hivi vinaonekana katika maandishi ya mlazo.

| | *Kipengele* | *Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa* |
|---|---|---|
| 1 | Jina la kikundi | |
| 2 | Mawasiliano | |
| 3 | Maana ya jina | |
| 4 | Kibwagizo cha kikundi | |
| 5 | Eneo la shughuli la kikundi | |
| 6 | Mlezi wa kikundi | |
| 7 | Lengo kuu<br><br>Malengo mahususi | *Madhumuni ya kikundi cha RIPAT ni kuboresha maisha na kujenga uwezo wa wanakikundi wake kujisaidia wao wenyewe na kuhakikisha matokeo yanapatikana, pia kusaidia watu wengine kwenye eneo hilo ambao sio wanakikundi kupata mabadiliko/matokeo kama ya wanakikundi.*<br>Malengo mahususi ________________________________<br>________________________________<br>________________________________<br>________________________________<br>________________________________ |
| 8<br>8.1 | Uanachama<br>Majukumu ya wanakikundi | *Kwa RIPAT, wakulima wote wahusika wanajukumu la kufundisha wakulima wengine watatu ambao sio wana RIPAT kwenye jamii kile walichojifunza na walichokifanya. Kama kwa mfano, migomba imelimwa kama zao na mkulima, mkulima atatoa miche mara tatu zaidi kwa wakulima wasiokuwa wana RIPAT; na kwa mifugo kama vile mbuzi au nguruwe, mkulima atatoa mzao wa kwanza jike kwa wanakikundi wengine kama inavyoelezwa kwenye mnyororo wa pamoja wa kugawana mbuzi wa shirika.*<br><br>Majukumu mengine: ________________________________<br>________________________________<br>________________________________<br>________________________________<br>________________________________<br>________________________________ |

| | *Kipengele* | *Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa* |
|---|---|---|
| 8.2 | Hatua za kufuata wakati wa kumuondoa mwanachama na kupokea mwanakikundi mpya kwenye kikundi wakati wa muda wa mradi | a) Mwanachama anayejiunga: ______________________<br>______________________<br>______________________<br>______________________<br>b) Kumfukuza mwanachama: ______________________<br>______________________<br>______________________<br>______________________<br><br>*c) Kuacha uanachama*<br>*Mwanakikundi anaweza kuacha kikundi wakati wa muda wa mradi, mtu huyo hatapewa mali au utajiri uliopatikana kwenye kikundi. Mwanakikundi aweke sawa mahesabu yake na kulipa madeni yote anayodaiwa pamoja na pembejeo alizopewa (mbegu, vifaa, wanyama n.k) kwa SLM* |
| 8.3 | Kujiondoa kwa kikundi wakati wa mradi | *Kikundi kinaweza kuvunjwa na shirika au kwa uamuzi wake wakati wa muda wa mradi, vifaa na vitendea kazi walivyopewa bure vitarudishwa kwa shirika. Wanachama ambao ni wanakikundi walipe madeni yao kama inavyoelezwa kwenye kipengele cha 8.2.c* |
| 8.4 | Kugawana faida za kikundi wakati mradi unaendelea | *Wakati mradi unaendelea, hakuna gawio lolote kutoka mapato ya kikundi watakalolipwa wanakikundi* |
| 9 | Uchaguzi wa viongozi | *Uchaguzi wa viongozi uwe wa kidemokrasia ambapo kura lazima zipigwe kwa siri (Angalia Kiambatanisho cha 1 kwenye taratibu za kupiga kura). Mwanzoni mwa mradi, viongozi wa muda watachaguliwa kwa kipindi cha miezi mitatu. Baada ya miezi mitatu, viongozi wapya watachaguliwa. Viongozi waliokuwa wa mpito wanaweza kuchaguliwa tena iwapo wanakikundi wanawaona wanafaa, lakini kwa kutumia taratibu za kidemokrasia kama inavyoelezwa kwenye kiambatanisho cha 1. Uchaguzi mwingine unaweza kufanyika kila baada ya miezi 12. Kikundi kitaamua ni vpindi vingapi kiongozi anaweza kuendelea kuongoza.* |
| 9.1 | Kazi za viongozi | Majukumu ya mwenyekiti yatajumuisha:<br>• Kuanzisha mkutano wanapokutana<br>• Kutangaza ajenda na kuongoza majadiliano<br>• Kuhakikisha kwamba kikao kinafuata utaratibu na kwamba katiba inafuatwa na kuheshimiwa<br>• Kusimamia nidhamu na kutoza faini inapotakiwa<br>• Kuendesha majadiliano na kuhakikisha mawazo ya kila mtu yanasikilizwa na kuheshimiwa<br>• Kutatua migogoro<br>• Kukiwakilisha kikundi nje na kwa wasiokuwa wanakikundi kama vile serikali ya kijiji |

| Kipengele | Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa |
|---|---|
| 9.1 Inaendelea | • Kuwa wakili wa mali za kikundi.<br>____________________<br>____________________<br>____________________<br><br>Majukumu ya Katibu yanajumuisha:<br>• Kupanga muda na mahali mkutano utafanyika na kutoa taarifa<br>• Kuandika mihtasari ya vikao<br>• Kusoma mihtasari ya vikao vilivyopita<br>• Kutunza kumbukumbu za kikundi<br>• Kuandika barua na taarifa kwa niaba ya kikundi<br>• Kumsaidia mwenyekiti kwenye vikao<br>• Kufanya kazi kwa pamoja na mwenyekiti ili kuhakikisha kwamba katiba ya kikundi inafuatwa.<br>____________________<br>____________________<br>____________________<br><br>Kazi za mtunza hazina zinajumuisha:<br>• Kuweka kumbukumbu za mahesabu za kikundi<br>• Kutunza kumbukumbu za miamala za wanakikundi<br>• Kutunza kumbukumbu za mali za kikundi<br>• Kuandaa taarifa ya fedha<br>• Kutunza akaunti ya kikundi<br>• Kusoma taarifa ya fedha kwa kikundi inapohitajika<br>• Kukishauri kikundi njia bora za matumizi ya fedha.<br>____________________<br>____________________<br>____________________ |
| 9.2 Kamati ndogo ndogo za kikundi | Kamati ndogo ndogo za kikundi: Kikundi kitaanzisha kamati ndogo ndogo kulingana na teknolojia za kilimo zinazofuatwa na wanakikundi. Kila kamati itachagua kiongozi ambaye atatoa taarifa kwa mwenyekiti wa kikundi. Kazi za wajumbe wa kamati itakuwa ni kufanya ufuatiliaji kwenye teknolojia, mauzo ya mazao, na kuhakikisha kwamba ahadi zote zilizotolewa kulipia pembejeo zinatimizwa, kama vile malipo kupitia mnyororo wa kugawana mbuzi.<br><br>Kamati-ndogo: ____________________<br>____________________<br>____________________<br>____________________ |

| | Kipengele | Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa |
|---|---|---|
| 10 | Kazi kubwa ya kikundi na ratiba ya kukutana | Kazi kuu za kikundi: ________________________________<br>________________________________<br>________________________________<br>________________________________<br>Mahali, muda na siku ya wiki kwa ajili ya kukutana:________________________________<br>________________________________<br>________________________________ |
| 11 | Adhabu za utovu wa nidhamu kwa wanakikundi | Adhabu/faini:________________________________<br>________________________________<br>________________________________ |
| 12 | Marekebisho kwenye katiba | *Katiba inaweza kurekebishwa wakati wowote kama theluthi mbili ya wanakikundi watakubaliana. Ibara zilizoandikwa kwa mlazo zinaweza kubadilishwa na theluthi mbili ya kura zote baada ya muda wa mradi kuisha na baada ya malipo kufanywa kwa wanakikundi kama wakiacha kama inavyoelezwa kwenye paragrafu/ kifungu cha 16* |
| 13 | Mahesabu ya kikundi: Mapato na matumizi | *Mradi unapoanza, kikundi kitafungua akaunti ya kikundi. Akaunti ya kikundi itasimamiwa na viongozi waliochaguliwa ambao ni Mwenyekiti, Katibu na Mtunza hazina. Watahusika na kujaza kitabu cha fedha na kutengeneza mizania. Mapato na matumizi ya kikundi yawekwe/yaandikwe vizuri kwenye vitabu vya fedha. Taarifa ya fedha itatolewa kwa wanakikundi kila mwezi na kwa shirika itakuwa kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya ufuatiliaji.*<br>*Mapato ya kikundi yanatokana na kuuza mazao, adhabu na ada ya uanachama pale ambapo kikundi kinakuwa kimeamua kuwatoza wanachama wake.*<br>*Katika kipindi cha mradi fedha za kikundi zitawekwa benki au SACCOS iliyo jirani kwa mapendekezo ya shirika au zitatumika kwa kuendeleza kazi za kikundi. Baada ya miaka miwili, kikundi kitawekeza kwenye mali zisizohamishika kama theluthi mbili ya wanakikundi na shirika watakubaliana. Makubaliano ya shirika yatategemea kama kikundi kina;*<br>• *Mahudhurio mazuri*<br>• *Uongozi bora na kama walikuwa wanafuata katiba*<br>• *Mapato ya kila siku na utunzaji wa kumbukumbu.* |
| 14 | Mwisho/Kikomo cha mradi au mwakikundi kuacha mradi baada ya mradi kuisha | *Mwishoni mwa kipindi cha mradi kuisha, taarifa ya fedha itaandaliwa. Siku ya mwisho ya kumaliza mradi, madeni yote yawe yameshalipwa. Kikundi kinaweza kulipa kama inavyoelezwa kwenye kifungu cha 15 au kinaweza kuendelea kama ushirika baada ya wale wanaohitaji kulipwa kuwa wamelipwa hisa zao kama inavyoelezwa kwenye kifungu cha 16* |

| | Kipengele | Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa |
|---|---|---|
| 15 | Ufilisi wa mali na madeni ya kikundi | *Ufilisi wa mali za kikundi utafanyika baada ya mradi kuisha (kwa kawaida kila baada ya miaka mitatu) kama theluthi mbili watalipigia kura jambo hilo.*<br>*Kama shirika limetoa vitendea kazi bure kwa kikundi wakati mradi kama vile ripa, mabomba ya kupulizia dawa, machimbuo na vifaa vidogo vidogo, vitu hivi vitarudishwa kwenye shirika. Hakuna malipo yatakayotozwa na shirika kwa kurudisha vifaa hivyo. Mali za kikundi zitagawanywa na fedha itakayoridhiwa itagawiwa kwa wanakikundi. Mali za kikundi ni kama:-*<br>*a) Fedha taslimu kwenye mahesabu ya kikundi*<br>*b) Shamba lolote la kikundi la kukodisha (kawaida kwa mkataba wa miaka mitano). Shamba hilo kama itawezekana litakodishwa kwa muda uliobaki. Mfano mkataba wa kipindi cha miaka miwili kwa yeyote atakayelipa kwa bei ya juu*<br>*c) Shamba lolote linalomilikiwa na kikundi. Shamba hilo litauzwa kwa bei ya juu itakayokubaliwa*<br>*d) Mali nyinginezo*<br>*Fedha itakayopatikana kutoka a – d hapo juu itagawanywa kwa usawa kwa wanakikundi, mfano hisa 1/30 kwa kila mwanachama kama kuna wanakikundi 30 wakati wa kuhitimisha mradi* |
| 16 | Malipo kwa wanakikundi wanaoacha iwapo kikundi kimeamua kuendelea kama ushirika baada ya mradi kuisha | *Mwanakikundi anaweza kuacha kikundi wakati wa kuhitimisha na akaendelea kukifanyia kazi kile alichojifunza hata kwenye shamba lake au kwenye vikundi vingine. Mwanakikundi anayeacha atapata theluthi mbili ya hisa zake ya kile alichokizalisha. Kilichozalishwa na kikundi kinakokotolewa jumla yake kama ifuatavyo:*<br>*a) Fedha taslimu kwenye mahesabu ya kikundi*<br>*b) Kadirio la thamani yote ya shamba la kikundi, kama limekodishwa au linamilikiwa na kikundi; kama limekodishwa, thamani yake inabakia pale pale. Thamani yake itatathiminiwa na wanakikundi wenyewe. Kama kikundi hakitakubaliana kuhusiana na thamani na iwapo wanakikundi wanahitaji, shirika litapanga kwa ajili ya kufanya tathmini ya thamani kwa kumtumia mtaalamu mwingine huru. Gharama ya kukadiria italipwa na kikundi.*<br>*c) Thamani ya mali zingine kama ilivyokadiriwa na kikundi. Kama makubaliano hayatafikiwa, hatua kama zinavyoelezwa hapo juu zitafuatwa.*<br>*d) Madeni yote lazima yalipwe.* |

| | *Kipengele* | *Mambo yanayojadiliwa na yanayohusishwa* |
|---|---|---|
| 16 | inaendelea.. | Mfano: Kwenye kikundi chenye wanachama 30, wanakikundi 5 wanataka kuondoka baada ya kuhitimisha mradi, ambapo 25 wanahitaji kuendelea kama ushirika. Malipo ya wanaoacha inakokotolewa kama ifuatavyo:<br><br>Fedha halisi kwenye akaunti ya kikundi (kama ilivyo kwenye maelezo ya akaunti: TZS 500,000<br>Mapato kutoka shamba la kikundi (mauzo/kukodisha na kilichobaki: TZS 1,000,000<br>Mali nyingine TZS 500,000<br>Jumla ya fedha za kikundi TZS 2,000,000<br><br>Theluthi mbili ya mali zilizopatikana itaweka misingi ya kukokotoa hisa.<br>Kila mwanakikundi anayeacha kikundi atapata:<br>2,000,000 x2/3 x 1/30 = TZS 44,444<br><br>Kwa hiyo, kikundi kitalipa<br>5 x 44,444 = TZS 222,222. Hii italipwa ndani ya siku 60 baada ya barua ya maombi kupelekwa kwa mwenyekiti na mwanachama anayeacha kikundi.<br><br>(Kama pungufu ya theluthi mbili ya wanachama wanahitaji kuendelea kama ushirika, mali za kikundi zitakuwa zimelipwa, na wanakikundi wote kwenye suala hili la kinadharia watapokea<br>2,000,000 / 30 = TZS 66,666) |
| 17 | Mwanachama mpya anayejiunga na ushirika mwishoni mwa mradi wa RIPAT | Ada/masharti:________________________________<br>________________________________________<br>________________________________________<br>________________________________________<br>________________________________________<br>________________________________________<br>________________________________________<br>________________________________________<br>______________________________________ |

**KIAMBATANISHO CHA 3**

# Mwongozo wa kitaalamu na rasilimali

Mradi wa RIPAT unajumuisha ‘kapu la uchaguzi’ linalowapa wakulima fursa ya kuchagua teknolojia nzuri ya kilimo atakayoiga. Mfumo wa kuweka na kukopa na wenyewe umekuwa sehemu ya kutekelezwa na mradi wa RIPAT hadi sasa. Mwongozo uliopo kwa sasa hausimami wenyewe kama rasilimali kitabu. SLM linajumuisha mwongozo wa RIPAT na maelezo ya mwongozo wa kitaalamu kwa teknolojia husika ya kilimo na shughuli zinazojumuishwa katika mradi wa RIPAT husika. Utajiri wa rasilimali nzuri (mwongozo, waraka wa kitaalam) vinapatikana katika mashirika mbali mbali na nyenzo nyingi zinaweza kupakuliwa kutoka kwenye mtandao bila malipo. Zifuatazo hapa chini ni baadhi ya rasilimali zinazoweza kutumika. Hii inahusishwa na teknolojia halisi kwenye ‘kapu la uchaguzi’ lililotumika katika miradi halisi ya RIPAT hadi sasa.

Inapatikana kutoka:

**Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Dar es Salaam, Tanzania**

Kanyeka, E., Kamala, R., Kasuga, R. (2007) *Improved agricultural technologies recommended in Tanzania.* Dar es Salaam: Department of Research and Training, Ministry of Agriculture Food Security and Cooperatives

Inapatikana kutoka:

**Village Savings and Loan Associates**

The*VSL programme guide for field officers* and the*VSL programme guide for vilage agents* are available for free download at http://vsla.net/home

Inapatikana kutoka:

**Sustainet E.A.**

Miongozo mingine rahisi inapatikana bure hapa:
www.sustainetea.org/sustainet_programme_03_knowledge_information.html_

Kwa mfano

- *Mbuzi bora wa maziwa*
- *Uhifadhi wa maji na udongo*
- *Kilimo hifadhi*
- *Mfumo jumuishi wa kilimo*

Inapatikana kutoka:

**FAO (Food and Agriculture Organization of the United Nations)** Better Farming Series

Kwa Mfano:

- *Sheep and Goat breeding* – Better Farming Series 12
  http://www.cd3wd.com/cd3wd_40/lstock/001/goats/sh-goatbreedingfao/fb12se/index.htm
- *Keeping chickens* – Better Farming Series 1 3
  http://www.cd3wd.com/cd3wd_40/lstock/001/chickens/keepchickensfao/fb13ke/index.htm
- *Roots and tubers* – Better Farming Series 1 6
  http://www.cd3wd.com/cd3wd_40/cd3wd/agric/fb1 6re/en/b81 .htm
- *Bananas* – Better Farming Series 18
  http://www.cd3wd.com/cd3wd_40/cd3wd/agric/fb1 8be/en/b83.htm
- *Processing of Cassava and sweet potatoes for animal feeding* – Better Farming Series 44
  http://www.cd3wd.com/cd3wd_40/lstock/001 /lsfeed/fb44pe/index.htm
- *Use of Cassava and sweet potatoes in animal feeding* – Better Farming Series 46
  http://www.cd3wd.com/cd3wd_40/lstock/001 /lsfeed/fb46ue/index.htm

**Vyanzo vingine kutoka FAO vilivyohusishwa, kwa mfano,**

- *Conservation Agriculture. A manual for farmers and extension workers in Africa.*
  http://www.fao.org/ag/ca/AfricaTrainingManual.html
- *A study guide for farmer field schools and community based study groups. Soil and water with a focus on water harvesting and soil moisture retention. Parts 1 and 2*
  http://www.fao.org/fileadmin/templates/nr/images/resources/pdf_documents/FARMESA_SWC1 .pdf
- http://www.fao.org/fileadmin/templates/nr/images/resources/pdf_documents/FARM ESA_SWC2. Pdf

Vinavyopatikana kutoka:

**The Conservation Farming Unit in Zambia** http://conservationagriculture.org

Baadhi ya mifano:

- *A guide for farmers: Conversion from ox ploughing to min-till ripping using the Magoye ripper:* http://conservationagriculture.org/u ploads/pdf/ADP%20M IN-TI LL%20 RIPPING%20FARMERS%20GUIDE.pdf
- *The practice of conversional and conservation agriculture in East and Southern Africa.*
  http://conservationagriculture.org/uploads/pdf/CONVENTIONAL%20%20CA%20FARM I NG%20SYSTEMS%20IN%20ESA.pdf
- *Hoe CF – Land preparation and basal dressing.* http://conservationagriculture.org/uploads/pdf/CF%20Hoe%20Land%20Preperation%20%20Basals%20201 2.pdf

Vinavyopatikana kutoka:

**Agromesia – Knowledge sharing for sustainable agricultural development**
Agrodok – Popular series of 44 books on small-scale sustainable agriculture
http://www.agromisa.org/

Kwa mfano:

- *Kilimo cha soya na mazao mengine ya jamii ya mikunde*
- *Ufugaji wa mbuzi kwenye maeneo ya kitropiki*
- *Ufugaji wa nguruwe kwenye maeneo ya kitropiki*
- *Utunzaji na uhifadhi wa nafaka na kunde*
- *Uzalishaji mdogo mdogo wa kuku*
- *Usimamizi wa rutuba ya udongo*
- *Uvunaji wa maji na uhifadhi wa udongo wenye unyevu*

Vinavyopatikana kutoka:

**IPM info**

*Manual on group dynamics for Farmer Field Schools*

Free to download from their website http://ipm-info.org/group-dynamics/exercises.htm

## KIAMBATANISHO CHA 4

# VIELELEZO

## KIAMBATANISHO CHA 4A:

# MKATABA WA KUKODISHA SHAMBA LA KIKUNDI

[Nembo ya SLM]

FOMU YA MKATABA WA KUKODISHA SHAMBA LA KIKUNDI

Tarehe...................................................................

Kijiji.....................................................................

Kata......................................................................

Wilaya...................................................................

Jina la Kikundi ..........................................

Sisi viongozi watatu wa kikundi cha RIPAT kilichotajwa hapo juu, kwa niaba ya wanakikundi wenzetu tunakodisha shamba kutoka kwa .................kwa masharti yafuatayo hapo chini:

Shamba litatumika kwa shughuli za kikundi cha RIPAT. Ukubwa wa shamba ni eka ............ ambalo liko eneo la ............. katika kijiji cha ............ na kitongoji cha ......... Mkataba huu ni kwa miaka.......(kama shamba ni kwa ajili ya kilimo cha ndizi isiwe chini ya miaka mitano). Gharama ya kukodisha ni TZS......kwa mwaka.

Mkataba huu unaweza kurudiwa tena kwa upya kwa makubaliano na mwenye shamba. Shamba hili litatumika kwa ajili ya shughuli za kilimo tu (kama ni kwa ajili ya kujifunzia, uzalishaji wa mbegu, uzalishaji wa mazao n.k.)

Kikundi kitahusika na usalama na utunzaji wa shamba kwa kipindi chote cha mkataba. Mwenye shamba haruhusiwi kulitumia shamba kwa shughuli yoyote ile mpaka kipindi cha mkataba kitakapokwisha ndipo atakaporudishiwa shamba lake. Baada ya mkataba kuisha, mazao yote yatakayokuwepo shambani yatakuwa ni mali ya mwenye shamba. Ndani ya kipindi cha mkataba, ukodishaji wa shamba unaweza kuhamishiwa kwa mtu watatu (likiwa na mazao yake) ili aweze kuenndeleza shughuli za kilimo.

Mkataba huu umesainiwa na:

1. Mwenye shamba

Jina....................................... Sahihi...................... Tarehe..................

2. Mwenyekiti wa kikundi

Jina....................................... Sahihi...................... Tarehe..................

3. Katibu wa kikundi

Jina....................................... Sahihi...................... Tarehe..................

4. Mhasibu wa kikundi

Jina....................................... Sahihi...................... Tarehe..................

5. Shahidi

Jina....................................... Sahihi...................... Tarehe..................

6. Mwenyekiti wa Kijiji na au/ Afisa Mtendaji wa kijiji

Jina....................................... Sahihi...................... Tarehe..................

7. SLM

Jina....................................... Sahihi...................... Tarehe..................

KIAMBATANISHO CHA 4B:

# FOMU YA MKATABA UNAOHUSU MNYORORO WA MGAWANYO WA WANYAMA

Mkataba huu unatumika kwa kila mwanakikundi ambaye anapokea mnyama kwa mara ya kwanza kutoka kwenye hazina ya wanyama bora. Kwa wale wanakikundi wanaopokea wazaliwa wa kwanza, kikundi kitaandaa mkataba rahisi kati ya mwanakikundi na viongozi wa kikundi.

[Nembo ya SLM]

## FOMU YA MKATABA WA MNYORORO WA MGAWANYO WA WANYAMA KATI YA SLM NA VIONGOZI WA KIKUNDI

Tarehe.......................................................

Kijiji.........................................................

Kata..........................................................

Wilaya.......................................................

Jina la Kikundi ..........................................

Sisi viongozi watatu wa kikundi cha RIPAT waliotajwa hapo juu, tunakiri kuwa kwaniaba ya wanakikundi wenzetu, tumepokea madume watatu na majike watano wa.............(Aina) bila malipo kutoka kwa..................... (SLM)

Madume wawili na majike watano wanagawiwa kwenye kikundi kama hazina ya uzalishaji.Watoto waliozaliwa watagawanywa tena ndani ya wanakikundi kwa kutumia 'mnyororo wa mgawanyo'. Mara baada ya kumaliza kugawa Majike...... waliozaliwa kwa wanakikundi wenzake, huyo mnyama ambaye aliyepewa awali anabaki kuwa mali yake.

Sheria zifuatazo zitafuatwa:

1. Kabla ya kupokea mnyama (kama hazina ya uzalishaji au watoto waliozaliwa), mwanakikundi awe amejenga banda kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na mradi.

2. Majike ……….. wa kwanza waliozaliwa lazima wagawanywe kwa wanakikundi wengine wanaofuata kwenye mnyororo kama ilivyopangwa na kikundi. Jike lililopokelewa kwa mara ya kwanza litabaki kuwa mali ya kikundi hadi hapo mgawanyo utakapokuwa umekamilika.

3. Wanachama wa mnyororo wa mgawanyo wanapaswa kutoa taarifa kwenye kikundi juu ya hali ya afya ya mnyama/wanyama ambao wamewapokea na juu ya mpango wa uzalishaji. Wanawajibika kuwatunza wanyama kwa gharama zao wenyewe, ikiwa ni pamoja na kuwapa matibabu. Kama mnyama atapotea au kufa na sababu zikajulikana kuwa ni uzembe kwa suala la mnyororo wa mgawanyo, mtu huyo atapaswa kumrudisha mnyama kwa gharama zake mwenyewe au kulipa thamani ya huyo mnyama kwenye kikundi.

Wafuatao ni wanakikundi saba ambao wamechaguliwa na kikundi kupokea mgao wa kwanza wa hazina ya wanyama walioboreshwa.

Wanakikundi waliopokea majike

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Wanakikundi waliopokea madume:

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Viongozi wa Vikundi:

Mwenyekiti wa kikundi

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Katibu wa kikundi

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Mhasibu wa kikundi

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Mwenyekiti wa Kijiji/au Afisa Mtendaji wa kijiji

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

Shirika linalotekeleza mradi - SLM

Jina…………………………………… Sahihi…………………….. Tarehe…………………..

KIAMBATANISHO CHA 4C:

# FOMU YA MKATABA WA PEMBEJEO/ZANA

[Nembo ya SLM]

## FOMU YA MKATABA WA PEMBEJEO/ZANA KATI YA SHIRIKA LINALOTEKELEZA MRADI NA VIONGOZI

Tarehe.................................................

Kijiji.................................................

Kata.................................................

Wilaya.................................................

Jina la Kikundi .......................................

Sisi viongozi watatu wa kikundi cha RIPAT waliotajwa hapo juu, tunakiri kuwa kwa niaba ya wanakikundi wenzetu tumepokea zana/vifaa vifuatavyo

.......................................................................................................................................................

.......................................................................................................................................................
............................ pasipo gharama yoyote kutoka kwa.................................................... (SLM)

Sheria zifuatazo zitafuatwa:

1. Kikundi kitawajibika kutunza zana na kufanya matengenezo ya mara kwa mara, na kitachagua mtu mmoja au zaidi kuangalia zana hizo.
2. Viongozi wa kikundi watahakikisha kuwa vifaa/ zana hizo zitapatikana kwa yeyote anahitaji kwa usawa kwa wanakikundi wote.
3. Kama kikundi kitakuwa kimesambaratika kabla ya miaka 3 ya mradi kama ilivyopangwa, vifaa/zana lazima zirudishwe kwenye SLM. Hakuna malipo yoyote yatakayofanywa na SLM kwa vifaa vilivyorudiswa.
4. Baada ya miaka mitatu, wakati mradi unafikia mwisho, na kama kikundi kitaendelea kama ushirika zana hizi zitabakia na kupatikana kwa matumizi ya kikundi na kwa wanakikundi wake.
5. Baada ya miaka 3, wakati mradi umefikia mwisho na kama kikundi kikaamua chenyewe kufikia mwisho baada ya sherehe za kuhitimisha mradi, vifaa/zana zitarudishwa kwenye shirika linalotekeleza mradi. Hakuna malipo yatakayofanywa na SLM kwa ajili ya vifaa vilivyorudishwa.

Mkataba huu umesainiwa na:

1. Mwenyekiti wa Kikundi

Jina……………………………………………….. Sahihi…………….. Tarehe……………………..

2. Katibu wa kikundi

Jina………………………………………………. Sahihi……………. Tarehe……………………..

3. Mhasibu wa Kikundi

Jina ………………………………………….… Sahihi…………… Tarehe……………………

4. Mwenyekiti wa kikundi/au Afisa mtendaji wa Kijiji

Jina…………………………………………… Sahihi………….. Tarehe……………………

5. SLM

Jina………………………………………….. Sahihi…………… Tarehe……………………

KIAMBATANISHO CHA 4D:

# KIELELEZO CHA MKATABA WA MAKUBALIANO

[Nembo ya shirika tekelezaji ] [Nembo ya Wilaya husika]

**MKATABA WA MAKUBALIANO (MwM)**

Kati ya

____________________________(weka jina la shirika linalotekeleza mradi - SLM)

na

__________________________________________________________ (weka jina la wilaya)

Mkataba huu wa maelewano unafafanua namna ambavyo waweka sahihi wa taasisi au mashirika watashiriki na hii haimaanishi namna yoyote ya fedha ambazo zitatunzwa kama msingi wa matumizi.

## 1. KUSUDI NA MADHUMUNI

Makusudi ya mkataba huu wa maelewano ni kuainisha kazi na wajibu wa kila upande kwakuwa wanahusika katika utekelezaji wa mradi wa RIPAT.

RIPAT ni mbinu ya maendeleo ya kiuchumi inayolenga kuleta karibu teknolojia za kilimo ili kuziba pengo kama njia ya kuboresha maisha na kuwafanya wakulima wadogo wadogo wa Tanzania waweze kujitegemea.

Kwa zile familia za wakulima wanaoshiriki moja kwa moja kwenye miradi ya RIPAT, lengo ni kuboresha mifumo ya wakulima wadogo wadogo na hivyo kuongeza usalama wa chakula katika kaya na kupunguza umaskini- kwa kuanzia na idadi ndogo ya wakulima - lakini baadaye kuenea kupitia uwezeshaji wa jamii kwa ukubwa.

Mradi wa RIPAT wa sasa utalenga vijiji vifuatavyo:

1. ______________________________
2. ______________________________
3. ______________________________
4. ______________________________
5. ______________________________
6. ______________________________
7. ______________________________
8. ______________________________

……

x. ______________________________

Vikundi viwili vya wakulima vitaundwa kwa kila kijiji, kila kikundi kitaundwa na wakulima 30-35.

Tathmini wa awali imekamilika kwa kushirikiana na mamlaka za wilaya, na hii imewezesha kutengenezwa kwa mradi wa RIPAT ambao upo tayari kwa kuzinduliwa. Mpango kazi wa eneo/kijiji husika umetengenezwa kwa kushirikiana na wawakilishi wa wilaya, na hii inajumuisha maandalizi mazuri ya 'kapu' la uchaguzi wa teknolojia za kilimo zilizoboreshwa ambazo zimepangwa na kuwekwa wazi kwa vikundi……. vya RIPAT kwa kipindi chote cha mradi.

SLM linategemea kwamba mwisho wa mradi wawakilishi wa wilaya – hasa maafisa ugani (AU) - watawajibika zaidi kwa kusimamia vikundi hivi vilivyoundwa na kuendelea kueneza na kukuza ili kuweza kuinufaisha jamii kwa upana zaidi.

## 2. WAJIBU

A. SLM litafanya:

1. Kwa kushirikiana na mamlaka za serikali za vijiji i) kwa uangalifu wataihamasisha jamii kwa kiwango cha kubadilika na kuwahamasisha wakulima kuchukua hatua ya maendeleo yao wenyewe na ii) kuchagua wakulima na kuunda vikundi …. vya wakulima (viwili kwa kila kijiji)
2. kuunda uongozi bora na kukijengea uwezo kikundi itawezesha kupeleka teknolojia za kilimo kwa usahihi kwa kupitia kushiriki kwenye majaribio kwa kutumia majaribio na mbinu za kujifunza zinazoleta mabadiliko.
3. kuwapatia pembejeo za kilimo zinazohitajika, zana /vifaa, na kuwezesha kikundi cha wakulima walengwa kulingana wa mchanganuo wa mradi.

4. kujumuisha kipengele cha RIPAT cha usambaaji kwenye mradi kwa kuchagua na kuwajengea uwezo wakulima vichocheo (Wv) na kuwajengea uwezo maafisa ugani wa serikali (AU).
5. kutoa taarifa kwa kila robo mwaka kwenye wilaya na kuratibu pamoja na mratibu wa mradi wa wilaya (MMW) wa RIPAT kwa kipindi chote cha utekelezaji.

B. Uongozi wa Wilaya utafanya;

1. kusaidia utekelezaji wa mradi kwa kumteua mratibu wa wilaya wa RIPAT ambaye ndiye atakuwa chanzo cha mawasiliano katika ngazi ya wilaya. Lazima awe tayari kushiriki wakati mikutano ya robo mwaka ya mradi kila inapofanyika na kutoa msaada na ushirikiano.
2. kama italazimika, saidia kukazia sheria za kijiji ambazo zitasaidia teknolojia kuwa endelevu.
3. kuhakikisha kuwa Mratibu wa Wilaya wa RIPAT na maafisa ugani wa serikali wanashiriki mikutano ya kata na kijiji wakati wa mchakato wa uhamasishaji, ikiwa ni pamoja na mikutano ya hadhara kwa kila kijiji wakati wa uundwaji wa vikundi unapofanyika.
4. kuhakikisha kuwa maafisa ugani (kilimo) wanashiriki kwa kadri inavyowezekana kwenye mikutano ya kila wiki ya vikundi vya RIPAT, fanya ufuatiliaaji mara inapohitajika, na wasaidie wakulima vichocheo (Wv) kwenye majukumu yao ya uenezaji wa teknolojia kwa kaya ambazo sio wanakikundi wa RIPAT katika kaya zilizokusudiwa.
5. kuhakikisha maafisa ugani (kilimo) na Mratibu wa Wilaya wa RIPAT anashiriki kwenye kuratibu mikutano ya robo mwaka ikihusisha vikundi vyote
6. kuhakikisha kuwa Maafisa ugani (AU) wanashiriki katika kipengele cha uenezaji wa mradi na kwamba wanafundishwa pamoja na wakulima vichocheo (Wv) jinsi ya uenezaji wa teknolojia bora kwa vijiji vya ziada

## 3. WAKATI WA KUSITISHA MKATABA HUU

A . Kipindi cha mkataba huu ni tarehe.mwezi.mwaka. mpaka tarehe.mwezi.mwaka

B. Mkataba huu unaweza kuvunjwa kwa aidha kwa kuandika notisi kwa upande mwingine angalau siku 30 kabla ya siku rasmi ya kuuvunja.

TAREHE NA SAHIHI

| Kwa niaba ya SLM | Kwa niaba ya serikali ya Wilaya |
|---|---|
| ______________________ | ______________________ |
| Jina | Jina |
| Cheo | Cheo |

KIAMBATANISHO CHA 4E:

# FOMU YA ZIADA YA UFUATILIAJI WA DATA/TAKWIMU KWENYE VIKUNDI

**Fomu ya Ufuatiliaji (uigaji kwa mwanakikundi mmoja mmoja)**

**Mfano: Kilimo Hifadhi (kilimo bora cha mahindi)**

Jina la kijiji ....................... Jina la kikundi.............................. Robo ya mwaka..............................

| | Jina la mwanakikundi | Ameandaa shamba kwa kutumia jembe la chaka/Zambia (Ndiyo/Hapana) | Ameandaa shamba kwa kutumia ripa (Ndiyo/Hapana) | Ametumia mafunika ardhi kuhifadhi udongo (Ndiyo/Hapana) | Ameacha mabaki ya mazao shambani kwa ajili ya kinga ya udongo (Ndiyo/Hapana) | Ametumia kilimo mseto kwa kuchanganya na mazao jamii ya mikunde (Ndiyo/Hapana) | Ametumia mzunguko wa mazao kwa mazao ya jamii ya mikunde (Ndiyo/Hapana) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | |
| 3 | | | | | | | |
| 4 | | | | | | | |
| 5 | | | | | | | |
| ... | | | | | | | |
| 35 | | | | | | | |
| Jumla | | | | | | | |

**Fomu ya Ufuatiliaji (Uigaji kwa mwanakikundi mmoja mmoja)**
**Mfano: Kuku (M2)**

| Jina la kijiji ............................ Jina la kikundi............................ Robo ya mwaka...................... | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Jina la mwanakikundi | Idadi ya majogoo ya kisasa aliyopokea kutoka kwenye mradi | Je, mkulima amejenga banda bora la kuku? (Ndiyo/Hapana) | Je, mkulima anawapa chanjo kuku wake? (Ndiyo/Hapana) | Je, mkulima anawapa kuku chakula bora? (Ndiyo/Hapana) |
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |
| 4 | | | | | |
| 5 | | | | | |
| ... | | | | | |
| 35 | | | | | |
| Jumla | | | | | |

**Fomu ya Ufuatiliaji (Uigaji kwa mwanakikundi mmoja mmoja)**
**Mfano: Mazao [M1]**

| Jina la kijiji .................................. Jina la kikundi............................. Robo ya mwaka.............. | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jina la mwanakikundi | Je, mkulima analima aina iliyoboreshwa ya mihogo? (Ndiyo/Hapana) | Je, Analima aina iliyoboreshwa ya viazi vitamu? (Ndiyo/Hapana) | Je, Analima aina iliyoboreshwa ya ngwara? (Ndiyo/Hapana) | Je, analima aina iliyoboreshwa ya mbaazi? (Ndiyo/Hapana) | Je, analima aina iliyoboreshwa ya mahindi? (Ndiyo/Hapana) |
| 1 | | | | | | |
| 2 | | | | | | |
| 3 | | | | | | |
| ... | | | | | | |
| 35 | | | | | | |
| Jumla | | | | | | |

KIAMBATANISHO CHA 5

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| **AKMW** | Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya |
| **AU(K)** | Afisa Ugani (Kilimo) |
| **KH** | Kilimo Hifadhi |
| **KP** | Kiongozi wa Programu |
| **KMK** | Kamati ya Maendeleo ya Kata |
| **KTM** | Katibu Tawala wa Mkoa |
| **KU** | Kapu la uchaguzi |
| **MHW** | Mkurugenzi wa Halmashauri wa Wilaya |
| **MK** | Mwezeshaji wa Kikundi |
| **MKM** | Mshauri wa Kilimo wa Mkoa |
| **MKU** | Mpango wa Kina wa Utekelezaji |
| **MM** | Meneja wa Mradi |
| **MMW** | Mratibu wa Mradi wa Wilaya |
| **MST** | Mbinu Shirikishi ya Mradi |
| **MU** | Mdhibiti wa Ubora |
| **MwM** | Mkataba wa Maelewano |
| **RECODA** | Research, Community and Organizational Development Associates |
| **RIPAT** | Rural Initiatives for Participatory Agricultural Transformation |
| **SACCOS** | Savings and Credit Cooperative Society (Ushirika wa kuweka na kukopa) |
| **FAO** | Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) |
| **SD** | Shamba la kikundi |
| **AZAKI** | Shirika lisilo la Kiserikali |
| **SLM** | Shirika linalotekeleza mradi |
| **TMHW** | Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya |
| **UKKV/VSLA** | Ushirika wa Kuweka na Kukopa Vijijini |
| **WU** | Wadhibiti Ubora |
| **Wv** | Wakulima Vichocheo |
| **WV** | Wawezeshaji wa Vikundi |

KIAMBATANISHO CHA 6

# Faharasa ya maneno

## WAZO KUU NA MISAMIATI YA KILIMO KATIKA MIRADI YA RIPAT

### *WAZO KUU*

**Kujenga Uwezo** Ni mfumo ambao watu binafsi, mashirika na jamii wanaimarishwa na kudumisha uwezo ili kuweka na kufikia maendeleo ya malengo kwa muda waliojiwekea.

**Kilimo kwenye ardhi kame** Ni kilimo kwenye ardhi isiyo ya umwagiliaji. Mafanikio yanategemea mvua, ulimaji wa kuhifadhi unyevu na mazao yanayovumilia ukame.

**Kuwezesha** Ni mchakato wa utaratibu ambao mtu/watu anapata kujiamini na kujisikia kuweza zaidi kuchagua kipaumbele na jinsi ya kutekeleza alichokipanga.

**Upanuzi/Uenezaji** Kwenye mwongozo huu, uenezaji unaeleweka kama huduma za kiserikali zilizobuniwa ili kuendeleza ujuzi unaotegemea utafiti na teknolojia inayofaa vijijini ili kuboresha maisha ya wakulima.

**Uwezeshaji** Ni kusaidia kikundi cha watu kufikia malengo kupitia majadiliano, kutia moyo na kusaidia kupanga na kutenda.

**Mwenendo wa kikundi** Ni muingiliano ambao unaleta fikra na tabia za watu pamoja wanapokutana na wengine. Mwenendo wa kikundi inahusiana na jinsi vikundi vinavyoanzishwa, muundo wake, utaratibu wake na ufanyaji kazi wake. Mara nyingi inasaidia kuboresha mwenendo wa kikundi iwapo michezo na mazoezi itatambulishwa wakati wa majadiliano ya kikundi.

**Mbao mantiki** Ni kipimo ambacho menejimenti inatumia kuboresha teknolojia, mara nyingi kwenye ngazi ya mradi. Inahusisha kutambua mambo ya kimkakati (pembejeo, pato/zao, matokeo, athari) na mahusiano yake, viashiria, na dhana/wazo au hatari zitakazosababisha mafanikio na kushindwa. Kwa hiyo, inawezesha kupanga, kutekeleza na kutathimini shughuli za maendeleo.

**Uhamasishaji** Vitendo vinavyokusudia kuwatia moyo watu kuwa pamoja ili kusaidia wazo fulani lililolengwa ili kufikia lengo. Inaweza kuelezwa kama mchakato wa kusisimua na wa kutia moyo na kusaidia jamii kutambua hali zao na kuchukua hatua ya kufanya kazi pamoja ili kubadilisha maisha yao.

**Ufuatiliaji** Mchakato wa uangaliaji kwa vipindi tofauti ambao unaangalia kama viwango na malengo yaliyowekwa kwenye mpango yamefikiwa kwa vitendo. Taarifa inatumiwa na uongozi ili kufanya maamuzi.

**Mti wa malengo** Kielelezo cha mchoro wa hali ya baadaye wakati ambapo tatizo linapokuwa limerekebishwa, ikifuatiwa na uchanganuzi wa programu na kuonyesha mwisho wenye kuleta maana.

**Umiliki** Wakati wananchi/wanajamii wanapochukua uthibiti na kukubali majukumu kwa mambo ambayo yataleta maendeleo yao binafsi.

**Mbinu Shirikishi ya Tathmini** (MST) Mfumo ambao umelenga kujumuisha maarifa na maoni ya watu wa vijijini katika kupanga na kusimamia maendeleo ya miradi.

**Uchanganuzi wa matatizo** ni uchunguzi maalum wa mitazamo hasi ya athari ili kujua visababishi na madhara yake.

**Mti wa matatizo** ni mchoro wa mfano wa hali hasi, ikionesha uhusiano wa chanzo – athari.

**Uhamasishaji** ni kitendo cha kujaribu kuwa na uelewa wewe mwenyewe au wengine na kuitikia juu ya mawazo fulani, matukio, hali, au jambo; uanzishaji wa uelewa wa hali iliyoko ili kuhimiza mabadiliko chanya kwenye siku za usoni na utayari wa kutenda.

**Mnyororo wa mgawanyo** kwenye RIPAT, aina mbili za mnyororo wa mgawanyo hutumika. 1) mnyama (mbuzi, kondoo na nguruwe). Kila kikundi hupewa wanyama majike na madume wa kisasa halisi kama wazazi wa mwanzo walioboreshwa. Wanachama hugawa mtoto wa kwanza jike kwa wengine kwenye kikundi kulingana na orodha iliyoandaliwa na kikundi. Ni pale tu ambapo mtu atakuwa amegawa watoto majike kwa mtu aliyeko kwenye orodha ndipo mnyama jike wa kwanza atakuwa kwenye miliki ya mwanakikundi aliyempokea wa kwanza. 2) Mgomba. Kila mkulima achaguaye teknolojia ya migomba iliyoboreshwa anatarajiwa kutoa kwa wakulima wengine wanaopendelea ndani ya jamii mara tatu ya idadi ya machipukizi ya migomba aliyopokea kutoka mradini na kuwafundisha katika mbinu za kilimo zilizoboreshwa.

**Wakulima vichocheo** ni watu ambao, wakati wa muda wa utekelezaji wa mradi, wametambulika kama watu ambao wameibuka kama wajasiriamali jamii na mawakala wa mabadiliko. Ni wakulima waliofanikiwa toka ndani ya kikundi ambao wamepata ujuzi kupitia mafunzo ya RIPAT na kwa mafanikio wametekeleza angalau teknolojia moja iliyoletwa na RIPAT.

**Uendelevu** ni uendelezaji wa faida kutoka teknolojia ya maendeleo baada ya usaidizi wa awali wa maendeleo umeshakamilishwa; uwezekano wa faida endelevu za muda mrefu.

**Kundi lengwa** ni watu maalum au mashirika ambao kwa ajili yao maendeleo ya teknolojia za mradi hufanyika.

**Pengo la kiteknolojia** ni pengo kati ya uzalishaji shambani uliofikiwa kwa kutumia teknolojia za sasa za kilimo wanazotumia wakulima na uzalishaji ambao ungefikiwa. Wakulima wanahitaji teknolojia nzuri zaidi, za kisasa na kuwa na uwezo wa kuweza kuzibadili kuendana na mazingira. Pengo husababishwa na ukosefu wa mbinu za ujuzi na mafunzo ya matumizi yake, na kutofikia vifaa na pembejeo za kilimo kwa ajili ya kutekeleza teknolojia nzuri zaidi.

*Misamiati katika kilimo*

**Kilimo – Ufugaji** ni utegemezi wa kaya kwenye mchanganyiko wa kilimo na ufugaji wa wanyama kwa ajili ya maisha yao.

**Zao la msimu** ni zao ambalo hulimwa kwa msimu mmoja tu (au mwaka) kabla halijafa, kinyume na zao la kudumu, ambalo hudumu kwa zaidi ya msimu mmoja.

**Mgomba (aina iliyoboreshwa kwenye RIPAT)** aina za migomba zilizoboreshwa, Grand Nain, Paz, Chinese, Williams, na Lakatan zilijaribiwa na kuonyeshwa kwa ajili ya RIPAT. Kwa baadhi ya maeneo aina ya asili Mshale ilitumika kwa ajili ya kulinganisha. Aina hizi za migomba iliyoboreshwa zilichaguliwa na kuletwa na mratibu wa migomba Tanzania kwa ajili uzalishaji wa juu, uhakika wa chakula, na mauzo ikijumuisha kuuza

nje ya nchi. Aina ya migomba iliyoboreshwa inaweza kutumika kwa ajili ya kupika na matunda, na inavumilia ukame kwa kiasi kikubwa, maji yaliyotuama na magonjwa.

**Mche wa mgomba** Machipukizi yanayotoka kuzunguka shina la mmea mkuu yanayounda kifungu kinachoitwa 'mche' chipukizi kubwa linachukua nafasi ya mmea mkuu wakati unapotoa matunda na kufa; mchakato wa kuchukua nafasi ya mmoja baada ya nyingine unaendelea bila kukoma.

**Machipukizi ya migomba** Ni vipandikizi vinavyotolewa kutoka kwenye mmea mama. Migomba inazalishwa kutokana na mgomba mama (kuzaa mimea mingi zaidi) kutokana na machipukizi (au uzalishaji wa kimaabara). Kama machipukizi hayatatolewa yatakuwa yanashindana na mmea mama na hivyo kupunguza mavuno.

**Jembe la chaka (la kizambia)** jembe la chaka linatangazwa katika kilimo hifadhi kwa kupunguza kugeuza ardhi kama mbadala wa kilimo cha asili (kienyeji) cha jembe la mkono. Linatumika kulima sehemu zile tu ambapo mbegu itapandwa, kufanya mashimo ya kudumu ya kupanda. Ni jembe zito imara zaidi lenye ubapa mrefu na mpini mrefu unaoweza kuzungushwa kupunguza nguvu, hivyo kufanya kuwe na uwezekano wa kuandaa mashimo kipindi cha ukame wakati udongo ni mgumu. Mashimo yana kina cha sm 20 na urefu wa sm 30, na nafasi ya sm 70 kati ya shimo na shimo kwenye mstari. Kati ya mstari na mstari ni sm 90. Kila mwaka mashimo yanachimbwa tena sehemu ile ile kama ilivyokuwa mwaka uliopita.

**Kilimo hifadhi (KH)** katika muktadha wa RIPAT, mbinu ya kilimo inayotilia mkazo juu ya kanuni tatu inayokusudia kuzalisha mazao mengi wakati ikipunguza gharama za uzalishaji, kudumisha rutuba ya udongo, na kuhifadhi maji. Kanuni tatu ni 1) kusumbua udongo kidogo kidogo iwezekanavyo (kupunguza kulima kwa kutumia jembe la chaka au ripa), 2) kuacha udongo ukiwa umefunikwa kadiri iwezekanavyo (kutumia matandazo na au mazao funiko), na 3) kutumia kilimo mseto na mzunguko wa mazao.

**Mfunika ardhi** Mazao yanayotumika kufunika na kuzuia uso wa udongo kupunguza mmomonyoko na kuwekea ardhi kivuli. Mmea unaokua haraka utumike, kwa kawaida mkunde. Katika RIPAT mikunde aina ya mucuna na ngwara inatangazwa kama mazao funika.

**Mzunguko wa mazao** Kupanda mazao tofauti kwa vipindi vinavyofuatana kwenye shamba moja, ili kuhifadhi uwezo wa udongo kuzalisha (kuepuka kupunguza virutubisho vya udongo, na kudhibiti magugu, magonjwa, na wadudu).

**Kilimo mseto** Kupanda mazao mawili au zaidi katika shamba moja kwa wakati mmoja, ama kwa kuchanganya pamoja au katika mistari au maeneo yaliyogawanywa, kwa mfano mbaazi na mahindi.

**Mkunde** Mimea ambayo inajulikana kwa uwezo wake wa kugeuza nitrojeni iliyo hewani kibaiolojia na uwezo wake kuboresha rutuba ya udongo kupitia kuchukua nitrojeni. Ni mazao muhimu katika mzunguko wa mazao na kilimo mseto. Ubora wake wa kuwa na kiasi kikubwa cha protini kwenye mbegu na majani unafanya mikunde kuhitajika kwa matumizi ya wanyama na binadamu. Katika RIPAT, mikunde mbalimbali imekuwa ikitangazwa, ikijumuisha ngwara, mkuna, mbaazi, soya, na kunde.

**Matandazo** Tabaka la mimea iliyokufa kama vile nyasi kavu, majani, na masalia ya mimea, yanayoachwa ili kufunika ardhi kwa lengo la kuzuia mmomonyoko wa udongo,

inayosaidia kupenyeza kwa maji ya mvua (kupunguza mtiririko wa maji), kuhifadhi unyevu (kupunguza mvukizo wa unyevu), na kupunguvu ukuaji wa magugu.

**Zao la kudumu** Ni zao linalokua zaidi au kidogo zaidi kutoka mwaka hadi mwaka (kwa mfano mgomba).

**Ripa** Ni kifaa kinatangazwa katika kilimo hifadhi kwa kupunguza kulima udongo kama mbadala kwa kilimo cha jadi cha kutumia jembe la plau la kukokotwa na ng'ombe. Kina fremu na jino refu lililojishikiza kwa ajili ya kuvunja udongo uliogandamana na kisahani kigumu cha udongo na kutengeneza mitaro ya kupandia. Mistari iliyotengenezwa kwa ripa, kawaida nafasi ni sm 75-90, inachimbwa kwa umbali iwezekanavyo katika sehemu ile ile kila mwaka, na udongo unaobakia katikati ukibakia haujaguswa/haujalimwa.

**Mazao ya mizizi** Ni kundi la mimea lililo kwa familia mbalimbali likiwa na tunguu chini ya ardhi au upande wa mizizi. Ni vyakula vikuu muhimu katika maeneo mengi ya tropiki, yanapandwa kwa ajili ya wanga. Mazao ya mizizi kimsingi yanazalishwa kutoka kwenye tunguu au vijiti (sehemu za mashina). Katika RIPAT, aina bora za viazi vitamu na mihogo zinatangazwa, hasa karibuni, kwa sababu ya uwezo wake wa kuzaa kwenye mazingira magumu na udongo ambao siyo mzuri na kuwa kama zao hifadhi wakati wa njaa.

**Mtiririko wa maji** Ni sehemu ya maji ya mvua ambayo hayaingii kwenye ardhi na yanatoka au 'kupotea' kutoka kwenye eneo kupitia mifereji/mitaro na njia za maji.

**Matuta ya kufunga** Vibwawa vidogo vinavyotengenezwa kwa udongo vyenye vipimo maalumu vya mpishano kwenye mitaro ili kuteka maji ya mvua na kuzuia kutiririka kufuata kontua (mbinu ya kuhifadhi maji).

**Kuhifadhi maji** Kuzuia, kuendeleza, na usimamizi fanisi wa rasilimali maji kwa ajili ya faida za makusudi. Katika RIPAT, teknolojia za kilimo zilizoboreshwa zinatangazwa kupunguza upoteaji wa maji kupitia kutiririka ardhini ( kwa mfano, kutumia matuta ya kufunga, kilimo cha kontua) na mvukizo (mfano kutumia matandazo).

*Muundo wa kiutawala wa Seriakali ya Tanzania*

**Mkoa** Tanzania imegawanyika katika mikoa 30, kila mmoja ukiwa na wilaya kadhaa
**Wilaya** Kuna wilaya 130 katika nchi ya Tanzania, kila wilaya ikiwa na idadi kadhaa ya kata
**Kata** Kuna kata zaidi ya 700 Tanzania. Hasa kata inakuwa na vijiji viwili hadi vinne.

*Viongozi wa vijiji*

Katika huu mwongozo, neno 'viongozi wa vijiji' linahusu watu wawili muhimu

- Mwenyekiti wa kijiji, ambaye anachaguliwa na wanajamii husika
- Afisa Mtendaji wa kijiji, ambaye huajiriwa na serikali

KIAMBATANISHO CHA 7

# Kilimo cha migomba kwenye miradi ya RIPAT

## *Kwa nini?*

Migomba ni mojawapo ya mazao yaliyobainishwa na RECODA kuwa na umuhimu wa kutosha kwa ajili ya usalama wa chakula, kipato na uboreshaji wa mazingira. Inatoa faida nyingi sana ukilinganisha na mazao mengine. Kwa mfano, 1) ni zao la chakula na biashara na linatoa mazao muda wote wa mwaka; 2) linatoa ajira kipindi chote cha mwaka – tofauti na mazao ya mwaka kama vile mahindi, ambayo yanahitaji mahitaji ya kazi za msimu; 3) Inatoa kiasi kikubwa cha uzalishaji wa chakula kwa eneo kwa mwaka ukilinganisha na mahindi na mazao mengine; 4) Inafaa sana kwenye muzunguko wa mazao na mifugo, ambapo wanyama wanatoa mbolea na masalia ya migomba ni chakula cha wanyama; 5) ni zao la kudumu linalongeza uwezo wa uzalishaji kwa miaka mingi kwenye maeneo ambayo kuna utofauti wa mvua; na 6) linaboresha mazingira kwa kufunika udongo mwaka mzima.

## *Wapi?*

Kwa ujumla, migomba inatoa mazao mazuri kwenye eneo ambalo lina mvua za wastani 1200 mm kwa mwaka, kiwango cha mwinuko wa mita 1800 kutoka usawa wa bahari. Udongo unaofaa ni ule wenye rutuba, kina (mita 2) na ambao haujaathiriwa na magadi (kiwango cha pH kati ya 5 na 8). Migomba mara nyingi inaelezewa isivyostahili kama zao linaloweza kuzalishwa kwenye eneo lenye mvua za kutosha au umwagiliaji. Hata hivyo mavuno mengi yanaweza kupatikana kwenye udongo ambao ni mzuri zaidi, wenye maji na hali ya hewa nzuri, baadhi ya aina za migomba inavumilia ukame

Fursa za kuendeleza aina za migomba kwenye miradi ya RIPAT lilitokana na matokeo yaliyopatikana baada ya utafiti uliofanywa na Chuo cha Utafiti wa Kilimo Selian (SARI) kilichopo Arusha kwenye aina mpya zilizoletwa Tanzania kama mbegu za kuzalisha maabara. Kutokana na matokeo mazuri ya mwanzoni ya SARI, RECODA iliamua kufanya mradi wa majaribio ili kuona umuhimu wake chini ya hali ya shamba. Mradi wa majaribio ulifanyika kwenye maeneo mawili: kwenye eneo zuri, lenye mvua za kutosha na uwezekano wa umwagiliaji; na kwenye eneo lisilokuwa zuri, lisilo na mvua za kutosha na ambapo wakulima wanalima kwenye ukame. Maeneo haya mawili baadaye yalikuja kuwa maeneo ya RIPAT 1 na RIPAT 2. Mradi wa majaribio ulidhihirisha kwamba aina mpya ya migomba inafanya vizuri sana kwenye eneo la RIPAT 1 na kuwa wanaweza kulima kwenye maeneo kame na magumu ya RIPAT 2. Kupitia uzoefu wa RIPAT, ilionekana kwamba kilimo kwenye maeneo ambayo ni kame ni muhimu kuchagua maeneo yanayofaa, hii ni kwenye maeneo ya mabondeni ambayo yana zuia upepo na kwenye uwezekano wa kuvuna maji. Vile vile, kupunguza msongamano wa mimea, kuongeza ukubwa wa shimo la kupandia na kutumia kiasi kikubwa cha mbolea pamoja na kuweka matandazo jambo ambalo litasaidia kufanikiwa kwa kilimo cha migomba kwenye maeneo kame. Ilionekana kwamba unapolima kwa kutumia mbinu bora za kilimo, migomba inaweza kuvumilia ukame zaidi kuliko mazao ya msimu kama vile mahindi.

## *Kwa jinsi gani?*

Inahitajika kazi kubwa unapoanza kupanda migomba. Kwa kutumia kipimo kinachopendekezwa cha nafasi ya mita 3 kati ya mstari na mstari na mita 3 kati ya mmea na mmea kwenye mistari, mashimo 450 yanaweza kuwepo kwenye kila eka 1. Shimo la mgomba linakuwa na kina cha sm 90 na upana wa sm 90 (ambazo ni sawa na mita za ujazo 0.6). Wakati wa kuchimba shimo, udongo wa juu (sm 45) unatenganishwa na ule wa chini. Baada ya kumaliza kuchimba, udongo wa juu unachanganywa na ndoo 5 mpaka 10 za samadi au mbolea na halafu unaurudisha kwenye shimo.

Migomba inaweza kupandwa muda wote kipindi cha mvua; hata hivyo, inabidi kupanda kiutaalamu na bila kuwepo upungufu wa maji kwa miezi minne mpaka sita ya kwanza baada ya kupanda. Kwahiyo, upandaji usifanyike miezi ya mwishoni ya msimu wa mvua. Machipukizi lazima yawe yenye afya, yasiyo na magonjwa wala wadudu. Matumizi ya miche inayotokana na kuzalisha mbegu za kupandikiza maabara ndio inapendekezwa zaidi, lakini bado haijaweza kupatikana nchini Tanzania. Kwa kuongezea kilichoelezwa hapo juu wakulima wanatakiwa kufundishwa mbinu za 1)kuondoa machipukizi na kuandaa vifaa vizuri vya kupandia; 2) kuepuka na kukabiliana na wadudu na magonjwa; 3) kutumia samadi na mbolea na kumwagilia (kama inawezekana) 4) uvunaji, usindikaji na masoko.

KIAMBATANISHO CHA 8

# Rejea na kusoma zaidi

Katika kuandika huu mwongozo, waandishi wamerejea miongozo na nyaraka nyingine. Nyaraka muhimu zaidi zimeorodheshwa chini na zinapendekezwa kwa kusoma zaidi. Orodha pana zaidi ya marejeo inatolewa katika kitabu kinachoitwa Chaguo la mkulima: Kutathmini mbinu ya uchukuaji wa teknolojia ya kilimo Tanzania (Lilleør and Lund-Sørensen, 2013).


Anderson J. R., Feder G. na Ganguly S. (2006) *The Rise and Fall of Training and Visit Extension: An Asian Mini-drama with an African Epilogue.* World Bank Policy Research Working Paper 3928, World Bank, Washington, D.C.

Braun A. na Duveskog D. (2008) *The Farmer Field School Approach – History, Global Assessment and Success Stories.* Background Paper for the IFAD Rural Poverty Report 2010, International Fund for Agricultural Development, Rome.

Carter, I. (2003) *Mobilising the community: A PILLARS guide.* Teddington, UK: Tearfund. Available at: <http://tilz.tearfund.org/Publications/PILLARS/Mobilising+ the+commu nity/>

FAO (1994) *The group promoter's resource book. A practical guide to building rural self-helpgroups,* Rome: Food and Agriculture Organization of the United Nations.

FAO (2001) *The inter-group resource book,* Rome: Food and Agriculture Organization of the United Nations.

Gallagher, K., Braun A. na Duveskog D. (2006). 'Demystifying Farmer Field School Concepts'. Paper prepared in response to Journal of International Agricultural and Extension Education paper by K. Davis, 15(3). Available from www.share4dev.info/ffsnet/documents/3200.pdf [accessed 24 January 2013].

Gautam, M. (2000) *Agricultural extension: the Kenyan experience: An impact evaluation.* World Bank, Washington, DC.

Groeneweg, K., Buyu, G., Romney, D. na Minjauw, B. (2006) *Livestock farmer field schools – Guidelines for facilitation and technical manual,* Nairobi: International Livestock Research Centre.

Lilleør, H.B. and Lund-Sørensen, U., eds (2013)*Farmers' choice: Evaluating an approach to agricultural technology adoption in Tanzania.* Rugby: Practical Action Publishing, and Copenhagen: Rockwool Foundation Research Unit.

MoA (2012) *Participatory extension approaches (PEA) in Zimbabwe,* Harare: Ministry of Agriculture, Mechanisation and Irrigation, Development, and Practical Action, Southern Africa.

Okoth, J.R., Nalyongo, W. and Bonte, A. (2010) *Facilitators' guide for running a farmer field school: An adaptation to a post emergency recovery programme.* Kampala: FAO Uganda.

Osborne, D. na Gaebler, T. (1992). *Reinventing government: How the entrepreneurial spirit is transforming the public sector.* Reading, MA: Addison-Wesley Publishing.

Paldam, M. (1997) *Dansk U-Landshjælp. Altruismens politiske økonomi (Danish Foreign Aid. The economic realities of altruism).* Aarhus: Aarhus University Press.

VSLA (no date) *Vilage savings and loan associations (VSLAs). Field officer training guide,* Version 1.03, Solingen: VSL Associates, available from Hugh Allen, hugh@vsla.net

# MWONGOZO WA RIPAT

Sehemu ya kusini mwa jangwa la Sahara imebaki kuwa eneo ambalo linaathirika sana na uhahaba wa chakula pamoja na kuwa na uwezo mkubwa wa kilimo. Katika jitihada za kuchangia kuondoa tatizo hili, mfumo wa kupeleka maendeleo vijijini unaoitwa RIPAT (Rural Initiatives for Participatory Agricultural Transformation) umebuniwa kwa muda tangu mwaka 2006 kupitia mfululizo wa miradi Kaskazini mwa Tanzania.

Mwongozo wa RIPAT unaelezea hatua kwa hatua jinsi ya kuratibu na kutekeleza mradi imara wa maendeleo ya kilimo unaotekelezwa kupiatia kikundi na unasifika kwa:

- KUSAIDIWA ILI KUJIMUDU NA KUSAIDIA WENGINE– kuepukana na UTEGEMEZI KWA WAFADHILI na kuhakikisha wakulima wanachukua jukumu kamili la kujiletea maendeleo yao wenyewe
- matumizi ya mashamba ya kikundi ya kujifunzia ambapo RIPAT huchukua MAZURI KUTOKA MFUMO WA CHINI kwenda JUU NA MFUMO WA JUU kwenda CHINI
- huwapatia wakulima UCHAGUZI wa teknolojia za kilimo na SAUTI kuhusu jinsi ya kujipanga kama kikundi na kufanya kazi pamoja
- USHIRIKIANO RASMI na serikali za mitaa na huduma za ugani kwa lengo la kuendeleza na kusambaza miradi.

'Huu ni mwongozo mzuri sana wa hatua-kwa-hatua na rahisi kufuata unaohusu namna mashirika yanayofanya kazi na wakulima wadogo wadogo yanavyotakiwa yafanye kazi zao. Kitabu hiki ni rasilimali ya lazima kwa watoa huduma ya ugani wote na wafanyakazi wote wa maendeleo vijijini kuwa nayo, iwe wanatoka serikalini au taasisi zisizo za kiserikali. Kwa muda mrefu hapajawahi kuwa na mwongozo wowote nchini Tanzania wa kuongoza kazi ya ugani. Mwongozo huu kwa hakika utaziba pengo hilo.'

*Profesa Amon Z. Mattee, Idara ya Elimu ya Kilimo na Ugani, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro, Tanzania*

'Katika wilaya za Arumeru na Karatu nilishuhudia wakulima wakitumia mfumo wa RIPAT kuongeza tija na kipato chao kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji wa ndizi; kuboresha kiwango chao cha uvumbuzi, ushiriki na umiliki wa miradi yao; na hivyo kubadili maisha yao. Mfumo pia umetatua suala la utegemezi kwa wafadhili wa wakulima na uhimizaji wa matumizi ya kanuni iliyo bora kabisa ya kujitegemea katika maendeleo yao.'

*Mh. Isidore Leka Shirima, Mkuu wa Mkoa mstaafu wa Arusha, Tanzania*

ROCKWOOL FONDEN
ROCKWOOL FOUNDATION